# Kiswahili

## Kwa Vyuo Vya Ualimu

### Kitabu Cha Mwanafunzi

**2**

**MCHEPUO WA ELIMU YA LUGHA (LE)**

© 2020 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# VIFUPISHO

**n.k:** na kadhalika

**k.v:** kama vile

**tnbh:** tanbihi

**m.f:** mfano

**agh:** aghalabu

**Bi:** Bibi

**Bw:** Bwana

**S.L.P:** Sanduku la Posta.

# Dibaji

Mwanafunzi mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima ya kuwasilisha Kitabu cha Kiswahili cha Mwanafunzi wa mwaka wa pili, mchepuo wa Elimu ya Lugha katika Vyuo vyaUalimu.

Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri maisha yake na kumpa fursa ya kujipatia ajira au kuandaa miradi mbalimbali kulingana na mahitaji ya jamii anamoishi.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza kuhusu umuhimu wa kufungamanisha shughuli za ujifunzaji na ufundishaji pamoja na zana na mitaala ili kufanikisha mchakato mzima wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale yanayofundishwa na uwezo waupatao wanafunzi. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Hivyo basi, kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza unaokuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti ya kibinafsi na yale utakayofanya katika makundi kwa msaada wa wakufunzi ambao huwajibika kufanikisha ufundishaji. Aidha, utapata stadi muhimu zitakazokuwezesha kutumia yale uliyojifunza katika miktadha mbalimbali ya maisha halisi ili uweze kuonyesha tofauti siyo tu katika maisha yako bali hata kwa taifa.

Mwelekeo uliozingatiwa katika kitabu hiki unatofautiana na ule uliotiliwa maanani katika mfumo wa zamani ambapo mchakato wa kujifunza ulifanywa kwa kutilia mkazo upataji wa maarifa kutoka kwa mkufunzi ambaye pia alifikiriwa kumzidi mwanafunzi.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi, maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi. Kwa hivyo, dhana huanzishwa aghalabu kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na kupata maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya ujifunzaji hujihusisha na shughuli mbalimbali zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri kuhusu yale anayoyafanya, kuonyesha uzoefu wake halisi na maarifa aliyonayo katika mchakato huo wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, utakuwa na majukumu yafuatayo ili uweze kutumia kitabu hiki kwa ufanisi:

- Kuendeleza maarifa na stadi kwa kufanya kazi, mazoezi yanayolenga kwenye mada. Kuwasiliana na kupeana taarifa sahihi pamoja na wanafunzi wengine kupitia mawasilisho, mijadala, kazi za makundi na mbinu nyingine za ufundishaji kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, uchunguzi na utafiti katika maktaba, mitandao na hata nje ya shule.
- Kushiriki na kuwajibika kuhusu ujifunzaji wako na kufanya utafiti, uchunguzi kwenye maandishi yaliyochapishwa /mtandaoni, wataalamu na kuwasilisha matokeo ya utafiti.
- Kuhakikisha ufanisi mzuri wa mchango wa kila mwanakundi katika kazi ulizopewa kupitia maelezo na majadiliano kila unapoongea hadharani.
- Kutoa hitimisho sahihi kuhusu matokeo ya utafiti uliotokana na mazoezi yako ya ujifunzaji.

Mwishowe, ningependa kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki na kutoa mchango wao kwa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioongoza mchakato wa kazi hii tokea ilipoanza.

Pongezi muhimu ziwaendee walimu kutoka shule tofauti kwa kuendeleza na kufanikisha kazi hii. Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki. Kitabu hiki kisingeliwezekana kufanikiwa bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu ziwaendee viongozi wa shule mbalimbali walioruhusu walimu wao kufanya kazi na Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi katika mradi wa ukamilishaji wa kitabu hiki. Napenda kutoa shukrani zaidi kwa walimu ambao juhudi zao na uandikaji wa kitabu hiki ulikuwa wa thamani.

Mwishowe, shukrani ziwaendee wafanyakazi wote wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (CTLR-REB) walioshiriki katika mchakato wa kufanikisha uandikaji wa kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

# YALIYOMO


**VIFUPISHO** .......... iii

**DIBAJI** .......... iv

**SHUKRANI** .......... vi

**UTANGULIZI** .......... 1

**MADA YA 1: MIDAHALO** .......... 3

**SOMO LA 1: MAANA YA MDAHALO** .......... 4

1.1. Kusoma na ufahamu: Hali ya maisha ya wasichana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya karne zilizopita .......... 4

1.2. Msamiati kuhusu mdahalo .......... 9

1.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI .......... 10

1.4. Matumizi ya lugha: Maana ya mdahalo .......... 12

1.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 13

1.6. Kuandika .......... 13

**SOMO LA 2: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO** .......... 14

2.1. Kusoma na ufahamu: Dawa za Kulevya Ndilo Tatizo Linaloathiri Maendeleo ya Vijana .......... 14

2.2. Msamiati kuhusu "Mdahalo" .......... 21

2.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya ngeli ya U-ZI: vivumishi vya kuonyesha, kumiliki, kuunganisha na kurejesha .......... 22

2.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na utekelezaji wa Mdahalo .......... 23

2.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 25

2.6. Kuandika .......... 25

**MADA YA 2: MIJADALA** .......... 26

**SOMO LA 3: MAANA YA MJADALA** .......... 26

3.1. Kusoma na ufahamu: Maana ya mjadala .......... 27

3.2. Msamiati kuhusu maana ya mjadala .......... 29

3.3. Sarufi kuhusu ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vya kuuliza .......... 30

3.4. Matumizi ya lugha: Maana ya mjadala .......... 31

3.5. Kusikiliza na Kuzungumza .......... 32

3.6. Kuandika .......... 32

**SOMO LA 4: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA . 33**
4.1. Kusoma na ufahamu: Mchango wa wazazi katika malezi ya watoto wao ........ 33
4.2. Msamiati kuhusu “Maandalizi na utekelezaji wa mjadala” ....... 37
4.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi visisitizi . 38
4.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na utekelezaji wa mjadala ....... 39
4.5. Kusikiliza na Kuzungumza ........ 40
4.6. Kuandika ........ 40
**MADA YA 3: UTUNGAJI WA BARUA ZA KIRAFIKI, MWALIKO NA MATANGAZO ........ 42**
**SOMO LA 5: BARUA YA KIRAFIKI ........ 44**
5.1. Kusoma na ufahamu: Barua ya kirafiki ........ 44
5.2. Msamiati ........ 45
5.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU ........ 46
5.4. Matumizi ya lugha ........ 47
5.5.Kusikiliza na kuzungumza ........ 49
5.6. Kuandika ........ 49
**SOMO LA 6: BARUA YA MWALIKO ........ 50**
6.1.Kusoma na ufahamu: Ndoa ya dadangu ........ 50
6.2.Msamiati ........ 51
6.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vyake ..... 52
6.4. Matumizi ya lugha: Maana ya barua ya mwaliko ........ 53
6.5.Kusikiliza na kuzungumza ........ 55
6.6.Kuandika ........ 55
**SOMO LA 7: MATANGAZO ........ 55**
7.1. Kusoma na ufahamu: Laiti ningefuata tangazo redioni ........ 56
7.2. Msamiati kuhusu uandishi wa matangazo ........ 58
7.3.Sarufi : Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vyake ..... 58
7.4. Matumizi ya lugha: Maana ya tangazo ........ 59
7.5. Kusikiliza na kuzungumza ........ 60
7.6. Kuandika ........ 60

**MADA YA 4: UTUNGAJI WA INSHA ZA WASIFU.........................61**
**SOMO LA 8: INSHA ZA WASIFU ...................................................62**
8.1. Kusoma na ufahamu: Insha za wasifu .......................................62
8.2. Msamiati kuhusu insha za wasifu ..............................................63
8.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi cha hali -KA-..............................64
8.4. Matumizi ya lugha: Insha za wasifu..........................................64
8.5. Kusikiliza na kuzungumza.......................................................66
8.6. Kuandika .................................................................................66
**SOMO LA 9: MATUMIZI YA ALAMA ZA VITUO ............................67**
9.1. Kusoma na ufahamu: Nchi ya Rwanda .....................................67
9.2. Matumizi ya msamiati kutoka kifungu cha habari ....................69
9.3. Sarufi kuhusu matumizi ya alama za vituo/uakifishaji.............70
9.4. Matumizi ya lugha ....................................................................73
9.5. Kusikiliza na kuzungumza.........................................................73
9.6. Kuandika ...................................................................................73
**MADA YA 5: HOTUBA.................................................................75**
**SOMO LA 10: MAANA YA HOTUBA .............................................76**
10.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Meya baada ya kazi za Umuganda ......................................................................................76
10.2. Msamiati kuhusu hotuba ya Meya ..........................................77
10.3. Sarufi: Alama za uandishi na matumizi yake ........................79
10.4. Matumizi ya lugha: Mambo muhimu katika hotuba ................80
10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .................................81
10.6. Kuandika: Utungaji wa hotuba................................................81
**SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA..........................................81**
11.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Mukuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano .........................................................81
11.2. Msamiati kuhusu hotuba ........................................................83
11.3. Sarufi: Alama za uandishi na matumizi yake ........................84
11.4. Matumizi ya lugha: Sifa za hotuba .........................................85
11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .................................86
11.6. Kuandika: Kuandika maelezo mafupi .....................................86

**MADA YA 6: UANDISHI WA RIPOTI ............................................ 87**

**SOMO LA 12: RIPOTI ........................................................................ 88**

12.1. Kusoma na ufahamu: Ripoti ................................................ 88

12.2. Msamiati kuhusu ripoti ...................................................... 89

12.3. Sarufi: Alama za vituo na matumizi yake ............................... 90

12.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu ripoti ............... 93

12.5. Kusikiliza na Kuzungumza ................................................. 93

12.6. Kuandika: Utungaji wa ripoti .............................................. 94

**SOMO 13: MFANO WA RIPOTI ZA MKUTANO ............................ 94**

13.1. Kusoma na ufahamu: Mfano wa ripoti za mkutano ................. 94

13.2. Msamiati kuhusu mfano wa ripoti ........................................ 96

13.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo ....................................... 96

13.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu uandishi wa ripoti .. 97

13.5. Kusikiliza na kuzungumza .................................................. 98

13.6. Kuandika ......................................................................... 98

**MADA YA 7: HISTORIA YA LUGHA YA KISWAHILI .................... 99**

**SOMO LA 14: ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI ........................ 100**

14.1. Kusoma na ufahamu : Asili ya lugha ya Kiswahili ................ 100

14.2. Msamiati kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili ....................... 102

14.3. Sarufi: Aina za sentensi ................................................... 103

14.4. Matumizi ya lugha: Mitazamo tofauti kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili ........................................................................... 105

14.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .............................. 105

14.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari .......................... 105

**SOMO LA 15: KUENEA KWA LUGHA YA KISWAHILI ............... 106**

15.1. Kusoma na ufahamu: Kuenea kwa lugha ya Kiswahili .......... 106

15.2. Msamiati kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili na mabadiliko yake ............................................................................... 108

15.3. Sarufi kuhusu aina za sentensi/tungo ................................. 110

15.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili ........................................................................ 111

15.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano .............................. 113

15.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari .......................... 113

**MADA YA 8: MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI ........................................................ 114**
**SOMO LA 16: MATUMIZI YA MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI ........................................................ 115**
16.1. Kusoma na ufahamu: Mutesa aingia benkini ........................ 115
16.2. Msamiati kuhusu mazungumzo ........................................ 117
16.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi hali -ki- ............................. 118
16.4. Matumizi ya lugha: Msamiati wa benkini ........................... 119
16.5. Kusikiliza na kuzungumza ................................................ 121
16.6. Kuandika ....................................................................... 121
**SOMO LA 17: REJESTA ........................................................ 122**
17.1. Kusoma na ufahamu: Mchezo wa kusisimua ........................ 122
17.2. Msamiati kuhusu kifungu cha habari ................................. 124
17.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya ku-na vivumishi vyake . 124
17.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu rejesta ........... 125
17.5. Kusikiliza na kuzungumza ................................................ 127
17.6. Kuandika ....................................................................... 128
**MADA YA 9: KISWAHILI NA TEKNOLOJIA ............................... 129**
**SOMO LA 18. MATUMIZI YA TARAKILISHI NA VYOMBO VYA HABARI ........................................................ 131**
18.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi ya tarakilishi ...................... 131
18.2. Msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi ........................... 133
18.3. Sarufi: Viambishi vya masharti -nge- na -ngali- .................... 134
18.4. Matumizi ya lugha: Mawasiliano ya kiteknolojia .................. 135
18.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ............................... 138
18.6. Kuandika ....................................................................... 138
**SOMO LA 19. MATUMIZI YA SIMU YA MKONONI ..................... 139**
19.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi ya simu ya mkononi ............ 139
19.2. Msamiati kuhusu matumizi ya simu ya mkononi .................. 141
19.3. Sarufi: Kiambishi cha masharti -ngeli- ................................ 142
19.4. Matumizi ya lugha: Matumizi ya simu ya mkononi ............... 143
19.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu matumizi ya simu . 144
19.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari .......................... 144

**MADA YA 10: SANAA KATIKA JAMII ............................................146**
**SOMO LA 20 : DHANA YA SANAA ................................................147**
20.1. Kusoma na ufahamu: Sanaa na manufaa yake ......................147
20.2. Msamiati kuhusu sanaa na manufaa yake ............................150
20.3. Sarufi: Matumizi ya aina za maneno ..................................150
20.4. Matumizi ya lugha: Dhana ya sanaa ...................................153
20.5. Kuzungumza na Kusikiliza: Majadliano ...............................153
20.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari...........................153
**SOMO LA 21. UMUHIMU WA SANAA KATIKA JAMII ............154**
21.1. Kusoma na ufahamu: Umuhimu wa sanaa katika Jamii.......154
21.2. Msamiati kuhusu sanaa katika Jamii ..................................157
21.3. Sarufi: Matumizi ya aina za maneno ya Kiswahili...............158
21.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu dhima za sanaa katika jamii ..........................................................................164
21.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ...............................165
21.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari...........................165
**MADA YA 11: FASIHI KATIKA JAMII.........................................166**
**SOMO LA 22: FASIHI NA UMUHIMU WAKE KATIKA JAMII ..167**
22.1. Kusoma na ufahamu: Maana ya fasihi .................................167
22.2. Msamiati kuhusu dhana ya fasihi .........................................168
22.3. Sarufi kuhusu matumizi ya aina za maneno..........................169
22.4. Matumizi ya lugha: Umuhimu wa fasihi katika jamii ...........171
22.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano ...............................172
22.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari...........................172
**SOMO LA 23: TANZU ZA FASIHI YA KISWAHILI.......................172**
23.1. Kusoma na ufahamu: Tanzu za fasihi ya Kiswahili ...............173
23.2. Msamiati kuhusu tanzu za fasihi .........................................175
23.3. Sarufi kuhusu matumizi ya aina za maneno..........................175
23.4. Matumizi ya lugha: Nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika jamii... 177
23.5. Kusikiliza na kuzungumza....................................................178
23.6. Kuandika ...........................................................................178
**MAREJEO.................................................................................180**

# UTANGULIZI

Kiswahili ni lugha ambayo imepewa kipaumbele zaidi kutokana na umuhimu wake wa kutumiwa kama lugha rasmi miongoni mwa lugha nyingine zinazotumiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, lugha ya Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondari kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha tatu katika ngazi ya chini ya sekondari. Zaidi ya hayo, mbali na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili hufundishwa katika mchepuo wa Fasihi, Kinyarwanda na Kiswahili, lugha hii hufundishwa pia katika michepuo mingine. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kimatumizi nchini Rwanda na hata katika jamii mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni. Nchi kama vile Marekani, Ujerumani na nchi nyingi za Ulaya, hufundisha Kiswahili na kukitumia katika mazingira tofauti.

Kitabu hiki kimeandikwa kwa kuwalenga wanafunzi wa mwaka wa pili katika Vyuo vya Ualimu nchini Rwanda.

Kila mada iliyojadiliwa katika kitabu hiki imegawanywa katika masomo ambapo kila somo limegusia vipengele vifuatavyo:

- Kusoma na ufahamu
- Matumizi ya msamiati wa msingi
- Sarufi
- Matumizi ya lugha
- Kusikiliza na kuzungumza
- Kuandika.

Masomo yaliyopendekezwa katika kitabu hiki yamezingatia matakwa na mahitaji ya nchi ya Rwanda kwa sababu Kiswahili kinahitajika kutumiwa katika mawasiliano mapana katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Aidha, mwanafunzi anatakiwa kujifunza hatua kwa hatua masomo yote yaliyopendekezwa ili aweze kujijengea na kujifungulia milango ya kujiendeleza na kuliendeleza taifa lake kwa ujumla.

Uwezo utakaopatikana kupitia masomo hayo, utamwezesha mwanafunzi kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza katika maisha yake ya kila siku: kutunza mazingira, elimu kuhusu uzalishaji mali au ujasiriamali, usawa wa jinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili, mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari, mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji, elimu kuhusu ujinsia na elimu jumuishi.

Ni vyema mwanafunzi ajitahidi kufanya kazi zilizotolewa kwa kila somo. Vilevile, ni jambo muhimu kusoma kwa makini na kufanya uchunguzi wa mada zilizojadiliwa katika kitabu hiki.

Kazi nyingi zilizopendekezwa zitamwezesha mwanafunzi kukuza uwezo wake katika kiwango cha utafiti, ushirikiano na utawala binafsi na stadi za maisha na kuendeleza ujifunzaji wa kudumu. Vilevile, kazi za mijadala ya kibinafsi na ya makundi zote zitasaidia kumjenga mwanafunzi kwa kumpa uwezo wa kuwasiliana na watu mbalimbali kwa kutumia Kiswahili fasaha.

Kazi za makundi zilizopendekezwa zitamsaidia mwanafunzi kuelewa nafasi yake katika kujenga desturi ya heshima kwa wengine, uvumilivu, upendo na amani, haki, umoja na mshikamano na demokrasia.

Ili kufanikisha ujifunzaji wake, ni vyema mwanafunzi akumbuke kwamba kitabu hiki kinafuata vitabu vingine vya Kiswahili ambavyo viliandaliwa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza nchini Rwanda. Kwa hiyo, mwanafunzi awe na ujuzi wa awali wa kutosha ambao utamwezesha kuelewa mada zilizotolewa katika kitabu hiki na kuhakikisha kwamba amepata uwezo wa kutosha wa kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano na shughuli mbalimbali za maisha.

# MADA 1

# MIDAHALO

## Uwezo mahususi wa mada


Kusikiliza kwa makini maoni ya washiriki wa midahalo na kutoa hoja kwa kutetea au/na kupinga mawazo yaliyotolewa.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutoa maana ya mdahalo
- Kutaja sifa za mdahalo
- Kuorodhesha hatua zifaazo kwa kufanya mdahalo
- Kukumbuka taratibu za kufuata wakati wa kutoa hoja katika mdahalo
- Kuchunguza kiini cha mada ya mdahalo
- Kupanga vizuri hoja za kuzungumzia katika mdahalo
- Kupinga maoni ya wazungumzaji kutoka upande mwingine katika mdahalo
- Kuongoza mdahalo kwa kuzingatia taratibu za mdahalo
- Kuonyesha tabia ya heshima wakati wa kujadiliana
- Kubaini na kuonyesha matumizi ya vivumishi vya majina ya ngeli ya U-ZI

## KIDOKEZO

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali hapo chini**



1. Wahusika wanaoonekana kwenye mchoro wanafanya nini?
2. Wahusika hawa wako wapi?

# SOMO LA 1: MAANA YA MDAHALO

## 1.1. Kusoma na ufahamu: Hali ya maisha ya wasichana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya karne zilizopita

**Soma mdahalo ufuatao, kisha jibu maswali yaliyotolewa hapo chini.**

**KIELELEZO CHA MDAHALO**

**Mwenyekiti (anasimama):** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa hivi leo, hamjambo? Asanteni kwa kuhudhuria mdahalo wetu leo hii. Mada ya mdahalo wetu wa leo, kama mnavyoiona ubaoni, ni « HALI YA MAISHA YA WASICHANA WA LEO NI BORA ZAIDI KULIKO ILE YA KARNE ZILIZOPITA." Mimi jina langu ni Kamana, mwenyekiti wa mdahalo huu. Nitashirikiana na Amina kama katibu pamoja na Usanase kwa kudhibiti muda. Vilevile tuna pande mbili, watetezi wa mada (akawaonyesha) na wapinzani wa mada (akawaonyesha). Bila kuchelewa, ningependa kumkaribisha bwana (ataje jina lake) ambaye ni msemaji mkuu wa kwanza kwenye upande wa utetezi ili atoe hoja zake kwa kukubaliana na mada.

**Msemaji wa 1 (Utetezi):** Asante sana bwana mwenyekiti na washiriki wote. Jina langu ni (akataja jina). Ni mimi msemaji wa kwanza kwenye upande

wa utetezi. Hapa nitashirikiana na (akataja majina ya wenzake). Sisi tunakubaliana na mada ya leo kwa sababu ni wazi kabisa kwamba hali ya maisha ya wasichana wa leo ni bora zaidi kuliko ile ya karne zilizopita katika nyanja tofauti. Kwa mfano, katika uwanja wa elimu, wasichana wa leo wana haki ya kwenda shuleni tangu shule za chekechea hadi vyuo vikuu na kupata elimu ya kiwango cha hali ya juu. Wanapohitimu masomo hayo, hupewa shahada na kuajiriwa kwa kufanya kazi mbalimbali kama kaka zao. Jambo hili ni muhimu sana ukilinganisha na jinsi wasichana wa zamani walivyokuwa wakiishi.

Mheshimiwa mwenyekiti, waheshimiwa nyinyi washiriki; haya ni baadhi ya mambo mengi yanayoweza kututhibitishia kwamba wasichana wa leo huishi vizuri kuliko wale wa zamani. Kwa sasa ninamalizia hapa. Nina imani kwamba wasikilizaji washiriki hamtasita kuniunga mkono kwa haya yote na mengine yatakayozungumziwa na wenzangu watetezi wa mada yetu. Maendeleo ya nchi ni kutomwacha msichana nyuma. Asanteni sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Naam! Baada ya kusikiliza hoja za msemaji mkuu wa kwanza kwenye upande wa utetezi, sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa kwanza kwenye upande wa upinzani (Ataje jina). Je, unakubaliana na yale ambayo mwenzako amekwisha kusema au la?

**Msemaji wa 1 (Upinzani):** Asanteni sana bwana mwenyekiti na wasikilizaji washiriki. Jina langu ni ....Mimi ni msemaji mkuu wa kwanza kwenye upande wa upinzani. Niko pamoja na (ataje majina). Mimi sikubaliani kabisa na hoja ya utetezi wa mada hii. Msemaji ambaye ametangulia amesema kwamba wasichana wa leo wanaanza kusoma wangali wadogo kufika kwa viwango vikubwa na kupewa shahada za hali ya juu wakapewa kazi na kunufaika. Bali, ni lazima tukumbuke kwamba wasichana wa karne zilizopita nao walikuwa na namna yao ya kujifunza na kujua mengi ya maisha ya nyakati zao. Chunguza kwa mfano shughuli zilizokuwa zikifanyika unyagoni (Urubohero kwa Kinyarwanda). Nyakati hizo zilizopita wasichana walikuwa wakichungwa na wazazi wao na kushauriwa mara kwa mara. Lakini leo wasichana wamebadilisha mienendo kutokana na hali ya maisha ya karne za leo. Siku hizi tunashuhudia wasichana wengi wanaopachikwa mimba wakiwa shuleni na wengine huwa wamezamia katika uasherati. Haya yote yanatokana na kwamba leo wana uhuru wa kufanya yote wayapendayo bila kujali maelekezo ya wazazi wao.

Ninapendekeza kwamba wasichana wabaki nyumbani ili mama zao wawachunge vilivyo na kuwaandalia maisha bora kama yale waliyokuwa nayo wasichana wa karne zilizopita. Asante sana kwa kunisikiliza.

**Mwenyekiti:** Ah ! Mambo yamepamba moto kweli ! Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, tumeishasikiliza hoja za wasemaji wakuu wa kwanza kutoka pande zote mbili. Sasa ningependa kuwakaribisha wasemaji wakuu wa pili ili nao watoe hoja zao. Zamu ni ya msemaji mkuu wa pili upande wa utetezi.

**Msemaji wa 2 (Utetezi):** Bwana mwenyekiti, bwana katibu na waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Sitarudia jina langu kwa sababu msemaji mkuu wa kwanza kwa upande wangu amenitambulisha. Asanteni sana kwa kunipa fursa hii ili nitoe hoja zangu. Maoni ya msemaji mpinzani siyakubali kabisa! Je, kumfungia nyumbani msichana ndiyo njia bora ya kumtafutia maisha? Leo sisi wasichana tuna uhuru wa kufanya tupendayo. Kupachikwa mimba zisizotarajiwa, ninakubali kuwa ni shida. Lakini ni kwa kiwango gani? Kwa sababu gani tunasikia kuwa zamani kulikuwepo wasichana waliokuwa wakitumbukizwa majini ilhali walikuwa wakichungwa na wazazi wao? Niwakumbushe kuwa jambo hili liliwezekana baada ya msichana kutambulika kuwa amepata mimba isiyotarajiwa !

Mheshimiwa mwenyekiti, wasikilizaji washiriki wapendwa, siwezi kumaliza fursa yangu bila kugusia jambo muhimu sana la matumizi ya teknolojia ya kisasa na mitandao ya kijamii. Wasichana wa leo kama kaka zao wamenufaika zaidi kwa kutumia teknolojia hii. Hivi leo, ni jambo rahisi kuwasiliana. Kupitia njia za mitandao ya intaneti, simu za mikononi, wasichana wa leo wanaweza kushirikiana na wengine. Haya huwasaidia wasichana kujichagulia wachumba na kuweza kuongea nao. Lakini zamani za kale, msichana alikuwa akitafutiwa mume tofauti na hiari yake. Siku hizi msichana anaweza kuchagua mwelekeo wa maisha yake. Anaweza kuolewa au la. Lakini zamani, maisha yake yalikuwa mikononi mwa wazazi wake hasa babake. Mheshimiwa mwenyekiti, kutokana na haya yote na mengine ambayo yamezungumziwa na mwenzangu yanadhihirisha kwamba wasichana wa leo huishi maisha mazuri kuliko wasichana wa karne zilizopita. Maendeleo ya nchi ni kutomwacha msichana nyuma. Asante sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Naam, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, mawazo yote mmeyasikia. Sasa ninamkaribisha msemaji mkuu wa pili kutoka upande wa upinzani.

**Msemaji wa 2 (Upinzani):** Bwana mwenyekiti, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, asanteni sana kwa kunipa furasa hii ili nami nitoe maoni yangu. Jina langu ni….. msemaji wa pili kwenye upande wa upinzani. Mimi sikubaliani hata kamwe na hoja za msemaji wa pili wa upande wa utetezi. Kumbukeni kwamba zamani msichana alikuwa akilindwa vizuri na jamii na kufundishwa mambo ya kike. Lakini leo wasichana wamepewa uhuru

uliowafanya kuvuka mipaka. Teknolojia imewatwaa. Mimi ninasikitika sana. Ukiangalia wasichana wa leo, mambo haya yote hawayajui. Badala yake, wao hupoteza muda mrefu kwa kutumia njia zile za teknolojia ambazo zimezungumziwa na msemaji ambaye amenitangulia. Teknolojia hii ndiyo chanzo cha mienendo mibaya na tabia mbaya miongoni mwa wasichana wa leo na mara nyingi wasichana hawa huitumia kwa kuangamiza maisha yao badala ya kuyaboresha au kuwaendeleza.

Angalia mavazi wanayovaa! Jamani, ni ya kusikitisha mno! Mengi ni ya kupotosha kabisa na ya kudhalilisha wanayoyavaa. Siku hizi huweza kumkuta msichana akitembea kitovu nje, mgongo wazi kutokana na mavazi anayoyavaa. Mavazi mengine kama sketi fupi zinazowabana nyonga na makalio huonyesha ukosefu wa nidhamu na heshima anayostahili msichana Mnyarwanda. Teknolojia! Ndiyo! Sipingi maendeleo. Lakini inawaletea wasichana madhara makubwa. Siku hizi tunashuhudia ndoa zinazovunjika baada ya muda mfupi. Haya ni kulingana na nini? Ni kulingana na uhuru huo wa wasichana kujichagulia wachumba kwa njia ya teknolojia ya leo. Wengine huambukizwa magonjwa ya zinaa. Hii inatokana na kujitoma katika tabia mbaya zitokanazo na teknolojia mpya. Kwa hivyo, ni wazi kwamba maisha ya wasichana wa leo si mazuri ukilinganisha na maisha ya wasichana wa zamani kwani ving'aavyo, vyote si dhahabu. Asanteni sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Mengi mmeyasikia kutoka kwa wasemaji wakuu kutoka pande zote mbili, nina matumaini kuwa mmeyazingatia yote. Sasa ningependa kuchukua fursa hii ili kuwakaribisha wasikilizaji washiriki ili nao watoe hoja zao kwa mada hii. (Mwenyekiti achague msikilizaji mshiriki aliyenyosha mkono).

**Msikilizaji mshiriki 1:** Asante sana bwana mwenyekiti, hoja zote zilizotolewa kutoka upande wa utetezi na upande wa upinzani ni nzuri; lakini kwa upande wangu ninawaunga mkono watetezi wanaposema kuwa maisha ya wasichana wa leo ni bora zaidi kutokana na maendeleo na teknolojia ya kisasa. Hata hivyo, ningependa kutoa wito kwao ili watambue kwamba teknolojia hii huhitaji uangalifu mno.

Ni lazima waitumie kwa shughuli za kujiendeleza kielimu, kisayansi na kijamii badala ya kujiharibu kwa kujiingiza katika vitendo vibaya na mienendo mibaya. Wengi wa wasichana hawa wanahitaji kubadilisha tabia zao ili wajenge maisha yao na kuwa watu wazima wenye nafasi na majukumu katika jamii nzima. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Bibi (ataje jina lake) Ninaona unanyosha mkono. Karibu!

**Msikilizaji mshiriki 2:** Asante bwana mwenyekiti. Mimi ninaunga mkono upande wa upinzani kwa sababu wasichana wa karne zilizopita walikuwa na nidhamu na heshima kuliko wasichana wa leo. Tabia na mienendo mizuri ndiyo ilituwezesha kuwa na ndoa zilizoimarika kiasi cha kuaminiana, tofauti na hali ilivyo leo ambapo familia nyingi zinafarakana kwa sababu ya kusalitiana. Siku hizi uchumba hufanyiwa kwenye simu na mitandao ya kijamii na jambo hili husababisha kutofuata mila na desturi za jamii ambazo zilimshirikisha mshenga katika masuala ya ndoa. Matokeo yake ni kujenga familia zisizodumu muda mrefu. Familia kama hizo ndizo huishia mahakamani na kupeana talaka baada ya muda mfupi wa kufunga ndoa. Hivyo basi, maisha ya wasichana wa leo siyo mazuri kuliko yale ya wasichana wa zamani. Asanteni sana.

**Mwenyekiti:** Waheshimiwa, baada ya haya yote, muda umeyoyoma. Ningependa kumkaribisha katibu wa mdahalo ili atusomee muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande zote mbili na hatimaye tupige kura na kuona mshindi wa leo. Zamu ni yako katibu.

**Katibu:** (Anasoma hoja zote ambazo zimetolewa na kila upande)

**Mwenyekiti:** Naam, baada ya kusikiliza hoja zote, ni wakati wa kupiga kura ili tujue mshindi wa leo. Sasa wanaotetea mada wanyoshe mikono (katibu anahesabu na kuandika idadi yao). Wanaopinga mada nao mikono juu (Katibu anahesabu na kuandika idadi yao). Katibu, tusomee matokeo ya kura.

**Katibu:** Upande wa utetezi umepata kura ishirini na moja (aandike 21 ubaoni). Upande wa upinzani umepata kura kumi na tano (anaandika 15 ubaoni).

**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana, baada ya kupiga kura na kuona matokeo ya kura, ushindi katika mdahalo wetu umekwenda kwa upande wa utetezi (wasikilizaji washiriki wanawapigia makofi). Asante sana kwa kuhudhuria mdahalo wetu leo hii. Tukutane wakati ujao.

## KAZI YA 1

### Maswali ya ufahamu

1. Andika kichwa au mada ya mdahalo wa hapo juu.
2. Ni pande gani zinazoonekana katika mdahalo huu?
3. Eleza hoja za mtetezi wa kwanza katika mdahalo huu.
4. Ni aina gani za teknolojia zinazozungumziwa katika mdahalo?
5. Eleza madhara yanayotokana na matumizi mabaya ya teknolojia ya kisasa.

## 1.2. Msamiati kuhusu mdahalo

### KAZI YA 2

**Unganisha maneno ya safu A na maana zake katika safu B.**

| Safu **A** | Safu **B** |
|---|---|
| 1. Mwenyekiti | a. Kovu lililoko katikati ya tumbo baada ya uzi wa mshipa kukatwa na kukauka. |
| 2.Unyago | b. Shule za watoto wadogo wasiozidi miaka mitano |
| 3. Mwenendo | c. Kufaidika. |
| 4.Shule za chekechea | d. Matendo ya mtu yanayojirudiarudia au tabia. |
| 5. Shahada | e. Karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo ili kuthibitisha kwamba amemaliza au amefaulu mitihani yake. |
| 6. Kitovu | f. Adabu. |
| 7. Nidhamu | g. Mtu anayetumwa na upande wa mchumba wa kiume kupeleka posa kwa mwanamke. |
| 8. Mshenga | h. Ngome ya kuwafundisha wari mila za kabila lao. |
| 9. Mchumba | i. Mtu aliyechaguliwa na watu kuongoza kama vile mkutano au mdahalo. |
| 10. Kunufaika | j. Mwanamume aliyepeleka posa au mwanamke aliyepelekewa posa na ikakubaliwa na wazazi. |

### KAZI YA 3

**Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno hapo chini:**

1. Chuo kikuu
2. Mimba
3. Magonjwa ya zinaa
4. Katibu
5. Majukumu

## 1.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya U-ZI

### KAZI YA 4

**Chunguza maneno yafuatayo na kueleza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ukuta | Kuta |
| Ukucha | Kucha |
| Unywele | Nywele |
| Waya | nyaya |
| Wembe | Nyembe |
| Uta | Nyuta |
| Ufa | Nyufa |

### Maelezo muhimu

- Ngeli ya U-ZI hurejelea majina ambayo huanza kwa U- (umoja)

Katika wingi majina haya huchukua umbo tofauti.

- Majina yenye silabi tatu au zaidi hubadilika kwa kutoa U- (Ukuta- kuta, ukucha-kucha)
- Majina yenye silabi mbili hubadilika kwa kuleta ny- katika wingi (uta-nyuta, ufa-nyufa)
- Majina yanayoanza kwa **w-** hubadilika kwa kuleta **ny**- (waya-nyaya, wembe- nyembe)
- Kuna majina yanayochukua **nd**- katika wingi (ulimi-ndimi)
- Kuna majina yanayochukua **mb**- katika wingi (ubao- mbao, ubavu-mbavu)
- Katika kitenzi majina ya ngeli ya U-ZI hufuatwa na kitenzi chenye kiambishi U- katika umoja na ZI- katika wingi.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| **Mfano:** Ufagio **u**menunuliwa. | Fagio **zi**menunuliwa. |
| **W**imbo **u**nafurahisha. | **Ny**imbo **zi**nafurahisha. |

## KAZI YA 5

**Andika sentensi zifuatazo katika wingi:**

1. Ukuta wa nyumba yangu umepakwa rangi.
2. Ulimi unaniumiza.
3. Ufagio umepotea.
4. Waya wa umeme umenunuliwa na kutumiwa vilivyo.
5. Ubavu wake umevunjika alipokuwa akicheza mpira.
6. Uzi uliotumiwa kwa kushona koti lake umepotea.
7. Ufa umezibwa.
8. Uso umesafishwa.
9. Ukurasa umechafuliwa na mwandishi.
10. Ubao wa kujengea nyumba umepasuliwa.

**Vivumishi vya sifa vya ngeli ya U-ZI**

## KAZI YA 6

**Chunguza vifungu vya maneno yafuatayo na kueleza mabadiliko ya kisarufi yaliyojitokeza**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Ukuta **mrefu** | Kuta **ndefu** |
| Uso **mzuri** | Nyuso **nzuri** |
| Waya **mfupi** | Nyaya **fupi** |
| Wembe **mkali** | Nyembe **kali** |
| Uta **mzito** | Nyuta **nzito** |
| Ukucha **mweupe** | Kucha **nyeupe** |
| Ukuta **dabwadabwa** | Kuta **dabwadabwa** |

- **Vivumishi vya sifa katika ngeli ya U-ZI huonekana kwa njia tofauti.**
  - Kuna vivumishi vinavyochukua **m-** katika umoja na **nd-** katika wingi.

    **Mfano:** Ukuta **m**refu- kuta **nd**efu
  - Kuna vivumishi vinavyochukua **m-** katika umoja na **nz-** katika wingi.

    **Mfano:** Uso **m**zuri- nyuso **nz**uri

- Kuna vivumishi vinavyochukua **mw**- katika umoja na **ny**- katika wingi.
  **Mfano:** Unga **mw**eupe- nyunga **ny**eupe
- Kuna vivumishi ambavyo huchukua **m-** katika umoja na kutoonyesha kiambishi chochote katika wingi.
  **Mfano:** Wembe **m**kali- **ny**embe kali.
- Kuna vivumishi visivyoonyesha viambishi katika umoja na wingi.
  **Mifano:** unga **tikitiki**- nyunga **tikitiki**
  Ukuta **dabwadabwa-** kuta **dabwadabwa**

## KAZI YA 7

**Weka sentensi zifuatazo katika wingi.**

1. Yeye ana ukucha mrefu.
2. Mtoto huyu ana unywele mwekundu.
3. Utatumia wembe mkali.
4. Ruganzu alikuwa akitumia uta mzito kwa kupambana.

## 1.4. Matumizi ya lugha: Maana ya mdahalo

## KAZI YA 8

**Soma maelezo hapo chini kisha ujibu maswali husika**

Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu. Kuna mada inayozungumziwa, wazungumzaji wakuu wanaotetea mada (upande wa utetezi) na wazungumzaji wakuu wengine wanaopinga mada (upande wa upinzani). Aghalabu katika mdahalo kuna wazungumzaji wakuu wawili kwa kila upande.

Mwenyekiti wa mdahalo ana wajibu wa kufungua na kuendesha mdahalo, kuwapa wasemaji nafasi ya kuzungumza, kupigisha kura na kufunga mdahalo.

Katibu wa mdahalo ndiye huandika hoja zinazotolewa na wazungumzaji mbalimbali, kufanya na kusoma muhtasari wa hoja zilizotolewa na pande mbili mwishoni mwa mdahalo na kutangaza matokeo ya kura zilizopigwa. Mdahalo ukifanyiwa darasani, mwalimu atatoa maoni yake juu ya mdahalo.

- ***Kwa kifupi*** *mdahalo ni mazungumzo, huhusisha mitazamo miwili (upinzani na utetezi), huhusu mada maalum; mada yenyewe huhusu jammii.*

**Maswali:**

1. Eleza maana ya mdahalo.
2. Eleza wajibu wa katibu katika mdahalo.
3. Ni pande gani zinazoonekana katika mdahalo?

## 1.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### KAZI YA 9

**Kwa kushirikiana na wenzako, jadilini mada zifuatazo:**

1. “ Umuhimu wa mdahalo kwa wanafunzi”
2. “ Ueneaji wa teknolojia katika maendeleo ya nchi”


## 1.6. Kuandika

### KAZI YA 10

**Tunga mdahalo kuhusu mada ifuatayo, kisha iwasilishe mbele ya darasa kwa kushirikiana na wenzako.**

“ Sifa moja ya mdahalo ni kwamba husaidia kutatua matatizo ya wanajamii ”

## SOMO LA 2: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MDAHALO



### KAZI YA 1

**Tazama kwa makini mchoro hapo juu, baadaye ujibu maswali yafuatayo:**

1. Unaona nini kwenye mchoro huu?
2. Unafikiri mchoro huu unazungumzia nini?
3. Mchoro huu unakukumbusha nini katika maisha yako?

### 2.1. Kusoma na ufahamu: Dawa za Kulevya Ndilo Tatizo Linaloathiri Maendeleo ya Vijana

#### Soma mdahalo ufuatao kisha ujibu maswali ya ufahamu

**Mdahalo : D*awa za Kulevya Ndilo Tatizo Linaloathiri Maendeleo ya Vijana***

**Mwenyekiti (anasimama):** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa leo, kwanza ningependa niwakaribishe katika mdahalo huu. Hapa mbele yenu, mimi ni mwenyekiti. Pembeni mwangu upande wa kushoto mnamuona katibu wa mdahalo wetu. Mdahalo wetu unazihusisha pande mbili: upande wa utetezi na upande wa upinzani. Mada yetu ya mdahalo kama mnavyoiona pale mbele, inahusu: "**Dawa za kulevya ndilo tatizo kuu linaloathiri maendeleo ya vijana".** Kila msemaji atakayepewa fursa ya kuzungumza asizidi dakika tano na ni sharti ya mdhibiti-muda kumkataza kuendelea kutoa hoja anapozidisha fursa yake ya kusema. Bila kupoteza muda, ningependa nimkaribishe msemaji mkuu wa kwanza upande wa utetezi ili atoe hoja zake.

**Msemaji Mkuu wa 1 (Utetezi)**: Mheshimiwa mwenyekiti, wasikilizaji washiriki, ni kweli kabisa kwamba dawa za kulevya ni tatizo kubwa linalojitokeza miongoni mwa vijana wa leo kiasi kwamba huathiri sana tabia zao na mwenendo wao mwema. Sisi sote tunajua kwamba Mwenyezi Mungu amemkirimu mwanadamu kwa kumpa akili na fahamu ili aweze kufikiri, kuongoza viumbe wengine na kutunza mazingira yake. Kwa hivyo, akili na fahamu ni johari zenye thamani na ni neema kubwa inayomtofautisha na wanyama. Hakika ni kwamba wanadamu wamefadhilishwa kwa fadhila kubwa kuliko viumbe wengine wote. Akili ni kipawa alichotunukiwa ili aweze kutekeleza vizuri wajibu aliopewa na Mungu kwa madhumuni ya kuboresha maisha yake.

Matumizi ya dawa za kulevya hujitokeza kama janga kubwa kwa jamii zetu. Vijana wengi wakiwemo wanafunzi wamezama katika janga hilo kwa kutumia uraibu huu mbaya unaowaangamiza kwa kuwafanya wapoteze afya au kutumbukia katika mienendo mibaya. Wanaotumia dawa hujikuta katika hali ya uvivu unaokuwa kikwazo muhimu katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kujiendeleza. Badala ya kujielimisha, vijana hao hujiingiza katika mambo mabaya kama vile ugomvi, ujambazi, umalaya, ukatili, n.k. Mtu anapotumia dawa za kulevya huanza kukosa akili timamu inayomwezesha kuwa na mipango mizuri kuhusu maisha yake.

Kwa yote hayo na mengineyo yatakayotolewa na wenzangu, ninaona kwamba wasikilizaji washiriki hamtasita kuniunga mkono kwamba dawa za kulevya ndilo tatizo kubwa miongoni mwa vijana wa leo. Lazima tupambane na dawa hizi ili tuweze kubadilisha maisha ya watoto wetu. Asante sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti**: Naam, waheshimiwa wasikilizaji washiriki, baada ya kusikiliza hoja za msemaji mkuu wa upande wa utetezi, sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu wa upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake.

**Msemaji mkuu wa 1 (Upinzani):** Asante sana mwenyekiti. Mimi sikubaliani kabisa na mtetezi wa mada hii. Msemaji huyo amesema kwamba dawa za kulevya ndiyo madhara makubwa kwa maendeleo ya vijana wa leo, lakini mimi ninaona kwamba kuna mambo mengine mengi yanayokwamisha maendeleo ya vijana na ya jamii kwa ujumla. Kwa maoni yangu, ninafikiria kwamba matumizi mabaya ya teknolojia mpya na mitandao ndilo janga kubwa kwa vijana wetu. Siku hizi vijana wengi hupoteza muda mrefu kwa kuangalia mitandao ambayo huwafanya waige tabia mbovu za watu wasio na adabu na mienendo mizuri. Kijana anamaliza muda wake kwa kuangalia mitandao isiyomnufaisha kwa chochote. Ni dhahiri kwamba hataweza kujiendeleza na hataweza kuwa na mipango mizuri ya kuendeleza jamii yake. Kama yeye ni mwanafunzi atakosa kujifunza kwa bidii ili aweze kuelimika na hata kama yeye ameishabahatika kumaliza masomo yake na

kupata kazi, hataweza kuifanya vizuri kwani muda mrefu ataumaliza kwa kuangalia mitandao hiyo, jambo ambalo litaathiri pato litakalotokana na kazi hiyo.

Aidha, ili kuthibitisha haya, hebu tuchukue mfano wa kijana ambaye kazi yake ni udaktari. Yeye anapofika kazini, jambo la kwanza ni kuchunguza kwenye mitandao mambo kadhaa yaliyotukia hapa na pale, kisha kuzungumza na marafiki zake kwa kutumia mitandao ya kijamii kama fesibuku na mitandao mingine ya kijamii. Kijana huyu hataweza kuleta matunda kwa kazi anayoifanya na jamii huweza kuangamia kutokana na mienendo yake kwani badala ya kuokoa maisha ya watu, yeye amezama katika mambo yasiyo na maana na faida yoyote kwa jamii.

Zaidi ya hayo, matumizi mabaya ya mitandao huendeleza tabia mbaya katika jamii pale ambapo vijana wengi wameanza kuonekana kama wakosefu wa nidhamu, wenye kiburi cha kupindukia baada ya kujitoma katika kutazama baadhi ya vijana wengine kutoka nchi mbalimbali. Ni mara ngapi tunasikia wazazi wakilalamika kwamba watoto wao huwaiga wahusika tofauti ambao wanawatazama katika filamu zisizo na maadili mema? Kumbukeni kwamba mambo haya hutukia wakati ambapo wazazi wameenda kazini na kuacha tarakilishi sebuleni ambapo watumishi wa nyumbani huziwasha na kuwaonyesha watoto hao filamu zenyewe. Wakati mwingine vijana wa leo hupata mienendo mibaya wanapowatembelea ndugu au jamaa zao ambao wana mazoea ya mienendo isiyo mizuri. Kwa kweli, filamu hizi huchochea tabia mbaya mno kama vile uasherati, uzinzi na nyingine miongoni mwa vijana wetu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba vijana wetu hukumbwa na matatizo mengine mengi na mazito zaidi kuliko matumizi ya dawa za kulevya. Ni vyema tuelewe kwamba matatizo haya yote yanapaswa kuchunguzwa na kukomeshwa ili kuwajenga vijana wetu badala ya kufikiri kuwa dawa za kulevya ndilo tatizo kubwa linalohitaji suluhisho kuliko yale mengine. Asante sana Mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, tumekwisha kuyasikiliza maoni ya wasemaji wakuu wa pande zote. Sasa ningependa niwakaribishe wasemaji wa pili wa pande hizi mbili watoe hoja zao. Atakayeanza ni yule wa upande wa utetezi.

**Msemaji wa 2 (Utetezi):** Asante sana Bwana mwenyekiti, Bwana katibu na waheshimiwa wasikilizaji washiriki. Nimeshaelewa hoja za msemaji anayemaliza kutoa hoja zake kwa kupinga mada yetu na kwa hakika aliyoyasema hayatofautiani na msimamo wetu kama watetezi. Mimi ningependa kumkumbusha tu kwamba matatizo mengi aliyoyazungumzia hutokana na matumizi ya dawa za kulevya au pengine nayo huweza kuchukuliwa kama dawa za kulevya. Kitu chochote kinachoweza kufanywa

kwa kipimo kinachozidi kiasi nacho huwa kama dawa za kulevya. Filamu hizo zinazomfanya mtu asahau wajibu wake, matumizi mabaya ya mitandao au simu inayokufanya ubadilishe mwenendo wa kawaida unaotakiwa katika jamii nayo huchukuliwa kama dawa hizo za kulevya.

Dawa za kulevya maana yake msingi ni dawa zinazoweza kumezwa, kujichoma ndani ya sindano, kutafunwa au kunuswa ili anayezitumia abadili hali na mienendo yake. Katika hali nyingine, wanaotumia dawa hizi hulenga kujiepusha na woga kwani wanapokula na wanapokunywa dawa hizo hufikiria kwamba wamejitia nguvu zinazowawezesha kufanya jambo lolote lile. Kwa hivyo, ni wazi kwamba matokeo ya kitendo cha kutumia dawa za kulevya humbadili mtu kwa kila kitu anachofanya kuanzia fikira zake, mipango na utekelezaji wa shughuli zake. Mtu huyu hatafaa tena kwa chochote kwani ameshageuka mtu mwingine ambaye hawezi kuwa na mpango imara wa kile anachofanya kwani dawa hizo ndizo humwelekeza katika matendo yake. Hivyo basi, maana hiyo ya dawa za kulevya hupanuliwa kwa vitu vyote vinavyomfanya mtu abadilishe tabia zake, na mienendo yake na akaonekana kama mtu asiye na akili timamu yenye kumwelekeza kutekeleza mambo kwa ufanisi.

Mbali na ukweli huo, tukichunguza dawa zenyewe katika uhalisi wa mambo, tutaona kwamba vijana wanaotumia dawa za kulevya huathirika sana kiafya pale ambapo dawa hizi huingia mwilini na kuua kinga za mwili wake hadi unapoanza kuwa dhaifu kiasi cha kupatwa na magonjwa ya aina mbalimbali. Chunguza kwa mfano hali ya mtu anayetumia dawa kama kokeni, heroini, bangi na miraa. Mtu huyu huathirika kwanza katika ubongo kama alivyozungumzia mwenzangu aliyenitangulia na kisha mwili wake hudhoofika. Madhara huzidi kuongezeka mpaka wakati anapoanza kukosa nguvu za kufanya kazi yoyote katika kulijenga taifa lake na yeye kugeuka mzigo mkubwa kwa taifa zima na wanajamii wengine.

Watu wengi ambao hutumia dawa za kulevya hawawezi kuaminika na mtu yeyote kiasi cha kupewa kazi ya kujiendeleza. Vilevile anapopewa kazi hiyo, matokeo ni kwamba yeye huzembea kufanya kazi hiyo mpaka anapofutwa kazini. Ama wakati mmoja ameenda kunywa pombe kali kiasi kwamba yeye husahau kwamba anatakiwa kwenda kazini, au yeye kubainisha mienendo mibaya mbele ya mkuu wa kazi yake kiasi cha kufukuzwa. Hali hii inapotokea mtu hukosa kazi na kuanza kushirikiana na makundi ya uhalifu kama vile wezi, makahaba, na watu wengine hatari. Kwa hiyo, ni vyema tuelewe kwamba matumizi ya dawa za kulevya ndilo tatizo kuu ambalo linatakiwa kutafutiwa ufumbuzi kwani ndicho chanzo cha matatizo yote yanayojitokeza miongoni mwa vijana wa leo. Ahsante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti**: Naam! Waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Maoni ya wasemaji wakuu upande wa utetezi yamekwisha kusikilizwa. Sasa ningependa kumkaribisha msemaji mkuu upande wa upinzani ili naye atoe hoja zake.

**Msemaji Mkuu wa 2 (Upinzani):** Asante sana Mheshimiwa Mwenyekiti! Waheshimiwa wasikilizaji washiriki! Msemaji aliyepita amebainisha kwamba matumizi ya dawa za kulevya husababisha matatizo yote yanayowakumba vijana na kwamba likitatuliwa tatizo hilo, matatizo mengine yote yatapata ufumbuzi. Je, ni vijana wangapi ambao wanakosa namna ya kuendeleza miradi yao ya kujiendeleza kwa sababu wao hawana uwezo wa kifedha? Hata kama vijana hawa hawajiingizi katika tabia za kutumia dawa za kulevya wao hukutana na tatizo la umaskini na ambalo halihitaji kukomeshwa kwa kuondosha tatizo la dawa za kulevya ili nalo litatuliwe. Jambo muhimu kwa vijana hawa ni kusaidiwa kupata mitaji inayowawezesha kuanzisha miradi ya maendeleo na kuendeleza taifa kwa ujumla. Ni vyema kwamba serikali yetu imefanya mengi kwa ajili ya kusaidia vijana hao kupata uwezo kuanzisha miradi yao, lakini tatizo lingali na ni muhimu zaidi lishughulikiwe ili kuyaboresha maisha ya vijana wetu.

Tatizo la ukosefu wa uwezo wa kutosha kuanzisha miradi ya maendeleo huambatana na lile la ukosefu wa kazi miongoni mwa vijana wanaohitimu masomo yao katika viwango mbalimbali vya elimu. Ieleweke hapa kwamba watu wengi wanaojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya huwa ni wale ambao hawana kazi. Kwa hivyo, ni lazima watu hawa wasaidiwe kupata kazi ili kupunguza au kumaliza tatizo la wanaotumia dawa za kulevya. Mtu akiwa na kazi hawezi kupata muda wa kwenda kunywa pombe hizo kali au kutamani kitu kingine kinachoweza kuharibu afya yake kwani atakuwa na wajibu wa kutekeleza. Kwa hivyo, wasikilizaji washiriki hamtakosa kuniunga mkono kwamba tatizo la matumizi ya dawa za kulevya ni sehemu ndogo ya matatizo mengine mazito kwani hujitokeza kama mojawapo ya athari au matokeo ya kuendelezwa kwa matatizo mengine makubwa kama vile ukosefu wa kazi na uwezo mdogo wa kuanzisha miradi ya kimaendeleo. Mara tu haya yatakapotatuliwa ndipo tatizo la matumizi ya dawa za kulevya litakapokomeshwa au kupunguzwa. Tufikirie namna ya kusaidia vijana wetu kupata kazi na shughuli nyingine za kuzalisha mali ili waweze kuwa watu muhimu katika jamii nzima. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana Wasikilizaji washiriki, watetezi na wapinzani kwa hoja zote zilizotolewa. Mengi yamekwisha semwa na nina imani kwamba wasikilizaji washiriki mmeisha kuyasikiliza maoni ya pande hizi mbili. Sasa ningependa kuzikaribisha hoja zenu kabla ya kumaliza majadiliano yetu. Hii ni fursa mwafaka ya kukaribisha hoja zenu. (Mwenyekiti humchagua anayenyosha mkono katika hadhira). Karibu msikilizaji mshiriki pale nyuma.

**Msikilizaji Mshiriki wa 1:** Asante sana Bwana Mwenyekiti. Siku hizi, vijana wengi wamejiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya, badala ya kujifunza na kuwasaidia wazazi katika kazi mbalimbali. Vijana hujitumbukiza katika vitendo potovu kama vile unyanyasaji, ukatili, ujambazi na ugomvi kutokana na matumizi ya dawa za kulevya. Vitendo hivi viovu hutokana na ukosefu wa maadili na tabia njema ambazo zingeweza kuwatambulisha vijana waliolelewa vizuri. Pengine, athari za dawa hizi zinapozidi, vijana hugeuka majambazi ya kutisha ambayo hayaogopi kuzibomoa nyumba za watu waliotoa jasho lao kwa kufanya shughuli mbalimbali za kutafuta mali zao. Kwa hivyo, vijana kama hawa, hawawezi kujiendeleza kila wanapozitumia dawa za kulevya. Asante sana mwenyekiti.

**Mwenyekiti:** Asante sana msikilizaji kwa kutoa hoja hizo. Sasa ningependa kukaribisha msikilizaji ambaye ana hoja tofauti ya hizi zilizokwishasemwa. (Mwenyekiti humchagua anayenyosha mkono kati ya hadhira). Karibu sana msikilizaji mshiriki.

**Msikilizaji wa 2:** Asante sana Bwana Mwenyekiti. Mawazo yaliyotolewa kutoka upande wa upinzani, yamenikidhi vya kutosha. Ninachoweza kusema kwa kusisitiza yaliyosemwa na upande huo ni kwamba malezi ndiyo msingi wa maendeleo ya vijana.

Sote tukishughulikia malezi ya vijana hawa, tutafanikisha maisha yao mema. Kama walivyosema wapinzani wa mada hii, suluhisho tunaloweza kupendekeza ni kuwafundisha vijana wote ili tuwajengee uwezo wa kuboresha maisha yao.

**Mwenyekiti:** Asante sana wasemaji na ninyi nyote wasikilizaji washiriki. Baada ya kusikiliza mawazo yote muhimu kutoka pande zote mbili, ningependa kumkaribisha katibu wa mdahalo huu ili atusomee muhtasari wa hoja zilizotolewa. Karibu sana katibu wetu.

**Katibu:** Asante sana Bwana mwenyekiti, wasemaji kutoka pande zote mbili na wasikilizaji washiriki! Huu ni muda mwafaka wa kuwasomea hoja zilizotolewa na pande zote za mdahalo wetu. Upande wa utetezi umetoa hoja zifuatazo:

- Dawa za kulevya huathiri sana tabia za vijana kimaendeleo na kimwenendo,
- Dawa za kulevya zina madhara hata katika maendeleo ya vijana wa jamii ya leo,
- Wanaotumia dawa za kulevya hujikuta katika hali ya uvivu unaokuwa kikwazo kwa maandalizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo,
- Badala ya kujielimisha na kujiendeleza, vijana wanaotumia dawa za kulevya hujiingiza katika mambo mabaya kama vile ugomvi, ujambazi, umalaya, ukatili, wizi au udokozi.

- Mtu anapotumia dawa za kulevya hukosa akili timamu inayomwezesha kuwa na mipango mizuri kuhusu maisha yake,
- Mtu anapotumia dawa za kulevya hukosa nguvu za kufanya kazi yoyote katika kulijenga taifa lake,
- Vijana wanaotumia dawa za kulevya huathirika sana kiafya pale ambapo dawa hizi huingia mwilini na kuua kinga ya mwili wake.

Upande wa upinzani umeelezea kwamba badala ya dawa za kulevya vijana wa leo hukumbwa na matatizo mengine mengi na mazito zaidi kuliko matumizi ya dawa za kulevya. Mawazo yao ni kama haya yafuatayo:

- Matumizi ya teknolojia mpya na mitandao ndilo janga kubwa kwa vijana wetu,
- Umaskini huchochea tabia mbaya mno kama vile uasherati, uzinzi,
- Tabia za uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umaskini, umalaya na uraibu mbaya hutokana na:
- Ukosefu wa mwenendo mwema na uhaba wa wajibu wa wazazi kuwashauri vijana,
- Hali ya kutosikilizana kwa wazazi katika familia,
- Ukosefu wa malezi mema,
- Hali ya kushirikiana na makundi ya vijana waovu, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wakuu, ninyi nyote wasikilizaji washiriki, hizi ndizo hoja muhimu zilizotolewa katika mazungumzo ya leo. Asanteni sana kwa kunitega sikio.

**Mwenyekiti:** Naam! Baada ya kusikia hoja zote tuko tayari kutangaza upande ulioishawishi hadhira kuliko mwingine. Hivyo basi, ni wakati wa kupiga kura ili tuonyeshe upande ulioshinda. Wanaounga mkono upande wa utetezi nyosheni mikono juu. Bwana katibu, nakuomba uchukue idadi yao. Wanaounga mkono upande wa upinzani nanyi nyosheni mikono. Wasiounga mkono upande wowote nanyi nyosheni mikono juu. Katibu! Tusomee matokeo ya kura.

**Katibu:** Waliounga mkono upande wa utetezi ni kumi na watatu. Wanaounga mkono upande wa upinzani ni kumi na sita. Wasio na msimamo wowote ni watano.

**Mwenyekiti:** Mabibi na mabwana kama mlivyoona upande ulioshinda ni ule wa upinzani. (Wasikilizaji washiriki wanawapigia makofi). Na huu ndio mwisho wa mdahalo wetu tukutane siku nyingine kwa mada nyingine. Asanteni. (Hadhira inampigia makofi).

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Ni watu gani wanaotajwa katika mdahalo huu?
2. Ni madhara gani yanayosababishwa na dawa za kulevya?
3. Toa majukumu ya wazazi kuhusu malezi ya watoto wao.
4. Eleza maoni ya watetezi kuhusu dawa za kulevya.
5. Ni ushauri gani unaowapa watoto wale wanaotumia dawa za kulevya?

### 2.2. Msamiati kuhusu "Mdahalo"

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Utetezi
2. Upinzani
3. Wajibu
4. Janga
5. Kuhofu

## KAZI YA 4

**Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yafuatayo:**
kutambulisha, kukukataza, kukumbusha, mitandao, fursa, uliridhika.

1. Adhabu ninayokupatia ni onyo la kwanza la……………………..... kujitoma katika matumizi ya dawa za kulevya.
2. Katika mdahalo ni wajibu wa mwenyekiti …………………….... makundi yanayoshiriki yaani upande wa utetezi na ule wa upinzani.
3. Ni wajibu wa mwenyekiti tena kuwapa ……………… ya kutoa maoni yao kuhusu mada husika.
4. ………………………...hadhira mada itakayozungumziwa katika midahalo ili wahusika wasiende nje ya mada husika ni wajibu wa mwenyekiti.

5. Kila upande ......................na kutia saini ya makubaliano ya amani.
6. Mara nyingi viongozi hupenda kutumia ........................ya kijamii wanapotaka kuwajulisha wenzao tukio muhimu.

## 2.3. Sarufi: Matumizi ya vivumishi vya ngeli ya U-ZI: vivumishi vya kuonyesha, kumiliki, kuunganisha na kurejesha

### KAZI YA 5

**Chunguza maneno yaliyopigiwa msitari, kisha eleza mabadiliko ya kisarufi yanayojitokeza katika umoja na wingi.**

**a. Vivumishi vya kuonyesha**

| | |
|---|---|
| Ukucha **huu** | Kucha **hizi** |
| Ufa **huo** | Nyufa **hizo** |
| Wembe **ule** | Nyembe **zile** |

**b. Vivumishi vya kumiliki**

| | |
|---|---|
| Ukucha **wangu** | Kucha **zangu/ zetu** |
| Wayo **wako** | Nyayo **zako/zenu** |
| Uso **wake** | Nyuso **zao** |

**c. Vivumishi vya kuunganisha**

| | |
|---|---|
| Ukuta **wa** nyumba | Kuta **za** nyumba |

**d. Vivumishi vya kurejesha**

| | |
|---|---|
| Ufa **wenyewe** | Nyufa **zenyewe** |
| Uzi **wowote** | Nyuzi **zozote** |

### Maelezo muhimu

- Vivumishi vya kuonyesha vya ngeli ya U-ZI ni: **huu, huo** na **ule** katika umoja na **hizi, hizo** na **zile** katika wingi.
- Vivumishi vya kumiliki vya ngeli ya U-ZI ni: **wangu, wako** na **wake** katika umoja na **zangu, zako, zake, zetu, zenu na zao** katika wingi.
- Vivumishi vya kuunganisha vya ngeli hii ni **wa** katika umoja na **za** katika wingi.
- Vivumishi vya kurejesha vya ngeli hii ni **mwenyewe, mwenye, wote, wowote** katika umoja na **zenyewe, zenye, zote na zozote** katika wingi.

## KAZI YA 6

**Andika sentensi zifuatazo katika wingi:**

1. Ukuta wenye matofali umeanguka.
2. Ufagio wa Mutesi umepotea.
3. Niletee wembe wangu.
4. Kata ukucha huo.
5. Uma wenyewe ulitumiwa kulia chakula.

## 2.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na utekelezaji wa Mdahalo

## KAZI YA 7

**Soma maelezo yafuatayo kuhusu maandalizi na utekelezaji wa mdahalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**

☞Mdahalo ni majadiliano kati ya watu wengi wenye misimamo tofauti. Yafuatayo ni mambo muhimu ya kuzingatia katika maandalizi na utekelezaji wake:

**Maandalizi ya mdahalo**

a. Kuchagua mada ya kuzungumzia katika mdahalo: uchaguzi huu hufanyika kwa kupiga kura.
b. Kumchagua mwenyekiti wa mdahalo: mwenyekiti huchaguliwa kwa kupiga kura na atakayechaguliwa ni yule mwenye uwezo wa kuongoza na kuendesha mdahalo.
c. Kumchagua katibu wa mdahalo: mhusika huyu pia huchaguliwa. Yeye ana wajibu wa kuandika na kuwasomea hadhira muhtasari na matokeo ya mdahalo.
d. Kumchagua mdhibiti-muda: huyu ana jukumu la kuchunguza kwamba kila mhusika anatumia muda wake wa kutoa hoja zake ipasavyo.
e. Kupanga wahusika kwa upande wa utetezi na upande wa upinzani kama wasemaji wakuu wa pande hizo.
f. Kupanga namna ya kukaa kwa wahusika wa mdahalo upande wa utetezi na upande wa upinzani na wasikilizaji pia. Kitendo hiki huweza kufanywa

kwa kupanga watetezi na wapinzani kwenye pande mbili (upande wa kulia na upande wa kushoto) ambapo watabadilishana mawazo kwa urahisi.

g. Kupanga muda utakaotumiwa na wahusika wa pande hizo mbili.

**Utekelezaji wa mdahalo**

a. Mwenyekiti hufungua mdahalo kwa kuwatambulisha wahusika wa mdahalo akianzia kwake kama kiongozi wa mdahalo kisha katibu na washiriki wa pande mbili zitakazojadiliana; yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani.
b. Kabla ya kuanza kutoa hoja za pande mbili husika mwenyekiti huwakumbusha mada mahususi itakayozungumziwa.
c. Katika mazungumzo, watetezi hutoa maoni yao kwa kutetea mada ilhali wapinzani huyapinga mawazo yanayotolewa na watetezi.
d. Kila mhusika hutakiwa kuheshimu muda wake wa kutetea au kupinga mada husika na muda wa kunyamaza kwa kusikiliza hoja za wengine.
e. Mwenyekiti huwapatia wasikilizaji washiriki muda wa kutoa maoni kuhusu mada inayojadiliwa.
f. Wahusika hupaswa kuheshimu amri ya mwenyekiti na kupata uamuzi maalum.
g. Mwenyekiti humpatia katibu fursa ya kuwasomea muhtasari wa waoni yaliyotolewa kama matokeo ya mdahalo.
h. Mwenyekiti huongoza zoezi la kupiga kura na kumuomba katibu aandike idadi ya kura kwa kila upande ili kuonyesha upande ulioibuka na ushindi na ule ulioshindwa.
i. Mwenyekiti hutangaza matokeo ya kura na kuwapongeza waliohudhuria na kufunga mdahalo.

**Maswali:**

1. Toa kanuni zinazoongoza maandalizi ya mdahalo.
2. Ni njia gani zinazotumiwa katika utekelezaji wa mdahalo.
3. Taja mifano mitatu ya mada zinazoweza kujadiliwa katika mdahalo.
4. Mdahalo ni zoezi zuri kwa anayetaka kukuza uwezo wake wa lugha. Jadili.

## 2.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### KAZI YA 8

**Andaa na kutekeleza mdahalo wenye moja ya mada zinazofuata kisha uwasomee wenzako.**

1. Usawa wa jinsia ni nguzo muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.
2. Ni vizuri kutumia mpango wa uzazi.

## 2.6. Kuandika

### KAZI YA 9

**Chagua mada moja kati ya hizi hapa chini kisha utayarishe mdahalo:**

1. Matumizi ya dawa za kulevya yanarudisha nyuma uchumi wa nchi yetu.
2. Kuzaa watoto wengi ni nguzo ya kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

### Tathmini ya mada ya

**A.**

1. Eleza sifa za mdahalo.
2. Eleza mambo ya kujiepusha katika mdahalo.
3. Taja pande zinazohusika katika mdahalo.

**B. Chagua mada moja kati ya hizi zifuatazo, kisha uandae mdahalo :**

1. Wakoloni walileta mabaya mengi kuliko mazuri.
2. Shule za mabweni ni bora kuliko shule za kutwa.

**C. Andika sentensi zifuatazo katika umoja.**

1. Nyufa za nyumba zinaonekana.
2. Walitumia nyuta zenye uzito kwa kupigana.
3. Walivua samaki kwa kutumia nyavu kuukuu.
4. Nyuso zao zimekunjama.
5. Nyoya hizi ni ndefu sana.

# MADA 2

# MIJADALA

**Uwezo mahususi wa mada**

Kutambua na kufafanua kiini cha mada husika ili kutoa maoni binafsi kwa ushirikiano na wenzake.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutoa maana ya mjadala
- Kutaja sifa za mjadala
- Kuordhesha hatua zifaazo kwa kufanya mjadala
- Kuonyesha matumizi ya vivumishi na majina ya ngeli ya PA-M-KU.

## SOMO LA 3: MAANA YA MJADALA

### KIDOKEZO

**Tazama mchoro huu ufuatao kisha jibu maswali hapo chini**



**Maswali :**

1. Unaona nini kwenye mchoro huu?
2. Unafikiri watu hao wanafanya nini?

## 3.1. Kusoma na ufahamu: Maana ya mjadala

***Soma kifungu kuhusu*** **"Maana ya mjadala"** ***ili ujibu maswali uliyotolewa hapo chini.***

Kuna mazungumzo ambayo hufanywa kuhusu suala fulani linalohitaji kujadiliwa na kutafutiwa ufumbuzi. Mazungumzo ya aina hii ndiyo hujulikana kwa jina la mijadala. Kwa kawaida, mjadala ni mazungumzo juu ya jambo maalum ambayo hufanywa na watu kwa kutoa hoja zao kwa jambo fulani linalotakiwa ufafanuzi au ufumbuzi wa suala lililopo.

Mjadala ni aina ya majadiliano ambayo huhusisha watu wengi wanaotoa hoja kuhusu mada fulani. Miongoni mwa watu wanaohusika katika mjadala kuna kiongozi ambaye jukumu lake ni kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji anayeshiriki katika mazungumzo hayo. Katika mjadala, hakuna msemaji ambaye anaruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba fursa kiongozi wa majadiliano.

Mjadala huwa na mada ambayo humulika hoja zote zinazotolewa wakati wa mazungumzo. Kama kuna wasemaji ambao wanataka kukiuka mada katika hoja zao, kiongozi wa mjadala huwarekebisha kwa kuwakumbusha mada inayotolewa hoja.

Mjadala huwa na malengo ya kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa majadiliano. Mjadala hukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani. Aidha, majadiliano hayo humtaka kila mzungumzaji apange mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapopewa fursa ya kuzungumza. Mjadala humsaidia mtu kutambua kipaji alichonacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira na kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha. Humzoeza pia mtu kusikiliza maoni ya watu wengine, kupinga au kutetea maoni na hoja zao. Jambo muhimu ni kwamba majadiliano haya humpa fursa ya kuelewana na watu anaotofautiana nao kimawazo.

Wazungumzaji wanapofanya mjadala hukuza uwezo wa mazungumzo na ujuzi walio nao kuhusu suala fulani na hupanua kiwango chao cha msamiati na kupunguza pia uoga wa kuongea hadharani. Vilevile, mjadala hutumiwa kama nyenzo bora za kutatua migogoro inayoweza kuzuka miongoni mwa wanajamii. Katika mjadala, watu wenye mawazo yaliyo kinyume na mada, hupata nafasi ya kujadiliana juu ya jambo fulani kwa madhumuni ya kutatua tatizo linalowakumba. Mjadala hutumiwa kwa kutatua tatizo na kuondoa migogoro miongoni mwa watu kwa njia ya amani.

Katika mjadala, kama tulivyokwisha kusema, kunajitokeza wahusika ambao ni kiongozi wa mjadala na hadhira. Kiongozi ndiye ambaye ana jukumu la kuongoza mjadala. Kiongozi anaweza kuwa mtu mmoja au wawili kulingana na mada iliyochaguliwa au malengo ya majadiliano yenyewe. Ukichaguliwa kama kiongozi ni lazima uongoze mjadala ipasavyo na usikose kumpangia kila msemaji muda atakaotumia ili aweze kuchangia mawazo yake.

Kwa upande wa mjadala, kiongozi humruhusu yeyote atakaye kutoa mchango kwani hakuna makundi ya watetezi na wapinzani wa mjadala. Kiongozi huyu huwa na majukumu tofauti kwani ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa.

Katika mjadala, kuna hadhira pia ambayo hushiriki katika mazungumzo kwa kusikiliza na kutoa mchango wao kuhusu suala linalojadiliwa. Kila mtu aliye na hoja hunyosha mkono kuomba fursa ya kuzungumza. Lengo la kwanza la kila msemaji katika mjadala si kupata ushindi, kwani si mashindano bali lengo la kila msemaji ni kutoa mawazo kwa nia ya kutatua tatizo fulani linalofafanuliwa na kujadiliwa kwa pamoja. Hivyo, katika mjadala hakuna kushindania ushindi; kila mtu ambaye ana la kusema huruhusiwa kutoa hoja zake kuhusu mada ile inayohusika bila kukiuka taratibu zilizowekwa.

Watu wanaoshiriki katika mijadala huhakikisha kuwa mjadala ni njia ya kukuza uwezo wa kufikiri na kutafuta masuluhisho kwa masuala yanayoikumba jamii fulani. Katika mazungumzo haya, kiongozi ndiye anayeongoza majadiliano ili wazungumzaji watoe mchango wao kuhusu suala lililopo. Kiongozi humpa fursa mzungumzaji kwa kusema, "Simama utoe mchango wako". Mzungumzaji huweza kutoa hoja zake kulingana na anavyolifikiria suala husika. Mara nyingi, mjadala huweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa. Kiongozi hubainisha mada ya mjadala na kuhakikisha kuwa wakati wote wa mjadala kuna mwenendo mwema unaowaongoza washiriki wa mjadala husika.

Mzungumzaji katika mjadala ni lazima awe na uwezo wa kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri. Yeye anakuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kuwa anaweza kuutumia msamiati na kujizoeza matamshi mazuri ya lugha. Jambo muhimu katika mijadala inayofanywa ni kwamba mazungumzo yanayofanywa huwazoeza wengi kusikiliza na kupima maoni na hoja za wenzao, kuelewana na watu wengine kutoka sehemu mbalimbali, kuheshimiana kulingana na mawazo tofauti yanayotolewa na kila mzungumzaji.

Kulingana na hayo yote, ni vyema kukumbuka kuwa mjadala ni mazungumzo yanayoendeshwa na kushirikisha watu tofauti kwa kukidhi haja na malengo yao ya kulifafanua na kulijadili suala lililopo na kulitafutia jibu. Ni lazima kuelewa pia kuwa mjadala ni nyenzo timamu za kuimarisha stadi ya maongezi kuhusu mada fulani.

Zoezi la mjadala ni zuri kwa yeyote anayetaka kukuza uwezo wa mawasiliano, majadiliano, mahojiano na uwezo wake wa kutoa maoni yake na kujitambua katika jamii yake.

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Eleza kwa ufupi maana ya mjadala.
2. Katika mjadala, kiongozi ana kazi gani?
3. Toa hoja tatu kuhusu umuhimu wa mjadala.
4. Ni ipi kazi ya hadhira katika mjadala?
5. Lengo la kila msemaji katika mjadala ni lipi?
6. Mjadala husaidiaje kujua lugha?
7. Ni maadili yapi yanayojengeka kupitia mijadala?

## 3.2. Msamiati kuhusu maana ya mjadala

## KAZI YA 2

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Suala
2. Hoja
3. Jukumu
4. Mchango
5. Majadiliano
6. Hadhira

## KAZI YA 3

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo:** kuwashirikisha, mjadala, kupanga, mazungumzo, hoja, kiongozi, fursa, kipaji, mahojiano, hadhira.

1. Mjadala humsaidia mtu kutambua …………alicho nacho cha kuzungumza bila woga mbele ya wengine.
2. Aliyechaguliwa kuongoza majadiliano kwa kupanga muda wa kuzungumza kwa kila msemaji huitwa ………………..
3. …………………ni jumla ya wasikilizaji au wasomaji wa kazi maalumu.

4. Katika mazungumzo lazima ...................mawazo kwa mfuatano vizuri.
5. Uulizaji maswali ili kufahamu maarifa aliyonayo mtu hujulikana kama.........................
6. .................... unahitajika kwa wanaohitaji ufafanuzi zaidi wa suala lililopo.
7. Mjadala huchukuliwa kama ............................juu ya jambo maalumu.
8. Watu wengi wanapojadiliana kuhusu mada fulani hutoa ............. ambazo husaidia wengine kuelewa ukweli fulani.
9. Mtu yeyote aliyehudhuria mkutano alipewa .................... ya kutoa hoja zake.
10. Mwalimu anaweza ........................wanafunzi katika uchaguzi wa mada.

## 3.3. Sarufi kuhusu ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vya kuuliza

### KAZI YA 4

**Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia viulizi vya ndani ya mabano:**

1. Pahali ......... hapafai? ( -pi na kiambishi -pa)
2. Mahali .......... pana maji ya kutosha? (-ngapi na kiambishi -pa)
3. Mahali ......... hamfai? (-pi na kiambishi m-)
4. Mahali ........... kuna wezi? ( -pi na kiambishi ku-)

### Maelezo muhimu

Vivumishi viulizi (vivumishi vya kuuliza) katika ngeli ya Pa-M-Ku vinaweza kutumika kama hivi:

| Kiambishi ngeli | Nomino | Kiulizi -pi | Kiulizi -ngapi | Mfano katika sentensi |
|---|---|---|---|---|
| Pa | Pahali | Papi | pangapi | Pahali papi hapafai? |
| | Pahali | - | pangapi | Pahali pangapi hapafai? |
| Ku | Mahali | Kupi | kungapi | Mahali kupi kuna mitaro? |
| M | Mahali | Mpi | mungapi | Mahali mpi mnasomea? |

## 3.4.Matumizi ya lugha: Maana ya mjadala

### KAZI YA 5

**Soma maelezo yanayofuata ili kujibu maswali hapo chini.**

☞"Maana ya mjadala"

- Mjadala ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Unaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.
- Mjadala unaongozwa na mtu mmoja au watu wawili ambao wanazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.
- Kiongozi wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa. Mada zinazojadiliwa katika mjadala ni zile ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi.
- Anayetoa hoja yake, anaweza kuunga mkono maoni ya mwenzake au kuyapinga kwa minajili ya kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.
- Katika mjadala mada hutolewa mawazo na ndiyo inamulikia mjadala. Kiongozi wa mjadala hulazimika kuwasaidia wasemaji kutokiuka mada.
- Mjadala huwa na malengo yafuatayo:
  - Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala.
  - Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
  - Kumwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari.
  - Kumwezesha mtu kutambua kipaji alichonacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira.
  - Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
  - Kumzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.
  - Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

- Wahusika katika mjadala ni kiongozi na hadhira.
- Katika mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa kutoa hoja yake na kiongozi.
- Katika mjadala hakuna washindi, kiongozi anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.
- Mjadala unapomalizika, kiongozi huwapongeza waliohudhuria mjadala na kuwaalika katika mjadala mwingine.

**Maswali:**

1. Mjadala unaweza kuongozwa na watu watano. Ni kweli au si kweli? Eleza.
2. Ni ipi kazi ya kiongozi katika mjadala?
3. Jadili malengo matatu ya mjadala mzuri.
4. Kwa sababu gani katika mjadala hakuna mshindi?
5. Eleza wajibu wa wale wanaohusika katika mjadala.

## 3.5. Kusikiliza na Kuzungumza

### KAZI YA 6

**Jadili mada ifuatayo:** "Maendeleo nchini huyafanya maisha ya Wanyarwanda yabadilike kwa kiwango cha juu."

## 3.6. Kuandika

### KAZI YA 7

**Bila kuzidi kurasa mbili, andika mjadala kuhusu mada ifuatayo:** "Ubaya wa dawa za kulevya katika maisha ya binadamu"

## SOMO LA 4: MAANDALIZI NA UTEKELEZAJI WA MJADALA

### KAZI YA 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Mjadala ni nini?
2. Taja watu wanaoshiriki katika mjadala.
3. Unafikiri kuwa majukumu ya watu hao ni yapi?

### 4.1. Kusoma na ufahamu: Mchango wa wazazi katika malezi ya watoto wao

**Soma kifungu hiki kuhusu mjadala kisha ujibu maswali ya ufahamu**

**Kiongozi:** Waheshimiwa mabibi na mabwana mliokusanyika hapa, kwanza ninataka niwakaribishe katika mjadala huu. Kama mnavyotuona hapa mbele yenu, mimi ninayewakaribisha ni kiongozi wa mjadala huu. Pembeni mwangu mnayemwona ni kiongozi msaidizi. Mada ya mjadala wetu wa leo ni kama mnavyoisoma mbele yenu "**MCHANGO WA WAZAZI KATIKA MALEZI YA WATOTO WAO**". Karibuni sana nyote na bila kupoteza muda, ningetaka kumkaribisha mshiriki aliye tayari atoe mchango wake.

**Mshiriki wa kwanza**: Ninawashukuru sana viongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu. Ni kweli kabisa wazazi ndio wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto wao. Kama inavyojulikana malezi ya kwanza kwa mtoto huanzia nyumbani. Nyumbani ndipo mtoto anapopata malezi ya msingi ambayo humulikia maisha yake. Malezi haya ya kwanza yapatikanayo nyumbani humsaidia mtoto kufanikiwa katika maisha yake. Malezi haya yanatolewa na wazazi ambao ndio walezi muhimu wa watoto wao. Bila mchango wa wazazi, watoto hawawezi kupata elimu. Kwa hiyo, wazazi wana jukumu la kwanza katika malezi ya watoto wao. Ahsanteni kwa kunitega sikio.

**Kiongozi**: Asante sana kwa hoja yako. Kama mlivyosikia, msemaji huyu ameeleza kwamba wazazi ndio wanaowapatia watoto wao malezi ya msingi ambayo yanawasaidia kufanikiwa maishani mwao. Tafadhali, naomba mjaribu kutoa maoni mengine kuhusu suala hilo. Karibu bibi!

**Mshiriki wa pili**: Asante sana kiongozi kwa fursa hii ya kuniruhusu kutoa mchango wangu. Kwa maoni yangu, ni kweli wazazi wana nafasi kubwa katika malezi ya watoto wao. Lakini, kuna matatizo makuu ambayo wazazi hawatilii mkazo katika malezi hayo. Chunguza jinsi watoto na vijana wengine wanavyotumia dawa za kulevya. Siku hizi, idadi ya wanaokumbwa na matumizi ya dawa za kulevya huzidi kuongezeka. Wazazi wenzangu, mjue kwamba dawa za kulevya ni hatari sana kwa

binadamu. Dawa hizi husababisha magonjwa mengi na huharibu ubongo wa watoto. Kwa upande wangu, kila mzazi lazima ashiriki katika malezi ya watoto wote anaokutana nao badala ya kufikiria watoto wake tu. Wazazi wote wakilitilia maanani tatizo hili lingemalizika haraka sana na watoto wetu watakuwa na maisha mazuri.

**Kiongozi**: Ninamshukuru sana mshiriki kwa maoni yake. Anaeleza kwamba wazazi hawazingatii wajibu wao kwa kutoa mchango ili kukomesha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana. Anaeleza pia kwamba malezi ya mtoto ni jukumu la kila mtu. Tunamshukuru sana. Hebu, tumsikilize pia mshiriki yule aliyenyosha mkono pale ili naye atoe hoja zake.

**Mshiriki wa tatu**: Mheshimiwa kiongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu. Watu ambao wako karibu sana na watoto ni wazazi wao. Hawa wanapaswa kutunza watoto wao inavyofaa tangu wanapozaliwa na kuwapatia malezi wanayohitaji maishani mwao. Wakati wa kwenda shule unapofika, wao ndio wanaopiga hatua ya kwanza kuwapeleka shuleni. Ni lazima kila mzazi atimize wajibu huu kwa muda unaofaa kwani imedhihirika kuwa kuna wazazi wanaochelewa kupeleka watoto wao shuleni. Shuleni ndipo mtoto anajizoeza kushirikiana na wenzake na kupata mwenendo mwema utakaomsaidia maishani mwake. Watoto wanapofika shuleni, ni vyema pia wazazi wao wawajibike kufuatilia malezi yao kwa kuwashauri, kuwafundisha kuwa na mienendo mizuri, kuwanunulia vifaa vya shule na kuwalipia karo. Waheshimiwa wasikilizaji, kama mnavyoelewa, bila mchango wa wazazi, watoto hawawezi kupata elimu inayotolewa shuleni kwani wao ndio wanarahisisha kila jambo linalotendewa mtoto, awe shuleni, nyumbani na mahali pengine. Asante sana kwa kunitega sikio. Hayo ndiyo maoni yangu.

**Kiongozi**: Waheshimiwa wasikilizaji washiriki, mawazo hayo ya mwenzetu mmeyasikia. Sasa ninataka kumkaribisha msemaji mwingine yeyote ambaye ana la kusema ili naye atoe mchango wake kwa ufumbuzi wa suala letu. Karibu sana bibi!

**Mshiriki wa nne**: Asante sana kiongozi na wasikilizaji washiriki kwa kunipa fursa hii. Wapendwa wasikilizaji washiriki, taifa letu hufanya mengi ili liweze kukomesha matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa wananchi. Kwa nini wazazi tusiwasaidie viongozi wetu kupambana na tatizo hili ili tupige marufuku dawa za kulevya ambazo huangamiza maisha ya watoto wetu?

Serikali yetu imechukua uamuzi mzuri wa kuanzisha mradi wa elimu kwa wote ambapo kila mtoto anapelekwa shuleni akaendelea na masomo yake mpaka anapomaliza shule za sekondari.

Kwa hivyo, ni lazima walimu na viongozi wa shule waelewe kwamba wanahitaji kushirikiana na wazazi ili waweze kutimiza wajibu wao mkubwa wa kubadilisha mienendo ya vijana wanaowalea hasa vijana wale wanaopatikana wakitumia dawa za kulevya. Bila mchango wa wazazi kwa malezi ya vijana hao, shule zetu haziwezi kufanikiwa kuwapatia watoto hao maadili yanayotakiwa. Kwa mfano, utamkuta kijana mmoja akikosekana shuleni kwa siku moja au mbili na akifika huwadanganya viongozi kwamba alikuwa ameenda nyumbani na viongozi hawa hukubali bila kuuliza wazazi wa mtoto huyo kuhusu ukweli wa yale aliyosingizia mtoto huyo. Kwa kumaliza, ni vyema kila mtu anayehusika na malezi ya watoto awe mwalimu, kiongozi wa shule na hata majirani waelewe kwamba wazazi wana nafasi kubwa katika urekebishaji wa mienendo mibaya ya watoto wetu. Asante sana kwa kunitega sikio.

**Kiongozi**: Ninamshukuru mshiriki mwenzetu kwa maelezo yake ambayo yamewagusa wengi. Yeye amesema kwamba ni lazima kuisaidia serikali katika kulinda watoto wetu dawa za kulevya. Ametoa wito pia kwamba kila mtu anayehusika na malezi ya watoto aitambue kwanza nafasi ya wazazi kwa kuwashirikisha kwa kila uamuzi kuhusu mienendo na tabia za watoto wao. Kwa hivyo, tunamshukuru sana kwa mawazo yake mazuri. Kama mnavyoona, mengi yamekwishaelezwa na muda unazidi kuyoyoma. Hebu nichukue fursa hii kuwakaribisha washiriki wengine wawili kabla ya kutamatisha mjadala wetu. Karibu sana.

**Mshiriki wa tano**: Asante sana kiongozi kwa kunipa muda huu ili nami nitoe maoni yangu. Washiriki wenzangu, mawazo yaliyotolewa na waliotangulia ni mazuri sana na yanaeleweka waziwazi. Ni ukweli mtupu kwamba wazazi ndio wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto wao na ndiyo maana wahenga walisema, “Mtoto hutazama kisogo cha mama yake”. Mzazi ni mfano unaoigwa na mtoto wake. Kama mzazi ana tabia nzuri mtoto bila shaka atafuata nyayo zake; lakini mambo yatakuwa kinyume kama mzazi ana tabia zisizopendeza kwani wakati huo mtoto naye ataathirika sana. Kwa hivyo, mimi ningependa kuhimiza wazazi wote kukuza na kuendeleza tabia nzuri mbele ya watoto wao ili waweze kuigwa na kutumiwa kama mifano mizuri kwa malezi ya watoto wao. Kumbukeni kwamba mtu hutoa kile alichonacho na pia huvuna kile alichopanda. Asanteni.

**Kiongozi:** Asante sana mshiriki kwa mawazo yako mazuri. Naona kuna wengine wanaonyosha mikono yao juu ili kutoa michango yao kuhusu suala letu. Lakini, hebu tumsikilize mzazi yule ili tukamilishe mazungumzo yetu. Karibu sana!

**Mshiriki wa sita:** Kiongozi na wasikilizaji washiriki wenzangu! Ni lazima tuelewe kwamba mtoto hulelewa na watu wote wanaomzunguka kwani hawa nao wana nafasi kubwa kwa kumwathiri vizuri au vibaya kulingana na mienendo na tabia zao. Mtoto afikapo shuleni, malezi yake huwa zaidi mikononi mwa walimu na viongozi wa shule ambao hufanya kazi kubwa ya kuwalea watoto na kuwaelimisha. Watoto humaliza muda mrefu mikononi mwa walimu na viongozi wa shule wanaomsaidia kurekebisha tabia mbaya na kuendeleza tabia nzuri huku wakimpa elimu itakayomfaa katika maisha yake. Mbali na hayo, mtoto akitembea barabarani, njiani na akienda kwingine anakotumwa na wazazi wake hukutana na watu ambao si wazazi wake, mtoto akipewa ruhusa ya kwenda kuangalia familia yake pana hukutana na watoto wengine katika familia hizo na hata watu wengine ambao si wazazi wake.

Kwa hivyo, mimi ninaona kuwa watu wote wanaomzunguka mtoto kuanzia wale wanaokaa naye nyumbani kama vile wazazi wake, ndugu zake na watumishi wa nyumbani, majirani na wengine ambao hukutana naye nao wanaweza kuathiri sana malezi ya mtoto. Ni mara ngapi tunasikia habari kwamba watoto wameathiriwa na watumishi wa nyumbani kwa kujiingiza katika vitendo na mienendo mibaya kama vile uzinzi, ulevi, matumizi ya maneno yasiyo na maadili, na kadhalika?

Haya yote yanathibitisha kwamba malezi ya watato yanahusu watu wote wanaomzunguka mtoto na kwamba wito unapaswa kutolewa kwao ili watambue wajibu wao wa kumlea mtoto huyo. Wazazi humwelekeza mtoto wakati angali mchanga lakini aanzapo kwenda shuleni na kukutana na watu wengine, nafasi ya wazazi katika malezi yao huendelea lakini wanaomwathiri zaidi huwa ni watu wote anaokutana nao katika shughuli zake mbalimbali. Asante sana kwa kunitega sikio; hayo ndiyo yamekuwa maoni yangu.

**Kiongozi**: Ninakushukuru sana kwa maelezo yako. Nasikia kwamba wewe unatilia mkazo kwamba watu wote wanapaswa kutoa mchango wao kwa kumlea mtoto badala ya kufikiria kwamba wazazi ndio wenye nafasi kubwa. Asante sana kwa mawazo hayo. Inaonekana kwamba watu wengi wangependa kutoa mchango wao lakini muda wetu hauturuhusu kuendelea kusikiliza hoja nyingine.

Mjadala wetu unakaribia kufikia mwisho na ningependa kuwapongeza ninyi nyote kwa maoni na mawazo mazuri mliyoyatoa katika mjadala huu. Asante sana kwa wote mlioshiriki katika mjadala huu. Kichwa cha mjadala wa leo kilikuwa "**MCHANGO WA WAZAZI KATIKA MALEZI YA WATOTO WAO.**" Miongoni mwa hoja mlizozitoa ni wajibu wa wazazi kuwalinda watoto kutumia dawa za kulevya, kuwapeleka watoto shuleni na kufuatilia masomo na mienendo yao kokote wanakoenda. Viongozi

wa shule na walimu nao wanapaswa kushirikisha wazazi katika malezi ya watoto wao na kushauriana nao ili kumrekebisha mtoto na kumpatia mawaidha muhimu katika shughuli anazozifanya. Watu mbalimbali nao kama vile majirani, watumishi wa nyumbani na wengine wanaokutana na mtoto hutakiwa kuelewa kwamba wanaweza kumwathiri mtoto huyo vizuri au vibaya. Kwa hivyo, ni lazima nao watoe mchango wao kumlea mtoto kwa kumwonyesha mienendo mizuri. Waheshimiwa mabibi na mabwana hoja zote mlizozitoa zimezingatiwa na zimeeleweka vizuri. Asante sana kwa mchango wenu katika kupigania malezi bora kwa watoto wetu. Mjadala wa leo unaishia hapa. Njooni tena wakati mwingine kwa mada nyingine. Ahsanteni sana kwa kushiriki.

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Malezi ya msingi mtoto huyapata wapi?
2. Dawa za kulevya zina madhara gani kwa maisha ya vijana?
3. Kwa nini mzazi ana wajibu wa kuwapeleka watoto shuleni?
4. Eleza nafasi ya Serikali katika malezi ya watoto kama ilivyozungumziwa katika mjadala huu.
5. Viongozi na walimu hutakiwa kufanya nini kwa kuzingatia nafasi ya wazazi katika malezi ya watoto wao?

## 4.2. Msamiati kuhusu “Maandalizi na utekelezaji wa mjadala”

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo yanayotumika katika mjadala:**

1. mchango
2. elimu
3. dawa za kulevya
4. kulea
5. serikali

## KAZI YA 4

**Husisha maneno yaliyoko katika sehemu A na maelezo yaliyopo katika sehemu B.**

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|
| 1) kutia motisha | a) jambo linalomlazimu mtu kulitimiza. |
| 2) jukumu | b) matendo ya mtu yanayojirudiarudia/tabia |
| 3) mshiriki | c) kukataza jambo kufanyika. |
| 4) malezi | d) ada ya shule inayotolewa na mwanafunzi. |
| 5) kuathiri | e) mpango fulani wa maendeleo k.v. ya nchi unaotarajiwa kutimizwa au uliokwisha anzwa. |
| 6) mwenendo | f) mtu anayeshiriki kufanya jambo fulani k.v. michezo au semina. |
| 7) kukiuka | g) kufanya isivyostahili. |
| 8) karo | h) kushawishi mtu kufanya jambo. |
| 9)kupiga marufuku | i) njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajiwa kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. |
| 10) mradi | j) kumtia mtu mwingine hamu zaidi ya kufanya jambo. |

### 4.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi visisitizi

## KAZI YA 5

**Badilisha sentensi hizi kwa kutumia visisitizi**

**Mfano:** Mahali **humo** mna watu wengi sana.

Mahali **humo humo/mumo humo** mna watu wengi sana

1. Pahali hapa hapapitiki wakati wa mvua nyingi.
2. Mahali kule kunavutia.
3. Darasani humo mna usafi kabisa!

### Maelezo muhimu

Vivumishi visisitizi katika ngeli ya Pa-M-Ku vinatumika kama ifuatayo:

| Ngeli | Nomino | Visisitizi | | | Mifano katika sentensi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Karibu | Mbali kidogo | Mbali sana | |
| Pa | Pahali | Hapa hapa | Hapo hapo | Pale pale | Pahali hapa hapa hapapitiki. |
| | | Papa hapa | Papo hapo | | Pahali papo hapo hapapitiki. |
| | | | | | Pahali pale pale hapapitiki. |
| Ku | Mahali | Huku huku | Huko huko | Kule kule | Mahali kuku huku kunavutia. |
| | | Kuku huku | Kuko huko | | Mahali huko huko kunavutia. |
| | | | | | Mahali kule kule kunavutia. |
| Mu | Mahali | Humu humu | Humo humo | Mle mle | Mahali humu humu mna usafi. |
| | | Mumu humu | Mumo humo | | Mahali humo humo mna usafi. |
| | | | | | Mahali mle mle mnavutia. |

## 4.4. Matumizi ya lugha: Maandalizi na utekelezaji wa mjadala

### KAZI YA 6

Soma maelezo muhimu hapo chini kisha ujibu swali linalofuata:

**Mambo ya kuzingatia katika maandalizi na utekelezaji wa mjadala**:

- Kuandaa chumba cha mazungumzo,
- Kuandaa vifaa maalum vinavyohitajika kama vile viti, meza, vipazasauti, nk.
- Kutumia vizuri muda uliopangwa,
- Kuepukana na fujo na kelele,
- Kupaza sauti unapotoa hoja kuhusu mada,
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala,
- Kutumia lugha isiyo ya matusi,
- Kuwaheshimu wengine,
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa.

**Swali**

- Jadili mambo muhimu ya kuzingatia katika uandalizi wa mjadala na utekelzaji wake.

## KAZI YA 7

**Chagua na uandike neno lifaalo baina ya yaliyomo katika mabano:**

1. Kiumbe kinachozaliwa hasa na mtu. (mtego, mtoto, moto).
2. Kufundisha mtu au kumpa maarifa (kukumbuka, kuelimisha, kusoma).
3. Mtu anayemtunza, kumhudumia na kumfundisha mtoto mpaka akue (mlezi, kiongozi, baharia).
4. Mtu aliye karibu na mahali unapoishi. (jinsia, jirani, jivu).
5. Maelezo yanayoweza kupingwa au kuungwa mkono na watu wengine katika majadiliano (hoji, hoja, hoi).
6. Mahali ambapo wanafunzi hufundishwa elimu k.v. kusoma, kuandika, hesabu na masomo mengine (shuli, shule, shume).
7. Mazoea yanayotokana na kurudiarudia hali, mwenendo au matendo. (tabibu, tabia, tabasamu).

## 4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

## KAZI YA 8

**Jadiliana na mwenzako kuhusu mada ifuatayo kisha mwasilishe maoni yenu kwa darasa:** "Faida na hasara za kuishi katika miji mikubwa."

## 4.6. Kuandika

## KAZI YA 9

**Kwa kuzingatia matumizi ya ngeli ya PA-M-KU, andika mjadala kwenye kurasa mbili kuhusu *"Malezi bora nchini Rwanda."* Toa maoni yako kwa kuonyesha namna serikali na taifa zima linavyoweza kuwasaidia wanafunzi.**

## TATHMINI YA MADA YA PILI

1. Toa maana ya mjadala.
2. Eleza mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala.
3. Eleza mambo ya kujiepusha katika mjadala.
4. Mjadala unaongozwa na nani? Anafanya kazi gani?
5. Tumia vivumishi visisitizi katika sentensi hizi:
   a. Mahali huku ni kuzuri.
   b. Barabarani mle mna changarawe nyingi.
   c. Mahali hapo hapapitiki katika majira ya Masika.
6. Tumia kiulizi –pi kuulizia swali
   a. Mahali huku kuna hewa nzuri.
   b. Mahali mle mna chaki za rangi.
   c. Mezani huku hakupelekwi chakula.
7. Tunga mjadala kuhusu mada “Shule za mabweni ni bora kuliko shule za kutwa.” Usizidi ukurasa mmoja.

# MADA 3

# UTUNGAJI WA BARUA ZA KIRAFIKI, MWALIKO NA MATANGAZO

**Uwezo mahususi wa mada:**

Kuandika barua za kirafiki, mwaliko na matangazo kwa watu mbalimbali

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutaja sehemu kuu za barua za kirafiki, mwaliko na matangazo
- Kuchunguza muundo wa barua za kirafiki, mwaliko na matangazo
- Kutofautisha aina za barua za kirafiki, mwaliko na matangazo
- Kuelezea lugha inayofaa kutumiwa katika uandishi wa barua, mwaliko na matangazo
- Kutunga barua za kirafiki kwa watu mbalimbali, barua za mwaliko na matangazo ya aina tofauti
- Kuonyesha adabu na hehima kwa watu anaowaandikia
- Kutumia kwa usahihi majina na vivumishi vya ngeli ya PA-M-KU katika uandishi wa barua za kirafiki, mwaliko na matangazo.

## KIDOKEZO

**Tazama kwa makini mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini:**



**Jibu maswali yafuatayo**

- Ni nini unachokiona kwenye mchoro huu?
- Ni mambo gani tunayotumia kwa kuwasiliana kimaandishi?

# SOMO LA 5: BARUA YA KIRAFIKI

## 5.1. Kusoma na ufahamu: Barua ya kirafiki

**Soma barua ifuatayo kisha ujibu maswali ya ufahamu.**

**Shule ya Sekondari ya Amahoro**<br>
**S.L.P. 102,**<br>
**HUYE**

16/07/2020

**Mpendwa Gahamanyi,**

Salamu!

Ninakuandikia waraka huu nikiwa nimejaa furaha ghaya kama mzazi aliyejifungua pacha salama salimini. Wewe u mzima? Wazazi wako hawajambo? Nasi hapa nyumbani kwetu Huye mambo ni shwari!


Nia yangu ya kukuandikia barua hii ni kukushukuru kwa dhati ya moyo wangu. Zaidi ya hayo ni kule kunialika kuja katika harusi ya dada yako huko kwenu. Harusi ile ilikuwa ya kukata na shoka kabisa. Ilinivutia sana, hasa nilivyoona kwamba harusi yenyewe ilionyesha utamaduni wetu wa Wanyarwanda bila kuchanganya mambo ya kizungu. Hilo ni jambo nadra sana siku hizi wakati ambapo watu wengi wamebobea uzunguni. Harusi ilionyesha mitindo ya asili na jadi. Ajabu ni kwamba shaibu na ajuza walikuwa kwenye mstari wa mbele katika shamrashamra kwa nderemo na vigelegele. Bibi na bwana arusi nao walikuwa wakipendeza mno na wakachagua kufanana sana kama mboni za macho. Ninawatakia maisha mema.

Zaidi ya hayo, usafi uliokuwa nyumbani kwenu ulikuwa wa kuvutia. Ugani kulikuwa kunametameta na kupendeza kutokana na maua yaliyokuwa yakitoa harufu nzuri. Vyakula na vinywaji vilivyoandaliwa mezani vilikuwa safi kwa kuwa havikuleta madhara kwa yeyote yule.

Isitoshe, ninakushukuru tena kwa msaada ulionipatia ukanisaidia masomoni wakati tulipokuwa shuleni. Msaada wako ulinifaa zaidi kwa sababu niliweza kushinda vizuri. Jambo hili lilinionyesha kwamba u rafiki wa kweli. Unajua? Nilipofika nyumbani wazazi wangu walinichinjia jogoo! Nami wakati wowote ule utakapohitaji msaada kutoka kwangu niko tayari kukupatia kwa kuwa akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki.

Kisha, nisalimie wote hasa wazazi wako na ndugu zako, maana walinishughulikia kupita kiasi. Kwa hakika, ninashindwa niandike yapi hata waweze kuelewa upeo wa furaha yangu.

Wako,



Kamaliza Amina

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

a. Ni nani aliyeandika barua hii?
b. Taja jina la aliyeandikiwa barua.
c. Mwandikaji wa barua anasomea katika shule gani?
d. Mwandikaji barua anaishi wapi?
e. Madhumuni ya barua hii ni yapi?
f. Jaza methali hii, kisha uieleze: « Akufaaye kwa dhiki.......... »

## 5.2. Msamiati

## KAZI YA 2

**Baada ya kusoma barua ya hapo juu, eleza maneno yafuatayo:**

- Waraka
- Ghaya
- Salimini
- Shwari
- Nia
- Dhati
- Ya kukata na shoka
- Nadra
- Wamebobea
- Nderemo

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

- Madhara:
- Jogoo:
- Ghaya:
- Ugani:
- Pacha:

## KAZI YA 4

**Twasema "*salama salimini*". Hapa tutasema namna gani?**

- Kwa udi na……….
- Kwa makofi na……..
- Kwa nderemo na ………
- Kwa shibe na …………..
- Kwa kufa na……………

## 5.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU

## KAZI YA 5

**Angalia sentensi zifuatazo ukichunguza majina yaliyopigiwa mstari na matumizi yake katika sentensi hizo.**

a. **Barabarani pa**mechafuka.
b. **Mezani ku**na sahani mbili.
c. **Mfukoni** mwangu **m**na fedha nyingi.
d. **Chumbani** humu **m**na wanafunzi.
e. **Mahali** hapa **pa**mesafishwa.

### Maelezo muhimu

- Majina yaliyopigiwa mistrari yamo katika ngeli ya **PA-M-KU.**
- Majina ya ngeli hii si mengi sana. Kwa hiyo, Kiswahili kilichagua kupachika kiambishi –ni mwishoni mwa majina ya kawaida ili kupata majima ya ngeli hii.

**Mifano:**

- Chumba+**ni**: chumbani
- Chupa+**ni**: chupani
- Kichwa+ **ni**: kichwani
- Mfuko+**ni**: mfukoni
- Meza+**ni**: mezani

- Katika kitenzi, ngeli hii huwakilishwa na viambishi **pa-, m-** na **ku-.**

- **Pa-:** huonyesha mahali panapotambulika.
- **M-:** huonyesha ndani ya.
- **Ku-:** huonyesha juu ya na mahali pasipotambulika.

## KAZI YA 6

**Tumia viambishi mwafaka katika sentensi zifuatazo:**

a. Darasani –na wanafunzi.
b. Nyumbani kwetu –nanukia sana.
c. Kichwani –na upara.
d. Mahali hapa –safishwa.
e. Chumbani –mechafuka.

## KAZI YA 7

**Ondoa neno "*katika*" ndani ya sentensi zifuatazo:**

**Mfano:** Simba anaishi **katika** msitu: Simba anaishi **msituni**.

a. Nyoka ameingia katika shimo.
b. Ameweka fedha katika mfuko.
c. Wao husomea katika ghorofa.
d. Katika nchi ya Rwanda kuna amani.
e. Wazazi wetu walikuwa wakichotea maji katika mitungi.

## 5.4. Matumizi ya lugha

## KAZI YA 8

**Soma upya barua uliyopewa kisha utoe maana ya barua ya kirafiki na uonyeshe sehemu zake kuu.**

**Maelezo muhimu kuhusu barua ya kirafiki**

**a. Maana ya barua**


Barua au waraka ni maandishi yaliyopangwa kwa utaratibu na mtiririko maalum kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe fulani. Barua ni risala au mjumbe mwepesi anayemwakilisha mtungaji wake kwa mtu mwingine na kuwasilisha taarifa yake kwa mtu huyo.

Barua huandikwa kwa madhumuni mbalimbali kama kuarifu, kuomba kitu kama vile kazi, ruhusa; kuagiza bidhaa, n.k.

Kuna aina tatu za barua:

- **Barua za kikazi** zenye madhumuni ya kazi.
- **Barua za mwaliko** zenye lengo la kualika mtu katika sherehe au sikukuu fulani
- **Barua za kirafiki** : ni zile ambazo huandikiwa na mtu au watu mbalimbali walio na uhusiano wa karibu na anayeandika ; kv. rafiki, mzazi, ndugu, n.k. Barua hizi zina uhuru mkubwa katika kuziandika. Hazidai utaratibu wa kipekee sana. Mtu huwa huru kuandika apendalo ilimradi halimvunjii mtu heshima yake.

**b. Sehemu za barua ya kirafiki**




- **Anwani ya mwandikaji na tarehe:** huandikwa kwenye pembe ya juu upande wa kulia wa karatasi. Mwandikaji anaandika mahali anapoandikia barua (au anapoishi). Anaweza kuongeza nambari za sanduku la posta (S.L.P…) na mji, nambari ya simu na akaunti ya barua pepe. Tarehe huandikwa chini ya anwani kwa kuacha nafasi ya mstari mmoja.
- **Jina la mwandikiwa :** huja chini ya tarehe lakini kwenye upande wa kushoto.
- **Salamu :** sehemu hii hutoa maamkizi kwa mwandikiwa na huandikwa chini ya jina la mwandikiwa.

- **Utangulizi :** hujitokeza katika aya ya kwanza. Mwandikaji hujumlisha mambo ya hali yake, hali ya anayemwandikia na hata wenzake.
- **Barua yenyewe :** huu ni ujumbe kamili wa barua. Mwandikaji anaweza kutumia aya moja au zaidi kulingana na urefu wa barua yake.
- **Hitimisho la barua :** ni sehemu ya mwisho ya barua. Sehemu hii huandikwa kwa aya moja na hujumlisha mambo ya kumuaga mwandikiwa. Kwenye sehemu hii unaongeza maneno ya kuvutia (Wako, Wako mpendwa, Mwanako, Wako mwaminifu, n.k.). Maneno haya huandikwa kwenye upande wa kulia kabla ya kutia sahihi.
- **Sahihi ya mwandishi :** huja chini ya hitimisho lakini kwa upande wa kushoto.
- **Jina la mwandikaji :** huja chini ya sahihi ya mwandikaji.

**c. Aina za barua za kirafiki**

Barua za kirafiki zinaweza kuwa mwana kwa mzazi au mzazi kwa mwana, za mapenzi, za kindugu (kati ya ndugu), za kijamaa, n.k.

## 5.5.Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 9

**Tunga barua kwa jamaa fulani kisha uisomee wenzako hadharani kwa kuonyesha vitabia**

### KAZI YA 10

**Jadiliana na wenzako kuhusu mada hii « *Barua ni nusu ya kuonana.* »**

## 5.6. Kuandika

### KAZI YA 11

**Waandikie barua wazazi wako ukiwajulisha hali yako ya shuleni**

## KAZI YA 12

**Mwandikie barua rafiki yako ukimwomba kuenda pamoja kutembelea Mbuga ya Wanyama ya Akagera.**

# SOMO LA 6: BARUA YA MWALIKO

## 6.1.Kusoma na ufahamu: Ndoa ya dadangu

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali ya ufahamu.**

Ilikuwa Jumamosi tarehe 15 mwezi wa Juni wakati nilipohudhuria harusi ya dada yangu Mukeshimana Roza aliyefungana pingu za maisha na Kalisa Joni. Harusi yenyewe ilikuwa ya kufana sana.

Kabla ya wiki mbili za arusi kufanyika familia mbili zilikuwa katika pilikapilika za hapa na pale ili kuandaa sherehe hii ya harusi. Kwa upande wa familia yangu sisi watoto tulikuwa tukitumwa huku na kule kwa kuwaalika watu watakaohudhuria harusi hii. Wazazi wangu waliwaalika wazee majirani na dada yangu akawaalika wenzake hasa wa rika lake. Wote walikuwa wakipelekewa barua za mialiko.

Siku moja kabla, nyumbani kwetu tulifanya usafi na majirani walikuja kumsaidia baba kutayarisha pombe ya mtama, ya ndizi na juisi. Wengine walikuwa wakipamba uga na kujenga nyumba za mahema. Uga wenyewe ulikuwa wa kupendeza sana.

Siku hiyo ilipowadia watu walimiminika kuelekea nyumbani kwetu. Asubuhi majira ya saa nne hivi, familia ya bwana harusi ilifika kwetu na kukaribishwa kwa taadhima. Walikuwa wamekuja kuposa na kutoa mahari. Waliandaliwa vyakula na vinywaji mezani wakafurahi sana. Furaha yao ilipandishwa na nyimbo pamoja na ngoma za wachezaji waliokuwa hapo.

Baada ya hapo, Bi harusi alivishwa veli. Bwana harusi alirudi kumchukua akiwa na gari la kifahari. Alimkabidhi shada la maua sote tukawapigia makofi, kisha wakaenda kanisani ili kuvishana pete mbele ya Mungu. Nasi tuliandamana nao tukiwa katika magari kadhaa. Watu walipoona mlolongo wa magari hayo waliduwaa wakidhani kuwa kulikuwa na kongamano la kimataifa katika kijiji chetu.

Tulipotoka kanisani, tulifurika bustanini kama ilivyoelezwa kwenye barua za mwaliko walizopewa watu. Watu walikuwa wengi sana na sherehe ilikuwa ya kupendeza sana. Tuliandaliwa vinywaji na vyakula tele tele. Bi harusi na Bwana harusi walipewa zawadi mbalimbali kama vile mikungu ya ndizi, mifuko ya

mchele, chupa za asali iliyokamuliwa kutoka kwa masega ya nyuki, mapambo ya aina tofauti, n. k. Watu wote walifurahi sana na kucheza ngoma na nyimbo za utamaduni.

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

a. Harusi inayosimuliwa ilifanyika lini?
b. Harusi hiyo ilikuwa ya kina nani ?
c. Ni vinywaji gani vilivyotayarishwa siku moja kabla ya sherehe?
d. Watu waliokuja harusini walipataje habari hizo?
e. Kwa sababu gani watu walioona magari walishangaa?

## 6.2.Msamiati

## KAZI YA 2

**Eleza maneno yafuatayo:**

a. Aliyefungana pingu za maisha
b. Pilikapilika
c. Kuandaa
d. Mahema
e. Taadhima

## KAZI YA 3

**Jaza mapengo kwa kutumia makundi ya maneno yafuatayo:** mlolongo wa, mkungu wa, masega ya, ilifana, shada la.

a. Harusi yenyewe ……….. sana watu wote wakafurahi.
b. Alipofunga ndoa alitunukiwa……maua.
c. ……nyati ulifunga barabara ulipokuwa ukigura.
d. Nyanya aliwaletea wajukuu wake……….ndizi.
e. Mzingani mle mna ……….nyuki.

## KAZI YA 4

**Tafuta majina ya vinywaji na vyakula kwenye jedwali hili:**

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | G | A | L | I | M | B | V | H | J |
| P | I | L | I | P | I | L | I | T | U |
| P | I | P | O | M | B | E | A | U | I |
| D | Z | I | I | B | O | Z | Z | N | S |
| W | A | L | I | L | G | Y | I | S | I |
| F | R | A | L | K | A | U | P | O | V |
| T | Y | U | J | I | K | P | O | D | G |
| M | C | H | U | Z | I | K | K | A | O |

## 6.3. Sarufi: Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vyake

## KAZI YA 5

**Tazama sentensi zifuatazo kisha ueleze maneno yaliyopigiwa mistari:**

a. Nyumbani **humu** mna usafi.

a. Mezani **kwetu** kuna vitabu vingi.

a. Safisha mahali **hapa**.

a. Chumbani **mwangu** mna giza totoro.

a. Mahali **penyewe** ni hapa.

### Maelezo muhimu

Maneno yaliyopigiwa mistari ni vivumishi. Vivumishi hivi vikitumiwa katika ngeli ya PA-M-KU huchukua viambishi vya ngeli hii (PA-M-KU).

**Mifano :**

- **Vivumishi vya kumiliki**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| Chumbani **mwangu** | Chumbani/vyumbani **mwetu** |
| Chumbani **mwako** | Chumbani/vyumbani **mwenu** |
| Chumbani **mwake** | Chumbani/vyumbani **mwao** |
| Mezani **kwangu** | Mezani **kwetu** |

| | |
|---|---|
| Mezani **kwako** | Mezani **kwenu** |
| Mezani **kwake** | Mezani **kwao** |
| Mahali **pangu** | Mahali **petu** |
| Mahali **pako** | Mahali **penu** |
| Mahali **pake** | Mahali **pao** |

- **Vivumishi vya kuonyesha**

  a. Chumbani **humu/humo/mle**
  b. Mezani **huku/huko/kule**
  c. Mahali **hapa/hapo/pale**

- **Vivumishi vya kurejesha**

  a. Mfukoni **mwenyewe**
  b. Mezani **kwenyewe**
  c. Mahali **penyewe**

## KAZI YA 6

**Jaza nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia kivumishi mwafaka.**

a. Alitia maji mtungini.............(pale, kule, mle, yule).
b. Nyumbani ......... kuna wanyama wengi wa mifugo (mwetu, petu, kwetu).
c. Mezani....... hakuna uchafu (humu, huku, hapa, mule)
d. Mahali .........pamejengwa nyumba nzuri (mwenyewe, kwenyewe, penyewe)
e. Nimekutunza moyoni......(kwangu, pangu, mwangu)

## 6.4. Matumizi ya lugha: Maana ya barua ya mwaliko

## KAZI YA 7

**Jibu maswali yafuatayo:**

a. Mtu anapowakaribisha wengine karamuni anatumia nini?
b. Mtu anaweza kuwaalika wengine kwa madhumuni gani?

**Maelezo muhimu kuhusu barua za mwaliko**

a. **Maana ya barua za mwaliko**

Barua ya mwaliko ni ujumbe unaotolewa kwa kumkaribisha mtu kuhudhuria shughuli au hafla fulani. Barua za mwaliko zinaweza kuwa na madhumuni yafuatayo:

- Sherehe
- Karamu
- Harusi
- Ubatizo
- Sikukuu ya kufunga mwaka
- Sikukuu ya kupata cheti au digrii
- Kuadhimisha miaka fulani
- n.k

b. **Mambo ya kuzingatiwa katika uandishi wa barua ya mwaliko**

1. Jina la mwalikwa
2. Sababu ya mwaliko
3. Mahali ukaribisho utakapofanyika, tarehe na saa
4. Jina na anwani ya mkaribishaji

c. **Mifano ya barua za mwaliko**

- Barua ya mwaliko kwenye harusi

Jamaa ya **Bwana** na **Bibi Gakwaya** na **Bwana** na **Bibi Rwema** zinayo furaha kubwa ya kuwaalika **Bwana na Bibi Murenzi** kwenye sherehe ya arusi ya wanao **Kanyana** na **Mugabe** itakayofanyika tarehe 20.05.2020, saa kumi magharibi katika Kanisa ya Mtakatifu Mariko Kabusunzu Mjini Kigali na baadaye kwenye tafrija katika bustani ya Hoteli Ibyiza.

Kufika kwenu ndiyo furaha yetu!

GAKWAYA Martini

SLP 35

KIGALI

- Barua ya mwaliko kwenye sikukuu ya kuzaliwa

15.10.2019

**Rafiki yangu Jenifa,**

Karibu ushiriki nami katika sherehe ya sikukuu yangu ya kuzaliwa tarehe 20/10/2020. Tarehe hiyo nitakuwa nimetimiza miaka ishirini. Sherehe itafanyika nyumbani kwetu saa mbili usiku.

Karibu sana

**Zuhla Akazuba**

## 6.5.Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 8

**Shirikiana na wenzako mzungumzie kuhusu umuhimu wa uandishi wa barua za mwaliko.**

## 6.6.Kuandika

### KAZI YA 9

**Mkaribishe mwenzako katika sikukuu yako ya kuzaliwa.**

# SOMO LA 7: MATANGAZO

### KAZI YA 1

**Tazama kwa makini mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyotolewa hapo chini:**



Jibu maswali yafuatayo:

1. Ni nini unachoona kwenye mchoro huu?
2. Unafikiri kuwa mtu huyo mwenye kipazasauti anafanya nini?

## 7.1. Kusoma na ufahamu: Laiti ningefuata tangazo redioni.....



**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali ya ufahamu.**

**Gapfizi:** Hujambo !

**Maria:** Sijambo! Wewe je?

**Gapfizi:** Mbona wajifunika gubigubi ! Na joto kama hili ungali na kabuti? Mimi siwezi kuvaa namna hiyo. Kujifunika kama mahindi?

**Maria:** Huoni kuwa mvua inakaribia kunyesha?

**Gapfizi:** Leo haitanyesha. Anga linang'aa…

**Mariya:** Asubuhi hii umesikiliza redio? Wametangaza kuwa mvua itanyesha leo hii. Tazama angani! Huoni kwamba maghubari yamejitanda?

**Gapfizi**: Watabiri wale wanatudanganya. Kuna wakati wao husema kinyume.

**Maria**: Ukumbuke kwamba ni wanasayansi ya anga. Na wao hujaribu kutoa habari ya mambo yatakayotokea kwa kutumia mitambo ya kisasa ya kuchunguzia hali ya hewa.

**Gapfizi**: Nielezee basi waliyoyasema leo. Mimi sikupata muda wa kusikiliza redio!

**Maria**: Wao wamesema kuwa mvua itanyesha leo saa za mchana. Unakumbuka kuwa dalili ya mvua ni mawingu. Tazama angani! Na tena leo asubuhi serikali imewatangazia raia kuwa msimu huu mvua itakuwa nyingi sana. Ndiyo maana inawahamasisha raia mambo yafuatayo :

- Kusafisha mifereji ya kupitisha maji
- Kufunga vizuri mapaa ya nyuma kwa kutumia kamba na nyaya
- Kutoka katika maeneo hatarishi
- Kutotumia simu mvua inaponyesha
- Kutofungua vifaa vinavyohitaji umeme mvua inaponyesha
- Kutojikinga chini ya miti mvua inaponyesha.

**Gapfizi**: Kumbe ni hayo? Na tangazo hilo lilitolewa na nani?

**Maria:** Tangazo limetolewa na Waziri wa Serikali za Mitaa na Uongozi Bora.

**Gapfizi**: Kama ni yeye ninaamini maneno yako. Nilifikiri kwamba ni fununu. Na wakati mvua itakapoanuka tutafanya nini?

**Mariya**: Tutasafisha mazingira yetu kwa kutengeneza njia na barabara hasa kwa kuzibua mifereji au mitaro ya kupitishia maji. Tutaendelea na shughuli za kilimo hasa mabondeni na tutaendelea kupanda miti ili tupambane na jangwa.

**Gapfizi**: Ninashukuru kwa mashauri yako mema. Ebu nirudi nyumbani haraka. Laiti ningefuata tangazo la redioni ningekuja na mwavuli.

**Maria**: Kwaheri!

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Mazungumzo haya yanahusu nini?
2. Kwa sababu gani Maria alivaa kabuti ?
3. Gapfizi alikuwa akivaa namna gani ?
4. Taarifa za kunyesha kwa mvua Maria alizipata wapi ?
5. Kwa sabu gani Gapfizi aliamua kurudi nyumbani?

## 7.2. Msamiati kuhusu uandishi wa matangazo

### KAZI YA 3

**Eleza maneno yafuatayo:**

a. Wajifunika gubigubi
b. Kabuti
c. Anga
d. Mawingu
e. Watabiri
f. Fununu

### KAZI YA 4

**Twasema amejifunika kama mahindi. Hapa tutasema namna gani?**

a. Analinga kama.........
b. Wao wamekonda kama........
c. Yeye ni mfupi kama.......
d. Jambo hili ni la lazima kama.......
e. Si vizuri kuwa mjanja kama..............

### KAZI YA 5

**Taja na kueleza misimu/majira yanayopatikana nchini Rwanda**

## 7.3.Sarufi : Matumizi ya ngeli ya PA-M-KU na vivumishi vyake

- **Vivumishi vya kuunganisha**
  a. Chumbani **mwa** mtoto.
  b. Nyumbani **kwa** Gapfizi
  c. Mahali **pa** kuchezea
- **Vivumishi vya sifa**
  a. Mahali **pazuri**
  b. Mezani **kuzuri**
  c. Chumbani **mzuri**

### KAZI YA 6

**Jaza mapengo kwa kutumia kivumishi mwafaka.**

a. Nyoka aliingia chumbani.....Kagabo (kwa, pa, cha, mwa).
b. Mezani huku ni.....(pazuri, mzuri, vizuri,kuzuri)
c. Mahali hapa ni.........kulima (ya, kwa, mwa, pa)
d. Tumboni .......kila mtu kuna ini (kwa, pa, mwa, ya)
e. Nyumbani......wazazi wake hakuna maji safi (mwa, pa, ya, kwa)

## 7.4. Matumizi ya lugha: Maana ya tangazo

### KAZI YA 7

**Soma upya mazungumzo kisha ujadiliane na wenzako kuhusu *maana ya matangazo* na *aina za matangazo.***

### Maelezo muhimu kuhusu matangazo

**a. Maana ya tangazo**

Tangazo ni mpangilio wa maandishi kwa mtindo maalumu kwa lengo la kupasha habari ama kupokezana ujumbe muhimu. Taarifa inayosambazwa kwa tangazo inaweza kuwa kifo, mkutano, taratibu za kutumia barabara vizuri, kazi na mengineyo. Aghalabu, tangazo linalotahadharisha watu kuepuka kufanya jambo fulani huitwa ***ilani***. Kwa mfano, kuna ***ilani kuhusu mkurupuko wa ugonjwa, ilani kuhusu unywaji na ulevi, ilani ya kutokanyaga nyasi,*** n. k.

**b. Aina za matangazo**

Zipo aina nyingi za matangazo

i. Matangazo ya kibiashara

ii. Matangazo ya kifo

iii. Matangazo ya serikali

iv. n.k

**c. Mambo ya kuzingatiwa katika uandishi wa matangazo**

Kwa kuandika tangazo ni lazima kuzingatia mambo yafuatayo :

- Kichwa cha tangazo
- Kutaja anayetoa tangazo
- Kutaja walengwa wa tangazo
- Ujumbe wa tangazo (maudhui)
- Sahihi na jina la anayetoa tangazo (tangazo lisilokuwa na sehemu hii huitwa **tetesi, fununu au uvumi**)

**d. Mfano wa tangazo**

**TANGAZO LA TANZIA/ KIFO**

Familia ya **Bwana Mussa** anayeishi Ngoma-Huye inayo masikitiko makubwa ya kuwatangazia jamaa, ndugu na marafiki kifo cha mtoto wao Akimana kilichotokea jana kutokana na ajali ya gari. Tangazo liwafikie:

- Familia ya Bw. Kamana anayeishi jijijni Kigali
- Familia ya Bw. Murekezi anayeishi wilayani Musanze
- Bw. Butera anayesomea Ufaransa
- Watu wote waliosoma pamoja na marehemu katika shule za msingi, sekondari na chuoni.

Mazishi yatafanyika katika Makaburi ya Pamoja ya Matyazo (Ngoma-Huye) tarehe 18/07/2020 saa nane baada ya ibada itakayosomewa katika kanisa la Parokia ya Ngoma. Mungu amrehemu mahali pema.

**Bwana Mussa**

## 7.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 8

**Sikiliza matangazo redioni kisha ujadiliane na wenzako kuhusu yanayozungumziwa katika matangazo hayo.**

## 7.6. Kuandika

### KAZI YA 9

**Tunga tangazo la kibiashara na kuliwasilisha mbele ya darasa.**

### TATHMINI YA MADA YA TATU

1. Eleza maana ya barua.
2. Taja aina za barua tulizozionа.
3. Zitaje sehemu kuu za barua ya kirafiki.
4. Ni mambo gani muhimu yanayopaswa kuonekana kwenye barua ya mwaliko?
5. Tunga tangazo la kazi.
6. Eleza jinsi ya kuunda maneno ya ngeli ya PA-M-KU- ukitoa angalau mifano mitano.

# MADA 4

# UTUNGAJI WA INSHA ZA WASIFU

## Uwezo mahususi wa mada


Kutunga insha za wasifu kwa kuzingatia kanuni husika.

**Malengo ya ujufunzaji:**

- Kueleza maana ya insha za wasifu na umuhimu wake.
- Kubainisha sehemu kuu za insha za wasifu.
- Kuonyesha sifa za insha za wasifu.
- Kutaja na kutumia kwa usahihi alama za vituo.
- Kuchambua insha za wasifu mbalimbali.
- Kutunga insha ya wasifu kulingana na mwongozo wa utungaji wa insha za wasifu.
- Kuelewa na kutumia kwa usahihi kiambishi hali -KA-

## KIDOKEZO

**Angalia mchoro hapo chini na kujadili na mwenzako kuhusu vile mnavyoona kwenye mchoro huo, kisha uwasilishe maoni yako mbele ya darasa.**



# SOMO LA 8: INSHA ZA WASIFU

## 8.1. Kusoma na ufahamu: Insha za wasifu

**Soma kifungu cha habari hiki kisha ujibu maswali ya ufahamu hapo chini**

Wasifu ni maelezo juu ya mambo, matendo na hulka ya mtu au kitu. Maelezo hayo yanawasilishwa kwa mdomo au maandishi. Kwa kawaida, wasifu wa mtu hutolewa na watu wengine. Mtu ambaye anajitolea wasifu husemekana kuwa anajinaki. Wasifu hutolewa katika sherehe mbalimbali. Sherehe hizi ni pamoja na siku ya kuzaliwa, kufunga ndoa, kumaliza kiwango fulani cha masomo, tunzo, kupewa wadhifa, kustaafu, n.k. Lakini wakati mwingine, wasifu husikika katika sherehe za mazishi.

Insha za wasifu ni aina ya utungaji ambao huchora picha ya kitu kinachozungumziwa. Huonyesha waziwazi hisia za msanii. Aghalabu, kuna vitu vingi ambavyo tunaviona kila siku kama vya kawaida lakini mtungaji anaweza akavitungia insha za wasifu na tukaviona katika mtazamo tofauti kabisa. Vilevile, insha za wasifu zinaweza kuwa na usanii.

Insha nzuri inapaswa kuwa sahihi kisarufi. Usafi huu huhusisha muundo wa sentensi na mpangilio wa aya ufaao. Lazima suala linalozungumziwa au yaliyomo ya insha yahusishwe na kichwa cha insha. Insha inapaswa kuepuka utata. Yaani kuwepo kwa maana nyingi kwa maneno yaliyotumiwa katika insha. Pasiwepo na kauli au sentensi ambazo hazionyeshi uhusiano wazi na sentensi nyingine.

Katika kutunga insha ya wasifu, mwandishi anatoa maelezo kuhusu jinsi au maisha ya kitu, mahali au mtu alivyo ama anavyoonekana, yaani sifa zake kitabia, kisura au kimaumbile pamoja na maisha yake. Madhumuni ya insha ya wasifu ni kutaarifu, kuwaelekeza wasomaji kuhusu mambo ili wayafahamu, kuwaeleza wasomaji ili waelewe au watambue kitu au jambo.

Insha ya wasifu, kama insha yoyote ile, inatarajiwa kuwa na urefu wa kutosha. Isiwe ndefu sana wala fupi sana. Aghalabu urefu wa insha unafungamana na mada yenyewe au kinachozungumziwa katika insha hiyo. Haipaswi kuwa mkusanyo wa maneno ya waandishi wengine isipokuwa pale ambapo mwandishi ameweka wazi kuwa anatumia maneno ya wengine. Inapaswa kugawanywa katika muundo wenye sehemu tatu kama ilivyo desturi kwa aina zote za insha. Ni lazima insha ya wasifu iwe na utangulizi mzuri unaojitokeza wazi pamoja, mwili au maelezo yenyewe na mwisho ambao unadhihirika waziwazi.

Insha ya wasifu ina kichwa ambacho ni mada ya insha au kinachozungumziwa. Kichwa hakipaswi kuwa na maneno mengi. Utangulizi nao ni sehemu hii hutanguliza insha.

Sehemu hii huwa na aya moja ambayo haina mistari mingi (labda minane). Hupaswa kuwa na mvuto kwa msomaji na kutoa mwelekezo wa insha yenyewe. Mwili au sehemu kuu: Hii huwa ndiyo hasa insha yenyewe. Mwili wa insha huundwa na aya zinazoendeleza mada ya insha. Kila aya lazima ichangie katika kuliendeleza wazo kuu. Ni vyema kuhakikisha kuwa pana muungano ulio wazi kutoka aya moja hadi nyingine.

Sehemu ya mwisho wa insha ni lazima ivutie kwa kurudilia kwa ufupi yale aliyoyaelezea mwandishi katika insha yenyewe. Yeye huhitimisha insha yake kwa kumwacha msomaji na picha kamili ya jambo alilolizungumzia katika insha nzima.

### KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Eleza maana ya insha ya wasifu.
2. Taja sifa za insha ya wasifu nzuri kwa kuegemea kifungu cha habari.
3. Insha za wasifu zinaweza kutolewa kwa njia gani?
4. Insha za wasifu zinatumiwa wapi?
5. Katika kutunga insha ya wasifu mwandishi anafanya nini?
6. Eleza muundo wa insha ya wasifu.

## 8.2. Msamiati kuhusu insha za wasifu

### KAZI YA 2

**Tumia Kamusi ya Kiswahili Sanifu kutafuta maana ya maneno ambayo yanafuata:**

1. Insha
2. Hulka
3. Kujinaki
4. Muundo
5. Sherehe

## 8.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi cha hali -KA-

### KAZI YA 3

**Chunguza kwa makini sentensi zinazofuata na kutambua kiambishi cha hali kinachorudia katika sentensi ambazo zinafuata:**

1. Mugeni aliendа mjini akanunua madaftari, kisha akarudi nyumbani.
2. Baada ya masomo nilibadilisha mavazi, nikaenda kucheza, nikaoga na kurudi darasani jioni.
3. Mwalimu wetu ni mwenye bidii kwa sababu anatufundisha, akatusahihisha haraka, akaandika vitabu na kutimiza majukumu mengine ya mwalimu.
4. Jana tulijifunza Kiswahili, tukaimba, tukachora na kucheza kabumbu.
5. Kaka yako alinitembelea akanipa zawadi ya kupendeza sana, nami nikamshukuru.

### Maelezo muhimu

Kiambishi simulizi **"ka"** kinatumiwa kusimulia kitendo au vitendo vinavyoandamana au kufuatana. Kitenzi cha kwanza hufuata mtindo wa nyakati za vitenzi wa kawaida ambapo vitenzi vinavyofuata hupata kiambishi **"ka"** kwenye nafasi ya kiambishi cha wakati. Pengine huitwa kiambishi cha wakati usiodhihirika **"ka".**

### KAZI YA 4

**Tunga sentensi kumi zenye kiambishi simulizi "-ka-" cha hali.**

## 8.4. Matumizi ya lugha: Insha za wasifu

### Maelezo muhimu kuhusu utungaji wa insha ya wasifu

Katika kutunga insha ya wasifu, maelezo yanayotolewa wasifu wa mtu yanahitaji mambo kama vile jina lake, sifa zake kimaumbile na kisura, hulka na desturi zake, elimu yake, shughuli anazozipenda na kuzifanya, fikra na falsafa zake pamoja na yale anayoyapenda. Endapo ni wasifu wa mahali, basi mwandishi

anatakikana kutoa maelezo juu ya: jina la mahali hapo, sifa za mandhari ya mahali hapo kama vile majengo yaliyopo (kijiji, mji, hali watu waishimo) na maumbile hasa hasa ya kijiografia.

Mwandishi atahakikisha kwamba anatoa maelezo kwa utondoti; yaani kinaganaga bila ya kuacha mambo yoyote muhimu. Maelezo yawe yanalenga kufunua milango yote ya hisia za msomaji, hususan kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa. Ataeleza mambo kama yalivyo na siyo kama anayadhani katika kutoa picha inayokusudiwa kumfikia msomaji.

Mwandishi apange maelezo katika mtiririko mzuri ulio na mantiki. Yawe na mshikamano baina ya aya na aya. Aeleze taratibu kila kipengele cha mada ili kumwezesha msomaji kupata dhana, hisia na picha kamili ya mtu, jambo au mahali, kitu, ijapokuwa hajapata kukiona. Mahali panapoelezwa hajapata kupafika au mtu anayeelezwa hajapata kumuona lakini anapata picha yake na kumwelewa alivyo.

## KAZI YA 5

**Soma insha ya wasifu ifuatayo na kujibu maswali ya ufahamu yanayoambatana nayo.**

Mukuzo ni kijana ambaye ana tabia ya uvivu hasa hasa darasani. Kila wakati mwalimu wake humuadhibu kwa vuruguvurugu na kwa tabia yake ya kusinzia darasani. Tangu alipoanza masomo yake katika shule za msingi, Mukuzo hakuandika maandishi darasani na kila mwalimu alipowaachia kazi za nyumbani, alimkuta Mukuzo hakuandika chochote daftarini mwake. Katika majaribio na mitihani, yeye alizoea kuiba na kunakili majibu ya wenzake au kumuuliza aliyekaa karibu naye. Mara nyingi alikuwa na vijikaratasi alivyokuwa akitumia kwa kuandika majibu na kuvificha ndani ya dawati lake.

Wazazi wake walijaribu kumfunza tabia ya kuwa na bidii kwa kumwelezea, "Bidii huzaa matunda." Vilevile, wazazi hao walimuonya aepukane na tabia hizo mbaya za uvivu lakini yeye hakusikia. Wao waliamua kushirikiana na walimu wake ili kujaribu kurekebisha tabia zake potovu. Walimuonya aige mfano wa ndugu yake mdogo aliyekuwa amempita kwani wakati huo yeye alikuwa katika shule za upili alipokaribia kuhitimu ilhali Mukuzo alikuwa angali bado katika shule za msingi.

Mukuzo aliendelea na tabia zake mbaya na kufunga masikio kwa kukataa mashauri na maonyo ya wazazi na walimu wake. Wakati wa kufanya mtihani

wa taifa aliendeleza tabia yake mbaya ya kunakili katika mitihani kiasi kwamba alikamatwa na kupelekwa kwenye kituo cha polisi, akatiwa gerezani. Walimu na wanafunzi wenzake walipomuona katika hali hiyo walikumbuka mawaidha aliyopewa, yeye akayapuuza, wakasikitika sana na kusema, "Asiyesikia la mkuu huvunjika guu." Baada ya muda mfupi, Mukuzo aliachiliwa huru kutoka gerezani na kuwakuta wanafunzi wenzake tayari wameishapata ajira nzuri; wengine wakisoma katika vyuo vikuu. Mara hii Mukuzo alianza kujutia makosa yake kwa kusema, "Majuto yangalikuwa mazuri kama yasingalikuwa mjukuu."

**Maswali:**

1. Ni tabia zipi alizokuwa nazo Mukuzo?
2. Mukuzo alikuwa akitumia mbinu gani ili aweze kushinda mitihani?
3. Je, alifanikiwa kutokana na mbinu hizo? Eleza.
4. Nini maana ya "Majuto yangalikuwa mazuri kama yasingalikuwa mjukuu?" Husisha msemo huu na kifungu ulichokisoma.
5. Eleza maana ya methali, "Asiyeskia la mkuu huvunjika guu."
6. Je, unakubaliana na tabia za Mukuzo? Eleza jibu lako.

## 8.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 6


**Soma tena insha ya wasifu katika kazi ya 5 ya hapo juu, kisha utoe muhtasari wake mbele ya darasa.**

## 8.6. Kuandika

### KAZI YA 7

**Tunga insha ya wasifu kuhusu mtu, kitu au jambo fulani.**

## SOMO LA 9: MATUMIZI YA ALAMA ZA VITUO




### KAZI YA 1

**Angalia mchoro hapo juu na kueleza yale unayoyaona.**

### 9.1. Kusoma na ufahamu: Nchi ya Rwanda

**Soma kifungu cha habari kisha ujibu maswali ya ufahamu**

Rwanda ni nchi nzuri iliyo katikati ya bara la Afrika. Imepakana na Uganda kwa upande wa Kaskazini, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa upande wa Magharibi, Burundi kwa upande wa Kusini na Tanzania kwa upande wa Mashariki. Mji mkuu wa Rwanda ni Kigali. Mji huu umesifika kwa usafi usio na kifani. Miji mingine ambayo huwapendeza wengi wanaoitembelea ni Huye, Muhanga, Musanze, Rubavu, Nyagatare na Rusizi.

Rwanda ni nchi ya milima na mabonde yake mapana yenye rutuba tele. Milima yake mikubwa ni Karisimbi, Muhabura, Sabyinyo, Gahinga na Bisoke.

Mlima wa Muhabura ndio wenye sifa kubwa kwa sababu huwavutia watu wengi sana hasa watalii. Rwanda ina mito na maziwa mengi. Mifano ya mito ni kama vile Akanyaru, Nyabarongo, Rusizi, Akagera, Mukungwa, nk. Mto wa Akagera ndio mkubwa kuliko yote na una maporomoko huko Rusumo. Maziwa yanayopatikana nchini nayo ni mengi : Cyohoha, Rweru, Muhazi, Mugesera, Burera, Ruhondo, Rwehikama, Rwanyakizinga, n.k. Ziwa Kivu ndilo kubwa kuliko maziwa mengine. Ziwa hili linapatikana sehemu za Magharibi ambapo maeneo yake hufikia wilaya ya Rubavu, Karongi, Rutsiro, Nyamasheke na Rusizi. Ziwa Kivu linatenga nchi ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Nchi ya Rwanda ina hali ya hewa iliyo nzuri sana ; si joto wala si baridi kwa wakati wote wa mwaka. Rwanda ina misimu miwili ya mvua. Mvua za vuli huanza mwezi wa Septemba hadi mwezi wa Novemba. Msimu wa masika ni wakati mvua hunyesha kwa mfululizo kuanzia mwezi wa Machi hadi Mei. Kuna misimu miwili ya jua. Kiangazi ni majira ya mwaka ambapo jua huwa kali sana baina ya mwezi wa Juni na Agosti. Kipupwe ni msimu ambapo jua huwa kiasi na hutokea kuanzia mwezi wa Desemba hadi mwezi wa Februari.

Nchi ya Rwanda ina mbuga za wanyama zinazovutia sana. Kuna mbuga ya wanyama ya Akagera ambayo ndiyo kubwa na yenye wanyama wa aina tofauti. Nyati, simba, chui, fisi, tembo, twiga, kiboko na wengine, wote hupatikana katika mbuga hii. Kuna pia mbuga ya wanyama ya Volkano ambayo inajulikana sana kwa sokwe-mtu wanaovutia watalii wengi kutoka sehemu zote duniani. Aidha, mbugani humu mnapatikana wanyama wengine wengi. Mbuga nyingine ni mbuga ya wanyama ya Nyungwe ambayo inahifadhi aina mbalimbali za ndege na wanyama kama vile masokwe, manyani, tumbiri au ngedere, choroa, kima, vipepeo wa aina tofauti, n.k.

Wananchi wa Rwanda ni Wanyarwanda. Wao wanalima mazao ya biashara kama vile kahawa, chai na pareto. Mazao ya chakula ambayo hulimwa sehemu nyingi za nchi ni maharage, viazi mviringo, viazi vitamu, ndizi, mihogo, mtama, mahindi, mpunga na kadhalika. Wanyarwanda hupenda kufuga sana ng'ombe, mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura, kuku na bata.

Rwanda ni nchi inayovutia watalii wengi kwa uzuri wa mbuga zake, mito, maziwa na hali ya hewa. Wageni wote wanaoitembelea nchi ya Rwanda huisifu kwa huduma nzuri wanayopewa, usafi na utunzaji wa mazingira usiopatikana mahali kwingi duniani.

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Kifungu cha habari ulichosoma ni aina gani ya mtungo?
2. Taja nchi zinazopakana na Rwanda kwa kila upande wake?
3. Ziwa kubwa nchini Rwanda ni lipi? Linapatikana wapi?
4. Taja mazao mawili ya biashara na mazao matatu ya chakula.
5. Andika majina matatu ya mbuga za wanyama zinazopatikana nchini Rwanda.
6. Kwa nini Rwanda inavutia watalii?

## 9.2. Matumizi ya msamiati kutoka kifungu cha habari

## KAZI YA 3

**Tumia maneno yanayofuata ili kujaza mapengo katika sentensi zifuatazo: pareto, mbuga za wanyama, huwavutia, hali ya hewa, misimu.**

1. Wanyarwanda hupanda mazao mengi sana katika ................ wa mvua za kutosha.
2. Nchi Rwanda imesifika kwa …………….. nzuri ambayo huwapendeza wageni wengi wanaoitembelea.
3. ................... ni miongoni mwa mazao ya biashara yanayopatikana nchini Rwanda.
4. …………… …… ni mojawapo ya vivutio vya utalii vinavyoleta pesa nyingi za kigeni.
5. Kaskazini mwa Rwanda kuna masokwe ambao .................. watalii wengi sana.

## 9.3. Sarufi kuhusu matumizi ya alama za vituo/uakifishaji

### KAZI YA 4

**Eleza aina za alama za vituo zilizotumiwa katika sentensi zifuatazo:**

1. Ehee! Kumbe yeye ni mwizi!
2. Mwalimu wa Mitaala wa shule yetu ni mtu mpole kabisa.
3. Ninaenda sokoni kununua vitu vingi: maembe, mapapai, machungwa, madaftari, kalamu na kuku.
4. Nyinyi mnaona vipi siku za leo?
5. Masomo haya si ya kukuangamiza; masomo haya ni ya kuboresha hali ya maisha yako.

### ALAMA ZA UANDISHI /ALAMA ZA UAKIFISHAJI NA MATUMIZI YAKE

Kuandika ni tofauti na kuzungumza. Katika maandishi, uakifishaji ni muhimu sana kwani ndio unaotusaidia kusoma yaliyoandikwa. Bila matumizi ya alama za vituo au alama za uandishi msomaji angepata taabu kwa kusoma na kupata ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Zifuatazo ni alama zinazotumiwa katika maandishi na matumizi yake.

1. **Nukta (.):** Nukta au kituo kikuu hutumika kama ifuatavyo:
   - **Kuonyesha mwisho wa sentensi**

     **Kwa mfano:** Mtoto amelala.

     Aliniponya kwa kuwa alipendezwa nami.
   - **Katika kufupisha maneno**

     **Kwa  mfano:** S.L.P.

     Dkt. Mukeshimana
   - **Kuonyesha Saa**

     **Kwa mfano:** Sasa ni saa 8.00
   - **Katika hesabu kuonyesha desimali**

     **Kwa mfano:** Nimepata alama 40.5
2. **Mkato/ koma (,):** Mkato au koma hutumika kama ifuatavyo:
   - **Kuonyesha orodha ya vitu**

     **Kwa mfano:** Usisahau kununua mkate, soda, kitumbua, na chapati.

- **Kugawanya mawazo katika sentensi**

  **Kwa mfano:** Baada ya kusikiliza kesi yake, hakimu alimhukumu kifungo cha miaka 10 jela.

3. **Alama ya mtajo/ kinukuu/ vinukuu (‘) na (“):** Alama za mtajo hutumika kwa:

- **Kunukuu usemi halisi**

  **Kwa mfano:** “Ukiniletea zawadi nitakupenda sana,” Mugenga alimwambia Ndayizigiye.

- **Kuonyesha maneno yasiyo ya Kiswahili unapochanganya lugha katika sentensi**

  **Kwa mfano:** Huyu ndiye mchezaji “number one.”

4. **Alama ya kuuliza/ kiulizi/ ulizo (?):** Kiulizi hutumika:

- **Kuulizia swali**

  **Kwa mfano:** Ulikuwa wapi muda wote huo?

5. **Alama ya hisi/ mshangao (!):** Matumizi ya alama ya hisi ni:

- **Kuonyesha hisia k.v mshangao, hasira, furaha, n.k.**

  **Kwa mfano:** Hoyeeeee!
  Haiwezekani!

- **Kuigiza tanakali za Sauti**

  **Kwa mfano:** Maji yalimwagika mwaaaa!

6. **Nukta-mkato/semi-koloni (;):** Nukta-mkato hutumika:

- **Kuorodhesha vitu au mawazo hasa ikiwa yana maneno zaidi ya moja**

  **Kwa mfano:** Maria alinituma nimpelekee kitabu cha kufundishia Kiswahili kwa Wageni; madaftari mawili makubwa; baiskeli ndogo za watoto na vikombe vinne.

- **Kuunganisha vishazi huru viwili**

  **Kwa mfano:** Tuliandamana kwa moyo wa kizalendo; tukapata haki yetu.

7. **Nuktambili/ nukta pacha/ koloni (:):** Nuktambili hutumika:

- **Kuonyesha mwanzo wa orodha**

  **Kwa mfano:** Ukifika sokoni nunua vitu vifuatavyo: maembe mawili, kilo moja ya sukari, kilo sita za unga wa ngano, kilo moja ya vitunguu, lita kumi za mafuta ya kupikia na mfuko mmoja wa unga wa mahindi.

- **Kunukuu ukurasa wa Biblia**

  **Kwa mfano:** Yohana kutoka 20:4 Biblia inasema….

- **Kuonyesha msemaji katika tamthilia au mchezo wa kuigiza**

  **Kwa mfano:** Mkulima: Nyinyi walanguzi mnatukandamiza sana!

  Mlanguzi: Viwanda hakuna, sasa unadhani sisi tutauza kwa faranga ngapi?

  Hatuwakandamizi bali ni mabadiliko madogo tu yaliyojitokeza katika biashara ya leo.

8. **Matumizi ya kistari kifupi (-):** Kistari kifupi hutumika:

- **Kuunganisha maneno mawili**

  **Kwa mfano:** Mfa-maji

  Mwana-harakati

- **Kuonyesha hadi, au mpaka**

  Kwa mfano: Umeme umepanda kutoka elfu 20 – 60 kwa mwezi.

9. **Alama za Mabano/ parandesi ( ):** Mabano hutumika:

- **Kutoa maelezo zaidi**

  **Kwa mfano:** Wanafunzi wote (wasichana na wavulana) wanaweza kujua Kiswahili.

- **Kufungia herufi za kuorodheshwa**

  **Kwa mfano:** (a) huelimisha (b) huburudisha (c) huonya

10. **Mkwaju (/):** Mkwaju hutumika :

- **Kuonyesha kuwa mojawapo ya vitu vilivyotajwa chaweza kutumiwa badala ya vingine.**

  **Kwa mfano:** Uwayo alikaa kimya/ alitulia.

## 9.4. Matumizi ya lugha

### KAZI YA 5

**Weka alama za vituo katika dondoo ya insha ya wasifu inayofuata.**

Hmm Unataka nikuambie sifa za mtu ninayempenda Bila shaka ninampenda sana baba Baba yangu anaitwa John Mugabo Yeye ni mrefu na mweupe Baba ana macho mazuri na nywele nyingi nyeusi kichwani Yeye hupenda kuvaa mavazi tofauti suti mashati meupe na suruali nyeusi kila wakati isipokuwa Jumamosi tunapoenda kucheza kandanda naye Baba ni mchezaji hodari sana katika kandanda yeye hufurahia sana mchezo huu.

Baba yangu ni mwalimu mkuu katika shule ya sekondari ya Kigali Anaheshimiwa sana na walimu wote, wanafunzi hata na wazazi Sifa zake nzuri ndizo humfanya baba apendwe na kila mtu.

## 9.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 6

**Tunga kifungu cha habari ambamo alama za uakifishaji zifuatazo zimetumika, kisha wasomee wenzako kifungu chenyewe kwa kuheshimu matumizi ya alama hizo:**

*alama ya kushangaa, alama ya nukta (kituo), mkato wa chini (koma), alama ya kuuliza (kiulizi), alama ya nukta mbili, alama za mtajo, alama ya nukta na mkato, alama ya kistari kifupi, alama za mabano na alama ya mkato.*

## 9.6. Kuandika

### KAZI YA 7

Tunga insha ya wasifu kuhusu mada unayojichagulia kwa kutumia alama za uakifishaji ulizojifunza.

## TATHMINI YA MADA YA NNE

1. Nini maana ya insha za wasifu?
2. Sehemu za insha ya wasifu ni zipi?
3. Taja sifa tano za insha ya wasifu.
4. Tunga sentensi sahihi tano ambazo zina kiambishi simulizi ***"-ka-"***
5. Weka alama za vituo katika sentensi zifuatazo:
   a. Afanalek Kumbe nimesahau kuwa leo ni siku yangu ya kuzaliwa
   b. Wanafunzi wa kidato cha tano wanakosa miaka mingapi kumalizia shule za upili
   c. Niletee kwenye ofisi yangu vyombo vifuatavyo kalamu karatasi meza viti deski na makabati
   d. Mwalimu alisema Fanyeni kazi hii katika dakika arubaini tu
   e. Watu wote wanaume na wanawake watashiriki katika mkutano wa kijiji chetu
6. Katika ukurasa mmoja, tunga insha ya wasifu yenye matumizi sahihi ya alama za vituo kuhusu shule yako.

# MADA 5

# HOTUBA

**Uwezo mahususi wa mada**
Kuandaa hotuba na kuisimulia hadharani

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutoa maana ya hotuba
- Kuonyesha tofauti iliyopo kati ya hotuba na insha za masimulizi au insha za maelezo
- Kutaja sehemu kuu za hotuba
- Kubainisha mwongozo wa kutunga hotuba
- Kueleza matumizi ya alama za vituo

## KIDOKEZO

**Tazama mchoro ufuatao kisha ujibu maswali yaliyopo hapo chini yake.**



**Maswali**

1. Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro hapo juu
2. Wahusika hawa wanafanya nini?
3. Ni vifaa gani unavyoona kwenye mchoro huu?

# SOMO LA 10. MAANA YA HOTUBA

## 10.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Meya baada ya kazi za Umuganda

**Soma hotuba ya Meya baada ya shughuli za Umuganda, kisha jibu maswali uliyopewa hapo chini:**

Mheshimiwa mgeni rasmi mkuu wa mkoa, Mheshimiwa mkuu wa kikosi cha askari jeshi wa wilaya yetu, Mheshimiwa bibi mkuu wa askari polisi wa wilaya yetu, Mheshimiwa katibu mtendaji wa wilaya yetu, na mabwana na mabibi mliokusanyika hapa leo, Hamjambo? Ninachukua fursa hii kuwakaribisha hapa katika wilaya yetu. Ninapenda kumshukuru mgeni rasmi kwa kuja kujiunga nasi leo kwa lengo la kushiriki pamoja nasi katika kazi za umuganda mwishoni mwa mwezi huu ili tuweze kujitengenezea barabara hii.

Mgeni wetu mheshimiwa, kazi hizi za umuganda zinatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa taifa letu na nguvu za kila mtu zinahitajika kwa ujenzi wa maendeleo ya nchi yetu. Mfano wa karibu, leo tumemaliza kujitengenezea barabara itakayotuunganisha na majirani zetu kutoka wilaya nyigine. Barabara hii bila shaka itatusaidia katika kurahisisha kazi ya ufanyajibiashara, utalii, kurahisisha uchukuzi wa wagonjwa mahututi kutoka zahanati kwenda hospitali. Aidha, hata matembezi nayo yatakuwa rahisi kwa kila mtu. Zaidi ya hivyo, usafi utaongezeka, na usalama barabarani utaweza kuimarishwa kwa kujiepusha na ajali zisizokuwa za lazima.

Mheshimiwa mgeni rasmi, haya yote yameweza kufanikiwa tu kutokana na ushirikiano miongoni mwetu. Ushirikiano huu umefanikisha maendeleo ya watu binafsi na hata ya nchi nzima. Bila ya kufanya kazi kama hizi, maendeleo hurudi nyuma. Shughuli za umuganda ni wajibu wa kila mwananchi anayependa nchi yake na maendeleo ya jamii nzima. Kumbukeni kuwa hakuna mtu mwingine atakayetujengea taifa letu. "Taifa letu litajengwa na sisi wenyewe, ni sisi tutakaojijengea taifa letu." Ni lazima sisi sote tujiunge pamoja ili tuweze kufanikiwa kuokoa fedha nyingi zinazoweza kutumiwa katika shughuli nyingine za kimaendeleo kama vile kuleta huduma za afya, kulipia mishahara ya watumishi, kuleta maji safi na salama na umeme.

Isitoshe, shughuli hizi za umuganda husaidia katika upandaji wa miti kwa kuzuia mmomonyoko wa ardhi, kuwajengea nyumba watu wasiojiweza, kujenga shule, hospitali, masoko na madaraja kwenye mito. Kama wahenga wasemavyo "Umoja ni nguvu na pia kidole kimoja hakivunji chawa". Tushirikiane sote ili tuzidi kuiendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa mgeni rasmi, mheshimiwa mkuu wa kikosi cha askari jeshi, mheshimiwa bibi mkuu wa askari polisi, mheshimiwa katibu wa wilaya yetu, na wananchi wapendwa, mabibi na mabwana ; ni vyema tuelewe kwamba mtaka cha uvunguni sharti ainame, na wahenga wengine walisema, «ukiona vyaelea vimeundwa». Ni vizuri sote tuelewe kuwa kila mwananchi hana budi kutoa mchango wake katika kulijenga taifa letu kwa kushiriki katika shughuli kama hizi za umuganda ambazo hufanyika kila mwisho wa mwezi. Tulinde miundombinu iliyojengwa, kwani ni kielelezo kizuri cha nguvu zetu na ushirikiano wetu. Bila shaka tutaweza kuimarisha maendeleo ya nchi yetu na maisha yetu yatakuwa mazuri zaidi.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza kwa makini, asanteni.

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Kwa kutumia sentensi moja, eleza jambo linalozungumziwa katika kifungu ulichosoma.
2. Ni watu gani wanaozungumziwa katika hotuba hii?
3. Eleza umuhimu wa kazi za umuganda katika ujenzi wa nchi.
4. Ni nani mgeni rasmi katika hotuba hii?
5. Taja shughuli zinazofanywa na watu wanaoshiriki katika kazi za umuganda.
6. Kufanya kazi za «Umuganda» kunamaanisha nini kwa mwananchi?
7. Baada ya kusoma hotuba hii, umepata fundisho gani?
8. Eleza umuhimu wa barabara kwa wananchi.
9. Wananchi wanahimizwa kufanya nini ili waweze kuimarisha maendeleo na kuboresha maisha yao?

## 10.2. Msamiati kuhusu hotuba ya Meya

## KAZI YA 2

**Husisha maneno kutoka sehemu A na maana zake kutoka sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1.Mheshimiwa | a) Neno la heshima linalotamkwa kabla ya kutaja jina la mtu maarufu. |
| 2. Wilaya | b) Sehemu ndogo katika jimbo au mkoa. |
| 3. Taifa | c) Jamii ya watu wanaoishi katika nchi moja na wanaounganika kutokana na matukio ya kihistoria. |
| 4. Barabara | d) Tukio lenye madhara linalotokea ghafla. |
| 5. Utalii | e) Korongo lenye maji yanayotiririka wakati wote. |
| 6. Ajali | f) Enye kushikwa na ugonjwa sana. |
| 7. Nyasi | g) Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |
| 8. Mto | h) Mmea pori wenye majani madogo madogo ya kijani unaoliwa na ng'ombe. |
| 9. Mgeni | i) Mtu ambaye si mwenyeji wa mahali fulani. |
| 10. Mahututi | j) Njia ipitayo magari na binadamu. |

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi zenye maana kamili kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Kazi za "Umuganda"
2. Askari
3. Askari polisi
4. Kukaribisha
5. aliwashukuru
6. tutajenga
7. bidii

## KAZI YA 4

**Jaza sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno uliyopewa:** mikoa, katibu mtendaji, ilitengenezwa, ujenzi wa taifa, rahisi, kazi, kupanda miti, kukata nyasi, mmomonyoko wa ardhi, asanteni.

1. Kusini ni mojawapo ya ………………………. ya Rwanda.

2. ……………………….. ndiye anayeongoza tarafa.
3. Barabara hii …………………….. vizuri.
4. Ushirikiano wetu unahitajika kwa ……………………………….. letu.
5. Itakuwa ………………………….. kujijengea taifa kila mtu akifanya kazi kwa bidii.
6. …………………….. ni mojawapo ya kazi za kulinda mazingira.
7. Tunapaswa ……………………………….karibu na makazi yetu ili tujikinge na ugonjwa wa malaria.
8. Katika majira ya mvua, tufanye iwezekanavyo ili tuzuie ………………………….
9. …………….. sana kwa kunisikiliza kwa makini.
10. ……………………….. ndiyo msingi wa maendeleo.

## 10.3. Sarufi: Alama za uandishi na matumizi yake

### Maelezo muhimu

- Ili maanadishi yaweze kusomeka na kueleweka vizuri ni muhimu sana kuzingatia uakifishaji (matumizi ya alama za vituo).

### KAZI YA 5

**Tunga sentensi moja kwa kutumia alama zifuatazo:**

1. Nukta
2. Alama ya kuuliza (kiulizi)
3. Alama ya hisi (mshangao)
4. Nuktambili
5. Mkato

### KAZI YA 6

**Tumia alama za vituo zinazofaa katika sentensi zifuatazo:**

1. Jina lako ni nani
2. Alinunua kalamu kitabu daftari viatu na soksi
3. Aisee ni wewe
4. Nami nimekubali kuwa mvua imenyesha asubuhi hii
5. Nawa mikono kabla ya kula

6. Wanyarwanda hufuga wanyama wafuatao mbuzi Kondoo Nguruwe Ng'ombe Sungura na kuku
7. Yeye alizaliwa tarehe 10 10 2010

## 10.4. Matumizi ya lugha: Mambo muhimu katika hotuba

### KAZI YA 7

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa hapo chini .**

**Mambo ya kuzingatia katika hotuba:**

Hotuba ni maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele ya kundi la watu. Hotuba inaweza kutolewa kwa madhumuni ya kutaka kuhimiza watu kufanya kazi, kufanya kampeni fulani, kutoa taarifa fulani kwa watu. Kwa hiyo, hotuba huwa ni za aina tofauti:

a. **Mahubiri**: Ni hotuba za mafundisho ya kidini, zinazotolewa makanisani, misikitini, n.k.
b. **Hotuba za kisiasa**: Ni hotuba zihusuzo taarifa ya serikali kama vile kuwahimiza watu kutenda jambo fulani na kuwahimiza kushiriki katika shughuli zilizopo za ujenzi wa taifa, n.k.
c. **Mihadhara**: Ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni anapofundisha kundi la wanafunzi na hasa wanafunzi wa vyuo vikuu.

- **Hotuba nzuri huwa na sifa za hotuba:**
  - Ukweli wa habari na taarifa
  - Kujua vizuri aina ya watu unaowatolea hotuba, umri wao, kazi zao, n.k.
  - Ufasaha wa lugha ili iweze kupendeza na kueleweka vizuri
  - Nidhamu au adabu ya mzungumzaji mwenyewe asimamapo mbele ya watu
  - Mantiki nzuri au mfuatano mzuri wa mawazo
  - Sauti ya kusikika vizuri
  - Kuvaa vizuri.

**Maswali**

1. Eleza maana ya hotuba
2. Hotuba hutolewa kwa lengo gani?

3. Eleza aina za hotuba
4. Eleza sifa muhimu za hotuba

### 10.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**KAZI YA 8**

**Jadili kuhusu "Umuhimu wa hotuba."**

### 10.6. Kuandika: Utungaji wa hotuba

**KAZI YA 9**

**Wewe ni kiranja mkuu wa wanafunzi katika shule yako. Tunga hotuba kwa ajili ya kufunga mwaka wa shule.**

## SOMO LA 11: MUUNDO WA HOTUBA

**KAZI YA 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

a. Unaelewa nini kuhusu neno hotuba?
b. Ni hotuba gani uliyoisikiliza ikakufurahisha?

### 11.1. Kusoma na ufahamu: Hotuba ya Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano

Soma hotuba ya Mkuu wa Kamisheni ya Umoja na Maridhiano wakati wa kuanzisha Utaratibu wa "Ndi Umunyarwanda"

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,

Waheshimiwa wengine katika ngazi tofauti, Mabibi na Mabwana, Hamjambo nyote! Ninayo furaha kubwa ya kuwakaribisha hapa kwenye Uwanja wa Amahoro. Watu wote walionitangulia walizungumzia mambo mengi kuhusu umoja wetu kama wananchi wenye utamaduni mmoja na mitazamo sawa ya kujiendeleza na kujitegemea. Kwa kuwa umoja wetu kama Wanyarwanda ndio nguvu na nguzo ya maisha yetu, tumekutana hapa leo hii ili tuweze kuanzisha rasmi utaratibu muhimu wa "Ndi Umunyarwanda".

Waheshimiwa mlioshiriki katika tendo hili maalumu la “Ndi Umunyarwanda”, ningependa kuwakumbusha kwanza kuwa nchi yetu iliteseka miaka mingi kutokana na ubaguzi ambao uliharibu watu na vitu vyao pamoja na mali ya nchi. Hotuba za ubaguzi zilitungwa mara nyingi na mwishowe zilisababisha ukimbizi na vifo vya Wanyarwanda wengi. Mauaji ya Kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994 yalikuwa kilele cha ubaguzi huo. Idadi ya watu zaidi ya milioni moja waliuawa na wananchi wenzao kwa uchungu unaopita kiasi. Baadaye, nchi ilikuwa na matatizo mengi.

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, Waheshimiwa wengine katika ngazi tofauti, Mabibi na Mabwana!

Wahenga walisema, “Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.” Hivyo basi, Serikali ya Rwanda iliamua kujengea nchi yetu kwenye msingi wa umoja na maridhiano na hivi sasa imefanikiwa. Utaratibu wa Ndi Umunyarwanda tunaouzungumzia leo, unahusu uimarishaji wa umoja wa Wanyarwanda ambao unatuwezesha kuwa na umoja na mshikamano katika namna endelevu. Katika utaratibu huu, kila mwananchi atajitambulisha kwanza kama Mnyarwanda kuliko kujitambulisha kwa utambulisho mwingine wowote. Hivi ni kusema kwamba kama mtu mmoja, ni lazima sisi sote tuwe na mshikamano, ushirikiano na mwelekeo mmoja kwa kufuatilia amani, usalama na maendeleo.

Malengo ya Ndi Umunyarwanda ni kuwapa Wanyarwanda fursa ya kufikiria Unyarwanda yaani uhusiano wao, utamaduni wa kupenda nchi yao, kuilinda nchi na kuiendeleza kwenye viwango vya juu kadiri iwezekanavyo. Vilevile, kila Mnyarwanda anatarajiwa: kulinda usalama, kuwasaidia watu ambao hawajiwezi kama vile watoto yatima, wazee, walemavu na maskini. Hili linafanikishwa kwa kuhakikisha makundi haya yote yanapata huduma ya shule, afya, chakula, na kuwapatia makazi.

Mheshimiwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Mkuu wa Mkoa, Waheshimiwa wengine katika ngazi zinazohusika, Mabibi na Mabwana,

Kila Mnyarwanda anapaswa kuzingatia uhusiano wetu kama wananchi kwa kuendeleza umoja wetu, kupenda, kuilinda na kuiendeleza nchi, na kujiepusha na ubaguzi wowote ili tuwe na amani ya kudumu. Ninamalizia kwa kuwashukuru nyote. Asanteni sana kwa kushiriki.

## KAZI YA 2

**Maswali ya Ufahamu**

1. Nani aliyekuwa mgeni wa heshima?
2. Mkutano ambamo kulitolewa hotuba hii ulifanyikia wapi?

3. Taja vyeo vya waheshimiwa waliokuwepo katika mkutano huo.
4. Maneno "Wanyarwanda ni kama mtu mmoja" yanamaanisha nini katika kifungu cha habari?
5. Kwa nini Serikali ya Rwanda iliamua kujengea nchi kwenye msingi wa umoja na maridhiano?
6. Kulingana na historia ya Rwanda, kwa nini ubaguzi ni jambo baya sana?
7. "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu." Husisha methali hii na kifungu ulichosoma.
8. Utaratibu wa "Ndi Umunyarwanda" una malengo gani?
9. Taja mambo muhimu matatu ya kimaendeleo ambayo hufanywa katika utaratibu wa "Ndi Umunyarwanda."
10. Kwa ufupi, utaratibu wa "Ndi Umunyarwanda" unahusu nini?

## 11.2. Msamiati kuhusu hotuba

### KAZI YA 3

**Jaza sentensi ambazo zinafuata kwa kutumia maneno haya:** usalama, kuimarisha, mwelekeo, anatarajiwa, huduma, udhaifu, maridhiano, mauaji ya kimbari, hotuba, malengo.

1. Nitatunga……. nzuri siku ya kuanzisha rasmi Shirika la Umoja na Maridhiano shuleni kwetu.
2. Tunapaswa kutoa ………… nzuri kwa watu wote wanaoizuru nchi yetu ili kudhibiti utamaduni wa Wanyarwanda.
3. Wanajeshi, askari polisi pamoja na watu wengine wanatarajiwa kuungana mkono kwa kulinda ……………..
4. "Ndi Umunyarwanda" ni utaratibu wa kutilia nguvu umoja na ………… miongoni mwa Wanyarwanda wote.
5. Watu zaidi ya milioni moja waliuawa katika ……… dhidi ya Watutsi.
6. Kutokana na ………… ya "Ndi Umunyarwanda," Rwanda imeweza kujijengea msingi imara wa maendeleo ya taifa.
7. Wahenga walisema vizuri, «Umoja ni nguvu, utengano ni ……….».
8. Kila Mnyarwanda ……….. kuwa raia mwema kwa kuitikia shughuli za kuendeleza taifa lake.
9. Wanyarwanda wote wana …………. mmoja wa kujenga na kuendeleza nchi yao.
10. Wanyarwanda hufanya shughuli mbalimbali ili waweze ………… uchumi wa taifa lao.

## KAZI YA 4

**Husisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B**

| A. Neno | B. Maana ya neno |
|---|---|
| 1.Hotuba | a.Hali ya kuwa pamoja, ushirikiano |
| 2.Umoja | b.Neno linalotamkwa kabla ya kutaja jina la mtu maarufu |
| 3.Maridhiano | c.Namna maalumu ya kutekeleza jambo |
| 4.Mheshimiwa | d.Kusema maneno au kuonyesha ishara ya kufurahia jambo la wema unalofanyiwa, kutoa shukrani |
| 5.Utaratibu | e.Kuanzisha jambo au kitu kwa kufuata utaratibu au kanuni zilizowekwa |
| 6.Kushukuru | f.Mahali ambapo kesi na mashtaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa, korti au baraza |
| 7.Kuanzisha rasmi | g.Makubaliano yanayofikiwa baina ya mataifa au makundi yaliyokuwa yanapingana na kutofautiana kiitikadi, maafikiano |
| 8.Mahakama | h.Hali ya kuwa na maadili au mwenendo mwema kulingana na utamaduni, mila na desturi za Wanyarwanda |
| 9.Unyarwanda | i.Mfumo wa kijamii wa kutoa huduma kwa upendeleo kwa misingi ya rangi, jinsia, kabila, n.k. |
| 10.Ubaguzi | j.Maelezo maalumu yanayotolewa na mtu mmoja mbele za watu |

## 11.3. Sarufi: Alama za uandishi na matumizi yake

## KAZI YA 5

**Tia alama za vituo mwafaka katika aya hii.**

Ngozi za baadhi ya wanyama hawa wachinjwapo hufaa sana kwa matumizi mbalimbali ngozi hufaa sana kwa kutengeneza viatu kanda mikoba mipira nk kinyesi cha wanyama hawa ni muhimu kwa kurutubisha mashamba ili yaweze kuotesha mimea mingi afisa wa kilimo aliwaambia raia

## 11.4. Matumizi ya lugha: Sifa za hotuba

### KAZI YA 6

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali hapo chini.**

**Muundo wa hotuba**

Hotuba ina sehemu zifuatazo:

1. **Anwani**: Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua mada ya hotuba. Hiki ndicho kichwa chake hotuba.

   **Mfano:** Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Rwanda kwenye Sikukuu ya Mashujaa.

2. **Utangulizi**: Mazungumzo katika utangulizi yanatoa mwanga ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano. Wataje kwa majina au vyeo vyao kuanzia kwa yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana. Kumbuka kwamba huhitaji kuwasalimia kwa majina yao. Kuwatambua kwa vyeo vyao vya pekee kunatosha.

   **Mfano:** Waziri wa Elimu, Gavana wa Jimbo la Kusini, Mkuu wa Wilaya ya Nyanza, Wanachama wa kikundi hiki cha Elimu Bora, mabibi na mabwana. Ni matumaini yangu kwamba nyote mna afya nzuri.

3. **Mwili/Kiini**: Hakikisha kuwa kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho. Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisi wala si wa taarifa. Panga mawazo kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo muhimu lazima lianze kuzungumziwa kwa ukamilifu halafu lifuatiwe na mawazo mengine, nayo kwa kikamilifu.

4. **Mwisho**: Hapa mazungumzo yajumlishe mawazo yote yaliyozungumziwa kwa maelezo fasaha. Ni vizuri kwa hotuba kufungwa kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari ibaki katika mawazo ya wasikilizaji.

**Sifa za hotuba**

**Hotuba huzingatia mambo haya:**

a. **Ukweli wa habari na taarifa:** Ni lazima mhutubi ahakikishe kuwa yale anayozungumzia yana uhusiano na ukweli.

b. **Ufasaha wa lugha:** lazima mhutubi kutumia lugha fasaha, nzuri, safi na yenye kusikika vizuri kwa kila msikilizaji. Si vizuri kutumia lugha ya mafumbo.

c. **Mantiki nzuri:** Ni lazima kuweka kwa mfuatano mzuri wa mawazo au fikra.
d. **Nidhamu:** Ni jambo muhimu mzungumzaji mwenyewe kuwa na adabu njema asimamapo mbele ya watu.
e. **Sauti ya kusikia wazi pamoja na ishara zinazoeleweka na zinazohusiana na yasemwayo.** Ishara hizo si za lazima iwapo hotuba inatolewa kwa njia ya redio.

**Maswali**

1. Hotuba inatarajiwa kuwa na sehemu zipi?
2. Katika kuanza hotuba yake, mhutubi hufanya nini?
3. Habari yenyewe hutolewa katika sehemu gani? Kwa nini?
4. Mwisho wa hotuba una maumbile gani?
5. Taja sifa tatu ambazo hotuba nzuri huzingatia.

## 11.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

### KAZI YA 7

**Kwa kushirikiana na wenzako, jadili mada zifuatazo:**

1. Hotuba inaweza kuharibu na kujenga taifa.
2. Wanyarwanda ni kama mtu mmoja.

## 11.6. Kuandika: Kuandika maelezo mafupi

### KAZI YA 8

**Soma hotuba iliyopo hapo juu na kuieleza kwa maneno machache. Tumia aya moja yenye mistari isiyozidi kumi.**

### TATHMINI YA MADA YA TANO

**Jibu maswali yafuatayo :**

1. Eleza angalau mambo matatu ya kuzingatia katika utoaji wa hotuba
2. Taja sehemu tatu za Hotuba na kuelezea sifa zake
3. Tunga hotuba inayohusu “Umuhimu wa mpango wa uzazi kwa familia”

# MADA 6

# UANDISHI WA RIPOTI

## Uwezo mahususi wa mada


Kutunga ripoti za mikutano kwa kuzingatia kanuni za utungaji

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya ripoti na umuhimu wake
- Kubainisha sehemu kuu za ripoti ya mkutano
- Kuonyesha sifa za ripoti ya mkutano
- Kubainisha aina mbalimbali za ripoti
- Kuorodhesha mbinu za kutunga ripoti ya mkutano
- Kutaja alama za vituo na matumizi yake sahihi

## KIDOKEZO

**Tazama mchoro hapo juu kisha jibu maswali yafuatayo:**



i. Watu unaowatazama kwenye mchoro huo wanafanya nini?

ii. Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

# SOMO LA 12: RIPOTI

## 12.1. Kusoma na ufahamu: Ripoti

**Soma kifungu kifuatacho kuhusu "Ripoti" kisha jibu maswali ya ufahamu**

Ripoti ni maelezo yanayotolewa kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea. Aidha, ripoti ni taarifa inayohusiana na shughuli au jambo fulani lililofanywa au kufanyika. Ripoti huandikwa kwa madhumuni ya kutoa taarifa ili iweze kufanyiwa kazi au kuhifadhiwa kama kumbukumbu. Ripoti huandikwa pia kwa madhumuni ya kuarifu watu kuhusu mabadiliko muhimu au maendeleo ya shughuli fulani. Vilevile, ripoti inaweza kuagiza utekelezaji fulani, kupendekeza kufanyika kwa jambo fulani na kupima au kutathmini utendajikazi fulani au maendeleo yaliyofikiwa.

Watu mbalimbali huweza kuandaa ripoti na kuiandika kulingana na majukumu yao ya kikazi. Kwa hiyo, baadhi ya ripoti huhitaji uchunguzi wa kiutafiti kuhusu jambo fulani ambapo tume fulani, ya polisi au ya kazi yoyote ile huweza kuundwa kwa ajili ya uchunguzi wao wa suala lililopo na ambalo linahitaji ufumbuzi kutegemeana na ripoti yao. Matokeo yanayoandikwa, uchunguzi unaofanywa na mapendekezo yanayotolewa huwa ni ripoti maalum ambazo hutokana na utafiti uliofanywa na tume iliyowekwa kwa ajili hiyo. Maendeleo yaliyofikiwa, maisha ya kawaida na utendaji kazi, matumizi ya fedha na mapato, haya yote hufanyiwa ripoti.

Muundo wa ripoti unategemea kwa kiasi kikubwa aina ya ripoti inayohusika. Lakini kimsingi, ripoti ni lazima iwe na mpangilio mzuri wenye mada zinazozungumziwa na labda hata mada ndogo ndogo zenye kuzingatia utaratibu wa nambari. Matumizi ya nambari husaidia kuipa ripoti mpangilio mzuri na wenye kueleweka kwa urahisi. Ripoti hazipaswi kuwa ndefu sana na zinapaswa kuwasilisha mambo muhimu kwa ufupi. Mwandishi wa ripoti hutumia mbinu za kufupisha lakini anahakikisha kuwa kila kitu kimezungumziwa. Ripoti hutumia sentensi fupi fupi zinazowasilisha mambo muhimu kwa uwazi. Ni vyema lugha inayotumiwa katika ripoti iteuliwe kwa uangalifu na isiwe na hisia au sifa ya kuathiri vibaya wanaoisoma.

Ripoti ina sehemu kuu nne ambazo ni kichwa, utangulizi, kiini na mwisho wa ripoti. Kila sehemu ina namna inavyoandikwa na mambo inayoyazingatia. Kichwa cha ripoti kinaandikwa kwa maelezo machache. Mambo muhimu yanayozingatiwa katika kichwa cha ripoti ni mahali tukio au jambo lilipofanyika, aina ya tukio au jambo lililofanyika, tarehe na muda wa tukio au jambo lililoshughulikiwa na ripoti hiyo. Baada ya kuandika kichwa cha ripoti, mwandishi anaandika utangulizi wa ripoti ambao unaonyesha lengo na madhumuni ya ripoti.

Katika kiini cha ripoti, mwandishi anaeleza kwa ufasaha mambo yaliyotokea, chanzo chake, ukubwa wake na madhara au faida yake. Mwisho wa ripoti huonyesha msimamo, mapendekezo na maoni ya mwandishi wa ripoti. Baadaye, ni lazima ripoti ionyeshe jina la mwandishi, cheo chake pamoja na terehe ripoti hiyo ilipoandikwa na iwekewe viambatisho vya kuthibitisha yaliyozungumziwa ikiwa vinahitajika.

Ingawa ripoti zina sehemu sawa, ukubwa na uzito wake unatofautiana kutokana na mambo na masuala yanayoripotiwa, madhumuni pamoja na aina ya ripoti. Ripoti ya polisi ni tofauti na ripoti ya daktari. Vilevile, ripoti ya tume ni tofauti na ile ya utafiti au ya kazi na kadhalika. Mwandishi wa ripoti anaweza kutoa ushahidi unaohusu suala au jambo fulani. Katika hali hii, mshahidi anasema kuwa alishiriki katika jambo hilo au anahakikisha kuwa aliona yaliyotokea.

Ripoti hutolewa kwa mkuu aliyeagiza uandishi wa ripoti hiyo na huhitaji umakini wa yule aliyepewa wajibu huo. Kwa hivyo, ni lazima anayepewa ripoti achunguze jambo kwa uangalifu ili aweze kutoa ufafanuzi mzuri wa jambo hilo kwani mapendekezo yake huathiri kwa kiwango kikubwa uamuzi unaochukuliwa kulihusu jambo hilo.

### KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Ripoti ni nini?
2. Madhumuni au malengo ya ripoti ni yapi?
3. Taja na kueleza aina za ripoti zilizozungumziwa katika kifungu hiki.
4. Utaratibu wa nambari unasaidia nini katika muundo wa ripoti?
5. Sentensi zinazotumiwa katika ripoti ni za aina gani?

## 12.2. Msamiati kuhusu ripoti

### KAZI YA 2

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo. Chunguza matumizi yake katika kifungu cha habari ulichosoma hapo juu kuhusu maana ya ripoti.**

1. Matokeo
2. Ripoti
3. Taarifa
4. Shughuli
5. Madhumuni

## KAZI YA 3

**Husisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1.Kumbukumbu | a. maelezo yanayoandikwa mwanzoni mwa kitabu ili kutoa kwa ufupi habari za mambo yanayozungumzwa humo |
| 2. Utekelezaji | b. kuweka mahali pa salama |
| 3. Kuhifadhi | c. tendo la kuona au maneno ya kuhakikisha kwa kueleza yaliyokuwa yakitendeka |
| 4. kutathmini | d. kitu au jambo linalofanya upate tena kufikiria juu ya kitu au jambo fulani. |
| 5. Mpangilio | e. hali ya kufanya jambo na kulitimiza kama ilivyokubaliwa |
| 6. Kufupisha | f. Ukataji shauri wa kufanya jambo fulani |
| 7. Utangulizi | g. hali ya kutokuwa epesi |
| 8. Uzito | h. kupunguza urefu |
| 9. Ushahidi | i. Kufanya uchunguzi na kisha kutoa maoni kuhusiana na yale yaliyobainika |
| 10.Uamuzi | j. mfuatano wa mambo kwa utaratibu unaoeleweka |

## 12.3. Sarufi: Alama za vituo na matumizi yake

## KAZI YA 4

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha bainisha majina ya alama zilizokolea.**

1. Jina lako ni nani **?**
2. Wewe ni mwanafunzi**.**
3. Yeye anafuga mbuzi**,** kondoo**,** kuku na ng’ombe**.**
4. Njoo hapa**!**

**Alama zilizokolea huitwa alama za vituo au alama za uafikishaji.**

### Maelezo muhimu kuhusu matumizi ya alama za vituo

Binadamu wanapozungumza, tunaweza kutambua jinsi wanavyopandisha sauti au kuishusha kwa ajili ya kutoa ujumbe fulani (kuuliza, kushangaa, kushtuka, n.k.). Vilevile, wanapomaliza usemi wao mtu huweza kutambua kuwa usemi umefikia kikomo kwa kusikia sauti zao tu. Lakini katika uandishi, hakuna sauti. Badala ya sauti, zipo alama za uandishi ambazo hutumiwa kuwakilisha sauti katika uandishi. Kutokana na alama hizo, tunatambua kama usemi umekwisha, kuulizwa swali, kushangaa na kadhalika. Pia, tunaposoma, tunajua wapi tunafaa kupumua kidogo, kushusha au kupandisha sauti na kadhalika.

Alama hizi huitwa pia **viakifishi.** Hivyo basi, viakifishi ni alama zinazotumiwa katika maandishi ili kuleta maana ikusudiwayo katika matini mbalimbali kama vile sentensi, aya, mtungo, barua, mialiko, matangazo, ilani na kadhalika.

**Mifano zaidi ya alama za vituo au viakifishi**

***Nukta (.)***

1. Huwekwa mwishoni mwa sentensi.

   **Kwa mfano:**

   i. Nimechoka**.**

   ii. Waziri mkuu wa Uchina amewasili mjini Kigali**.**

2. Hutumiwa kuonyesha ufupisho wa maneno.

   **Kwa mfano:**

   S.L.P. ( Sanduku la Posta )

3. Hutumika kubainisha saa na dakika au tarehe.

   **Kwa mfano:**

   i. 3.20: saa tisa na dakika ishirini

   ii. 14.5.2016: tarehe kumi na nne, mwezi wa tano, mwaka wa elfu mbili na kumina sita

***Kistari kifupi (-)***

a. Hutumiwa kuonyesha kuwa neno linakatwa kwa vile limefika ukingoni mwa mstari husika na bado linaendelea katika mstari unaofuatia.

b. Hutumiwa kuunga maneno yanayojenga neno moja. Mtindo huu aghalabu hujitokeza katika maneno yenye asili ya kigeni.

   **Kwa mfano :**

   i. Idd-el-Fitri

   ii. Dar-es-Salaam

4. Huweza kutumiwa badala ya koma.

   **Kwa mfano:** Nyimbo za asili-hasa Rumba-zinapendwa na wengi.

***Alama ya mshangao (!)***

Hutumiwa kuashiria mahangaiko ya moyo kama vile hasira, hofu, mshangao na kadhalika.

**Mifano:**

i. Lo! Mwanafunzi ameangusha kitabu cha mwalimu matopeni.
ii. Wamefungwa mabao kumi kwa nunge!

***Alama ya kuulizia/kiulizi (?)***

a. Hutumiwa mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa sentensi hiyo ni swali.

   **Mwa mfano:** Unaitwa nani?

b. Hutumiwa kuonyesha ukosefu wa uhakika kuhusu jambo kama vile mwaka.

   **Kwa mfano:** Shule hii ya Tumaini ilianzishwa 1992 (?)

**Mabano/parandesi ( )**

a. Hutumiwa kufunga maneno ya ziada katika sentensi.

   **Kwa mfano:** Nyamata (makao makuu ya Bugesera) inakua kwa kasi.

b. Hutumiwa na mwandishi anapotaka kutoa ufafanuzi kwa lugha nyingine tofauti na ile anayoitumia.

   **Kwa mfano:** Walowezi (settlers) walifukuzwa.

c. Hutumiwa kufungia herufi za kuorodhesha.

   **Kwa mfano:**

   (a) huelimisha, (b) huburudisha, (c) huonya.

***Mkwaju (/)***

Hutumiwa kuonyesha kuwa mojawapo ya vitu vilivyotajwa vyaweza kutumiwa badala ya hivyo vingine.

**Mfano:** Abera alishangaa/aliduwaa

***Mtajo: (" " au ' ')***

Hutumiwa kuonyesha maneno halisi ya mzungumzaji.

**Kwa mfano:** *"Nitafika kesho jioni," alisema mdogo wake.*

**Mkato au koma**

a. Hutumika kwa kutenganisha sehemu mbili za tungo
   Mfano: Mtoto anasoma Kiswahili, wazazi wanamtafutia karo.
b. Hutumika kwa kutenganisha maneno yanayofuatana.

   **Mfano:** Wao hufuga kuku, mbuzi, kondoo na ng'ombe.

## KAZI YA 5

**Tia alama za vituo mwafaka katika sentensi zifuatazo:**

1. Lo umemwona nyoka yule
2. unakwenda wapi
3. Unaitwa nani
4. Alinunua andazi mkate pipi biskuti na ndizi
5. Kigali mji mkuu wa Rwanda inavutia sana

## 12.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu ripoti

## KAZI YA 6

**Soma maelezo muhimu yafuatayo, kisha eleza umuhimu wa ripoti katika maneno yako.**

Ripoti ni maelezo yanayotolewa kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea. Aidha, ripoti ni taarifa inayohusiana na shughuli au jambo fulani lililofanywa au kufanyika. Ripoti huandikwa kwa madhumuni ya kutoa taarifa ili iweze kufanyiwa kazi au kuhifadhiwa kama kumbukumbu. Ripoti huandikwa pia kwa madhumuni ya kuarifu watu kuhusu mabadiliko muhimu au maendeleo ya shughuli fulani. Ripoti inaweza tena kuagiza utekelezaji fulani, kupendekeza kufanyika kwa jambo fulani na kupima au kutathmini utendakazi fulani au maendeleo yaliyofikiwa.

## 12.5. Kusikiliza na Kuzungumza

## KAZI YA 7


**Tunga ripoti ya jambo fulani ulilohudhuria kisha uisomee mwenzako.**

## 12.6. Kuandika: Utungaji wa ripoti

### KAZI YA 8

**Tunga ripoti kuhusu hali ya usafi katika shule yako.**

## SOMO 13: MFANO WA RIPOTI ZA MKUTANO



### KAZI YA 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

- Elezea kuhusu wahusika unaowaona kwenye mchoro huu.
- Wahusika hao wako wapi? Wanafanya nini?

## 13.1. Kusoma na ufahamu: Mfano wa ripoti za mkutano

**Soma ripoti ifuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

Mnamo tarehe 10/7/2020, wanafunzi wa mwaka wa tatu, Chuo cha Ualimu walifanya mkutano katika ukumbi wa shule yao kuhusu maandalizi ya mahafali yao.

Mkutano huo ulianza saa 4:00 asubuhi ambapo wanafunzi wa shule ya **IGANEZA** walifanya mkutano ili waweze kuweka vizuri mipango yao kuhusiana na hafla yao ya kuhitimu masomo ya Chuo cha Ualimu.

Mambo yaliyojadiliwa siku hiyo ni pamoja na haya yafuatayo:

i. Kuwakaribisha wazazi wao.

ii. Kuandaa michezo mbalimbali: mpira wa miguu, mpira wa kikapu, ngonjera, nyimbo, igizo, mashairi na muziki.

iii. Kuandaa zawadi kwa ajili ya walimu wao wa madarasa, walimu wa masomo na Mwalimu Mkuu wa shule.

iv. Kutoa mchango wa kununua zawadi hizo.

Wanafunzi walitoa mapendekezo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaalika wazazi wao, walimu na marafiki zao ili waweze kushiriki katika sherehe yao. Vilevile, mapendekezo mengi yalikuwa kuomba Mwalimu Mkuu wa shule awatafutie vifaa maalum kwa ajili ya sikukuu hiyo. Katika mkutano huo wanafunzi wote walikubaliana kutoa kiasi fulani cha faranga kulingana na uwezo wao ili kufanikisha shughuli hiyo.

Mkutano huo ulifungwa saa 6:00 baada ya wanafunzi kukubaliana kukutana tena wiki moja baadaye kwa ajili ya kukamilisha mpango wao.

**Imetayarishwa na:**

Jina: MUTESI Maria

Cheo: Katibu wa darasa

Saini……………………………..........

Tarehe: 14/7/2020

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Toa kichwa cha ripoti hii.
2. Mkutano unaosimuliwa ni wa kina nani?
3. Madhumuni ya mkutano yalikuwa yapi?
4. Matokeo ya mkutano huu ni yapi?

## 13.2. Msamiati kuhusu mfano wa ripoti

### KAZI YA 3

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

1. Mkutano
2. Hafla
3. Ukumbi
4. Kuchanga
5. Kiranja

### KAZI YA 4

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Mkutano
2. Kuandaa
3. Kuchanga
4. Kiranja
5. Ngonjera

## 13.3. Sarufi: Matumizi ya alama za vituo

### KAZI YA 5

**Angalia sentensi ambazo zinafuata na kujadili na mwenzako unavyoziona kisha ufanye maswali ya hapo chini.**

1. Ehee! Kumbe yeye ni mtoro!
2. Mtaalamu wa lugha shuleni kwetu ni mtu mpole kabisa.
3. Ameenda sokoni kununua vitu vingi: maembe, mapapai, machungwa, madaftari, kalamu na kuku.
4. Unaionaje hali ya hewa leo?
5. Masomo haya si ya kukuangamiza; masomo haya ni ya kuboresha hali ya maisha yako.

Ndani ya sentensi hizi kuna matumizi ya alama za vituo mbalimbali kulingana na maumbile ya kila sentensi. Kuna alama ya kushangaa, alama ya nukta au kituo, alama ya nukta mbili, alama ya mkato au koma, alama ya kuuliza au kiulizi pamoja na alama ya nukta na mkato.

## KAZI YA 6

**Tia alama za vituo mwafaka katika sentensi zituatazo:**

1. Alilima shamba akapanda mbegu akapalilia akavuna
2. Jina lako ni nani mwalimu wa Kiswahili aliniuliza
3. Binadamu mtu hupaswa kuishi kwa amani na wenzake
4. Mungu wangu mvua imenyesha
5. Mandhari setting ya eneo hili ni ya kupendeza

## 13.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu uandishi wa ripoti

## KAZI YA 7

**Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

Ripoti ni maelezo kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea. Ni aina ya kumbukumbu ambazo huandikwa kwa ajili ya matumizi ya baadaye. Ripoti inaweza kuwa ya uchunguzi wa utafiti kuhusu jambo fulani, inaweza kuwa ya polisi, daktari au ya tume fulani.

**Namna ya kuandika ripoti**

Kabla ya kuandika ripoti lazima kuwe na ushahidi unaohusu suala au jambo linaloandikiwa ripoti hiyo. Kwa hiyo, ni lazima mtunzi afanye uchunguzi kwanza. Pia mtunzi anapaswa kufahamu kiwango cha elimu na uwanja wa mtu anayemwandikia ripoti hiyo. Kwa mfano kama ni polisi, daktari, mwanasheria, mfanyabiashara, n.k. Lugha atakayoitumia mwandishi au mtunzi izingatie muktadha wa matumizi. Lugha itegemee aina ya ripoti. Hatua za uandishi wa ripoti

**a. Kichwa cha ripoti**

Mtunzi aandike kichwa cha ripoti ambacho kinaonyesha; kiini cha ripoti, sababu ya ripoti, tarehe ya tukio au jambo linaloandikiwa ripoti na mahali palipotokea jambo hilo.

**b. Utangulizi wa ripoti**

Katika hatua hii mtunzi hueleza kwa muhtasari madhumuni ya ripoti.

**c. Kiini cha ripoti**

Mtunzi aeleze mambo aliyoyaona, chanzo chake na madhara au faida yake.

**d. Hitimisho**

Katika kuhitimisha ripoti mtunzi aonyeshe msimamo na mapendekezo yake. Baada ya hitimisho mtunzi aandike au aonyeshe ripoti imeandikwa na nani, cheo chake (nafasi yake hasa katika ripoti hiyo) na tarehe ripoti hiyo ilipoandikiwa.

**Jibu Maswali yafuatayo**

1. Ripoti ni nini?
2. Kabla ya kutunga ripoti mwandishi analazimishwa nini?
3. Lugha itumiwayo kuandika ripoti inategemea nini?

## 13.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 8

**Tunga ripoti kuhusu mkutano wa wazazi wanaolelea katika shule yako baadaye uisomee wenzako darasani.**

## 13.6. Kuandika

### KAZI YA 9

**Andaa ripoti kuhusu mkutano uliohudhuria baada ya kufanya kazi ya umuganda.**

### TATHMINI YA MADA YA SITA

1. Eleza maana ya ripoti.
2. Taja sehemu kuu za ripoti.
3. Ni jambo gani la kutilia maanani kabla ya kuandika ripoti?
4. Afikisha sentensi zifuatazo:
   i. Binadamu mtu hupaswa kuishi kwa amani na wenzake
   ii. Mungu wangu Mvua imenyesha sana
   iii. Mandhari ya eneo hili ni ya kupendeza

# MADA 7

# HISTORIA YA LUGHA YA KISWAHILI

**Uwezo mahususi wa mada**
Kueleza dhima, asili au chimbuko la lugha katika jamii

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza asili ya lugha ya Kiswahili,
- Kudhihirisha ueneaji wa lugha ya Kiswahili barani Afrika,
- Kubainisha sababu za kubadilika kwa lugha,
- Kujadili asili ya Kiswahili,
- Kuonyesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili barani Afrika,
- Kuchunguza mabadiliko ya lugha katika mawasiliano,
- Kutambua aina za tungo,
- Kutofautisha tungo mbalimbali kulingana na aina zake.

## KIDOKEZO

**Tazama mchoro ufuatao kisha jibu maswali hapo chini.**



**Maswali:**

a. Unaona nini kwenye mchoro huu?
b. Ni lugha gani ya kiafrika ambayo ni rasmi nchini Rwanda na ambayo pia hutumiwa katika nchi za Afrika Mashariki?
c. Kwa maoni yako asili ya lugha hiyo ni ipi?

# SOMO LA 14: ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI

## 14.1. Kusoma na ufahamu : Asili ya lugha ya Kiswahili

**Soma kifungu cha habari kuhusu "Asili ya lugha ya Kiswahili" kisha, jibu maswali uliyotolewa hapo chini.**

Kiswahili ni lugha ya Kiafrika ambayo huhesabiwa katika lugha za Kibantu. Lugha hii ni maarufu sana ndani na hata nje ya bara la Afrika. Neno Kiswahili lilianza kutumika katika karne ya kumi na nne (Baada ya Kristo Kuzaliwa). Neno hili lilitoka kwa wageni wa Kiarabu waliokuja barani Afrika kwa shughuli zao za kibiashara. Wakati huo walifika Pwani ya Afrika Mashariki.

Eneo hili ndilo lililopewa jina la "*sawahil*" (au sahel) kwa maana ya eneo la watu wa pwani; yaani sehemu iliyo kandokando ya bahari au mwambao. Wenyeji wa sehemu hiyo ndio walioitwa "*sawahiliya*"*(Sawahel)*. Neno "Sahel" baadaye lilileta jina jingine "Kiswahili" kwa maana ya lugha ya watu wa sehemu hiyo ya pwani, ambapo watu wenyewe waliitwa Waswahili. Kiswahili ni lugha yenyewe. Watu wanaoizungumza lugha hiyo ni Waswahili wenye utu na utamaduni wao.

Hata hivyo, kuna mitazamo minne muhimu inayozungumzia kuhusu asili ya Kiswahili: Mtazamo wa kwanza ni ule unaotetea kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu. Watu wanaoshikilia mtazamo huu wanahoji kwamba katika lugha ya Kiswahili kuna maneno mengi ya Kiarabu. Maneno hayo ni kama vile laki, elimu, fahamu, daima, enzi, mahabusu, ilani, ratibu, nadra, jasisi, kauli, na mengineyo. Watetezi wa hoja hii wanaeleza pia kwamba Kiswahili kilitumiwa na wenyeji wa sehemu hiyo ya mwambao waliokuwa Waislamu. Kwa kuwa Uislamu ulileta na Waarabu, basi wao husisitiza kuwa lugha ya Kiswahili imeletwa na Waarabu hao.

Mtazamo wa pili ni wa kusema kwamba Kiswahili ni lugha chotara; yaani mchanganyiko wa lugha za pwani na Kiarabu. Madai haya yanajikita kwenye hoja kwamba wakati Waarabu walipokuwa wakifanya biashara, waliamua kukaa pwani na kuoa wanawake kutoka sehemu hiyo ya pwani. Kwa hivyo, ndoa hiyo kati ya wenyeji wenye lugha za Kibantu na Waarabu wenye lugha ya Kiarabu ndiyo iliyozaa lugha mpya iliyochanganya lugha ya Kiarabu na lugha nyingine za Kiafrika ili kuleta lugha chotara. Maana yake Kiswahili; mchanganyiko wa Kiarabu na lugha za Kibantu.

Mtazamo wa tatu hutetea Kiswahili kuwa lugha ya kibantu. Baadhi ya watetezi huchukua lugha ya Kiswahili kama lugha ya Kibantu ambayo ilikuwepo hata kabla ya majilio ya wageni; yaani lugha hii ilijitambulisha kama lugha ya Kibantu toka zamani. Wengine huitazama lugha ya Kiswahili kama lugha iliyotokana na mchanganyiko wa lugha tofauti za Kibantu zilizotumiwa sehemu ya pwani. Katika mawasiliano baina ya watumiaji wa lugha hizo, wao walilazimika kurahisisha lugha zao kwa kiasi fulani ili waweze kuelewana na kufanikisha shughuli zao katika maeneo mbalimbali.

Katika hali hii kulizuka lugha moja iliyoeleweka kwa watu wote wa eneo zima la upwa wa Afrika Mashariki kuanzia Kaskazini hadi Kusini. Matokeo yake yalikuwa lugha zilizojulikana kama lahaja za Kiswahili; yaani lugha zilizohusiana sana kiasi kwamba wazungumzaji wake waliweza kuzitumia na kuelewana kwa urahisi. Mifano ya lahaja hizo za Kiswahili ni Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbatu, Kibajuni, Kisiu, na Kiamu kwa uchache.

Mtazamo wa nne ni ule unaokiangalia Kiswahili kama pijini na baadaye ikaendelea hadi kufikia kuwa Kreoli. Pijini hujitokeza pale ambapo watu wanaotumia lugha tofauti wanapokutana hujaribu kutafuta lugha rahisi ya kufanikisha mawasiliano ya pande hizo mbili. Kila upande huchangia kutoa msamiati. Sarufi ya pijini huwa rahisi sana. Hivyo Kiswahili kinatazamwa kama kilichoanza kutokana na mchanganyiko wa lugha kadhaa za Kibantu zilizokuwa katika upwa wa Afrika Mashariki na ikaathiriwa sana na Kiarabu, kimsamiati katika kukua kwake.

Kwa kweli, ni lazima maoni ya watu mbalimbali kuhusu asili ya Kiswahili yachunguzwe kwa makini, ili yasiweze kupotosha watu wenye hamu ya kujua mengi kuhusu asili ya lugha hiyo. Kiswahili ni lugha yenye thamani kubwa katika Afrika nzima na hata nje ya Afrika. Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye uhusiano na lugha nyingine za Kibantu kama zilivyo lugha ya Kinyarwanda na Kirundi. Asili yake au chimbuko lake ni sehemu ya pwani ya Afrika Mashariki ambako kulizungumzwa lugha mbalimbali za Kibantu zilizofanana sana.

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Neno “Kiswahili” lilianza kutumiwa lini?
2. Neno “Kiswahili” lilitoka wapi? Eleza zaidi jibu lako.
3. Katika kifungu chetu tunaweza kupata mitazamo minne ya asili ya lugha ya Kiswahili. Taja mitazamo hiyo yote kwa ufupi.

4. Kwa nini baadhi ya watu walifikiria kuwa Kiswahili kilitokana na Kiarabu? Taja maneno matatu ya Kiswahili ambayo yalitokana na Kiarabu.
5. Kusema kwamba lugha ni "chotara" ni kumaanisha nini?
6. Asili ya Kiswahili ni ipi?
7. Taja lahaja za Kiswahili ambazo zinapatikana katika kifungu ulichosoma.
8. Waarabu walifika kwenye sehemu za pwani Afrika Mashariki kwa lengo gani?
9. Kwa nini ni lazima kuchunguza kwa makini maoni ya watu mbalimbali kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili?
10. Taja lugha za Kibantu zilizozungumziwa katika kifungu cha habari ulichosoma.

## 14.2. Msamiati kuhusu asili ya lugha

### KAZI YA 2

**Andika maana za maneno haya yafuatayo kwa kuzingatia matumizi yake katika kifungu ulichosoma hapo juu, kisha utunge sentensi kwa kutumia maneno hayo:**

1. Kibantu
2. Chotara
3. Chimbuko
4. Pwani
5. Mawasiliano
6. Maarufu
7. Utu
8. Utamaduni
9. Lahaja
10. Watetezi

## 14.3. Sarufi: Aina za sentensi

### KAZI YA 3

**Eleza mpangilio wa maneno katika sentensi au tungo zinazofuata:**

1. Mama amepika chakula kitamu sana.
2. Abayo anapenda kuangalia mpira wa kandanda.
3. Mayai yaliyokaangwa ni matamu sana.
4. Musaniwabo ni mdogo.
5. Nyumba zilizojengwa bondeni zitaharibika.
6. Mimi ninafua nguo lakini mama anasafisha sahani.

### Maelezo muhimu

Kiswahili kina mipangilio mbalimbali ya sentensi. Baadhi ya sentensi huwa ndefu ilhali nyingine huwa fupi. Kwa hiyo, kuna sentensi zilizojengwa kwa neno moja tu, maneno mawili au zaidi. Sentensi hizo zinaweza kubeba aina mbalimbali za maneno kama vile nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi na kiwakilishi.

**Kwa mfano:**

1. Tunasoma.
2. Wanafunzi wazuri walifaulu mitihani yao.
3. Wao wanasoma vizuri.
4. Baba na mama wamekwenda shambani.

Sentensi zote za lugha ya Kiswahili zinaweza kuwekwa katika makundi matatu muhimu: Sentensi sahili, Sentensi ambatano na Sentensi changamano.

**a. Sentensi sahili**

Hizi ni sentensi ambazo huundwa kwa kitenzi kikuu kimoja na zenye maana kamili iliyokusudiwa. Kitenzi chaweza kuwa kitenzi kikuu pekee au kitenzi kikuu kilichoandamana na kitenzi kisaidizi. Pengine sentensi hii huweza kuundwa na kitenzi kishirikishi.

1. **Kitenzi kikuu:** Kitenzi hiki hutoa taarifa ya tendo linalotendeka katika sentensi.

**Mfano:** - Maria **anaendesha** gari kubwa.

- Bibi **amebeba** mtoto mgongoni.
- Ndoli **anaogelea** mtoni.

2. **Kitenzi kisaidizi - kitenzi kikuu (TS+(-) + T):** Kitenzi kisaidizi hufanya kazi ya kusaidia kitenzi kikuu kukamilisha maana yake.

**Mfano**:- Watoto **walikuwa** *wanacheza* mpira (watoto = **N**, walikuwa = **TS**, wanacheza = **T**, mpira = **N**).

- Bamurange **alikuwa** *anataka* alama nyingi.

3. **Kitenzi kishirikishi (t):** Hiki hakionyeshi viambishi vyote vinavyojenga kitenzi kama ilivyo katika vitenzi vya kawaida.

**Mfano**: - Wanafunzi **ni** watu wazuri.

- Chakula **ki** mezani.
- Yeye **yu** shuleni.
- Mtoto **angali** njiani

**b. Sentensi ambatano**

Hizi ni sentensi zenye sehemu mbili au zaidi zinazounganishwa na kiunganishi kama vile *na* au *lakini*. Sehemu hizo huwa huru kwani kila moja inaweza kusimama pekee ikiondolewa katika sentensi kuu.

**Mfano**: - Wanafunzi wanaingia darasani lakini mwalimu wao hajaingia.

- Baba analima na mama anapanda mbegu.

**c. Sentensi changamano**

Hizi ni aina za sentensi ambazo huundwa kwa tungo tegemezi moja au zaidi, pamoja na tungo nyingine iliyo huru; yaani yenye muundo sahili. Tungo huwa tegemezi kutokana na hali yake ya kutoweza kujitosheleza kimaana; yaani haiwezi kusimama pekee na kuleta mana kamili bila kusaidiwa na tungo nyingine.

**Mifano:**

1. Mbuzi aliyepotea jana / ameonekana leo.
2. Mayai yaliyokaangwa / ni matamu sana.
3. Barabara zilizojengwa vibaya / zitajengwa upya.
4. Bibi aliyepika chakula ambacho ni kitamu sana / ameungua mkono.

## 14.4. Matumizi ya lugha: Mitazamo tofauti kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili

### KAZI YA 4

**Someni kifungu kifuatacho kwa kujaza nafasi zilizoachwa wazi, ukitumia baadhi ya maneno yafuatayo:** (a)Kiarabu, (b)Kibantu, , (c)Mashariki, (d)pwani, (e)Waislamu, (f)wamezaa, (g) kuiheshimu, (h)huwasiliana.

Mzee Habibu na mkewe huwasiliana katika lugha ya Kiswahili. Lugha hiyo ni lugha ya (1)................. kama vile Kinyarwanda, Kirundi na Kilingala. Mzee Hassan ambaye ni rafiki yake Mzee Habibu ni (2)............... Kila Ijumaa huenda msikitini kusali katika lugha ya (3)......... Zabibu Binti yake Hassan aliolewa na mwanamume Mwarabu. Hivi sasa (4).................. watoto wawili. Watoto hao (5)................. katika mchanganyiko wa Kiswahili na Kiarabu. Kila wanapowasikia wakizungumza, baba zao huwakumbusha kuwa asili ya Kiswahili ni (6)........ ya Afrika (7)............. na kwamba wanapaswa (8).............. na kuacha kuichanganya na lugha nyingine.

### KAZI YA 5

**Eleza kwa machache mitazamo kuhusu asili ya Kiswahili.**

## 14.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

### KAZI YA 6

**Shirikiana na wenzako katika kujadili kuhusu nafasi ya Kiswahili katika shule za Rwanda sasa hivi.**

## 14.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari


### KAZI YA 7

**Tunga kifungu chenye mada ifuatayo: "*Umuhimu wa Kiswahili katika jamii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.*" Hakikisha kwamba umetumia ukurasa mmoja.**

# SOMO LA 15: KUENEA KWA LUGHA YA KISWAHILI

## KAZI YA 1

**Tazama michoro hapo chini kisha utoe maoni yako kuhusu mambo yanayoendelea.**







## 15.1. Kusoma na ufahamu: Kuenea kwa lugha ya Kiswahili

**Soma kifungu cha habari kuhusu maenezi ya lugha ya Kiswahili, kisha jibu maswali uliyotolewa hapo chini.**

Tunaposema kuwa lugha fulani imeenea, tunamaanisha kuwa lugha hiyo imeongeza idadi ya watumiaji wake katika nchi inamotumika au hata na nje ya nchi hiyo. Idadi ya watumiaji wake huzidi kuongezeka hatua kwa hatua mpaka lugha hiyo inavuka mipaka ya awali na kusambaa mahali kwingi duniani. Leo hii, kwa mfano, lugha ya Kiswahili ambayo chimbuko lake la asili ni Pwani ya Afrika Mashariki, huzungumzwa katika nchi nyingi za Afrika kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji na mahali pengine pengi katika bara la Afrika na nje yake.

Ueneaji wa lugha ya Kiswahili ulitokana na shughuli mbalimbali za watu waliokuwa wakitumia lugha hiyo. Wenyeji wa pwani pamoja na watumiaji wa lugha ya Kiswahili walihitaji kuwasiliana na watu wengine, hivyo mawasiliano hayo yakasaidia lugha ya Kiswahili kuweza kuenea katika sehemu nyingine ambapo Kiswahili kinatumiwa mpaka sasa. Safari za kibiashara baina ya watu kutoka pwani hadi bara zilikuwa zikifanywa mara kwa mara. Kwa njia hii matumizi ya lugha ya Kiswahili yalizidi kuenea katika nchi mbalimbali ambako biashara hizo zilikuwa zikifanyika.

Sababu nyingine iliyochangia kueneza lugha ya Kiswahili ni misafara ya watumwa iliyokuwa ikifanywa na Waarabu. Kila mahali watumwa hao walipopitia, waliacha athari za lugha hii ya Kiswahili.

Shughuli za kiutawala na utangazaji wa imani za dini nazo zilisaidia sana katika kuisambaza lugha hii ya Kiswahili. Ujenzi wa makanisa na misikiti, makao makuu ya utawala pamoja na shule ni miongoni mwa mambo mengi yaliyosaidia kuenea kwa Kiswahili. Katika hali hii, mchango wa wakoloni, wasafiri wa kiarabu na hata wamishenari kutoka sehemu za pwani hadi maeneo mengine ya bara la Afrika ulikuwa mkubwa sana. Wakoloni katika Afrika Mashariki waliwashurutisha watumishi wao kuzungumza na kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kikazi kwani walifikiri kuwa lugha hii ya Kiswahili ilikuwa rahisi kujifunza kuliko lugha nyingine za kiasili.

Aidha, katika mfumo wa kufanikisha utawala, Waafrika na Wakoloni walitumia Kiswahili ili kurahisisha mawasiliano baina yao. Kwa mfano, Wajerumani katika kipindi chao kifupi cha utawala, hukoTanganyika walianzisha shule zilizotoa elimu kwa Kiswahili; na hii ilikuwa hatua muhimu iliyosaidia sana kueneza Kiswahili nchini kote. Waingereza walipofika nao walichangia sana kwa kuchukua hatua kubwa mnamo mwaka 1934 ambapo waliunda kamati kwa lengo la kufuatilia usanifishaji wa lugha ya Kiswahili. Wamishenari kwa upande wao, waliamua kutumia lugha ya Kiswahili kuwahubiria waumini wao mpaka wakajenga shule ambapo walifundisha lugha ya Kiswahili kwa madhumuni ya kuweza kueneza Injili.

Tangu wakati huo, Kiswahili kimezidi kuenea na kusambaa duniani kote kiasi kwamba siku hizi kimeishapata hadhi ya kuwa mojawapo ya lugha muhimu za kimataifa. Juhudi nyingine nyingi zinazidi kufanywa ili kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili barani Afrika na nje yake. Miongoni mwa shughuli muhimu zinazoweza kusisitiziwa hapa ni pamoja na uandishi wa vitabu vya Kiswahili, magazeti yanayotumia lugha ya Kiswahili, taasisi mbalimbali za kuendeleza Kiswahili na vyombo vya habari kama vile redio na televisheni zenye matangazo, habari na vipindi katika lugha ya Kiswahili.

Nje ya bara la Afrika, Kiswahili hutumika sana katika shughuli nyingi za kibiashara, elimu, siasa na dini. Mpaka sasa idadi ya vyuo vinavyofundisha lugha ya Kiswahili imeongezeka huko Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na Marekani ambapo watu wengi hujivunia kiwango cha masomo yanayotolewa katika lugha hii pamoja na kazi za utafiti zinazoendelezwa na wataalamu wa Kiswahili. Kumejitokeza idhaa za Kiswahili katika redio nyingi duniani, na watu wengi hufurahia vipindi na matangazo yanayotolewa kwa lugha hii. Vilevile, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili huzidi kuenea mahali pengi kwa kuwavutia wengi. Hivi sasa, idadi ya wapenzi wake huzidi kuongezeka kila kukicha.

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

**Soma kifungu hiki cha habari, kisha ujibu maswali yanayofuata.**

1. Mbali na nchi za Bara la Afrika, taja mahali pengine ambapo Kiswahili kinatumiwa.
2. Tunaposema kwamba lugha imeenea ni kumaanisha nini?
3. Ni shughuli zipi zinazochangia kueneza Kiswahili?
4. Ni nini maana ya watumwa wanaozungumziwa katika kifungu hiki?
5. Kwa nini wakoloni walizishurutisha baadhi ya nchi za Afrika kutumia Kiswahili?
6. Kwa nini wamishenari waliamua kutumia lugha ya Kiswahili?
7. Wakoloni walikuja barani Afrika kwa malengo gani?
8. Ni lugha nyingine zipi za kimataifa zinazotumiwa katika eneo la nchi za Afrika zinazotumia Kiswahili?
9. Kiswahili kimeathiri vipi lugha za kiasili katika nchi kinapotumiwa? Toa mifano.
10. Ujuzi wa Kiswahili una umuhimu gani kwako?
11. Eleza jinsi wageni walivyoathiri lugha ya Kiswahili kwa kutoa mfano.

## 15.2. Msamiati kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili na mabadiliko yake

## KAZI YA 3

**Tafuta maana za msamiati unaofuata kulingana na matumizi yake katika kifungu ulichosoma, kisha utunge sentensi kwa kutumia maneno hayo.**

1. Sambaa
2. Wenyeji
3. Watumwa
4. Walishurutisha
5. Kamati
6. Mathalan
7. Imani
8. Kuimarisha

## KAZI YA 4

**Chunguza jedwali hapo chini ili uandike maneno kamili yaliyopo Kwa mfano: "WAARABU"**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | O | P | K | I | S | W | A | H | I | L | I | T |
| G | A | C | I | D | H | A | A | N | O | E | M | E |
| A | F | G | W | W | D | L | R | T | L | N | A | L |
| J | R | A | A | A | V | I | H | K | U | G | N | E |
| K | I | U | T | A | A | S | I | S | I | O | I | V |
| L | K | Y | U | R | J | H | O | P | W | A | N | I |
| O | A | R | M | A | B | U | R | U | N | D | I | S |
| D | A | F | W | B | A | R | W | C | D | S | O | H |
| E | R | D | A | U | D | U | A | S | I | A | M | E |
| K | E | N | Y | A | H | T | N | F | O | A | A | N |
| A | B | C | V | T | I | I | D | A | D | I | L | I |
| M | N | H | E | K | U | S | A | M | B | A | A | L |
| A | L | I | L | I | S | H | W | A | L | E | W | E |
| T | S | O | P | R | S | W | U | V | W | Y | I | Z |
| I | N | J | E | Z | B | A | R | A | C | D | H | A |

## KAZI YA 5

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno haya:**
kimesambaa, kuimarisha, watumwa, vituo, walishauriwa, kamati, wenyeji, imani, mamlaka, idhaa.

1. Wanafunzi ................................ kuzungumza lugha Kiswahili kama njia bora ya kujua lugha hiyo.
2. .....................................walisafirishwa kutoka Afrika kuelekea Marekani.
3. Kiswahili .................................katika sehemu mbalimbali za dunia.
4. ........................................wa eneo hilo wamefurahishwa na shule waliyojijengea.
5. Sehemu tofauti za pwani barani Afrika zilitumiwa kama .......................vya utumwa.

6. Kuna ...................................mbalimbali zinazotangaza habari katika Kiswahili.
7. Kumeundwa ........................... ya kushughulikia elimu ya watu wazima.
8. Rais wa Jamhuri ya Rwanda amepewa ..............................ya kuiongoza nchi ya Rwanda.
9. Kila madhehebu humwenzi Mungu kulingana na ...................yake.
10. Serikali ina jukumu la ......................................amani nchini.

## 15.3. Sarufi kuhusu aina za sentensi/tungo

### KAZI YA 6

**Taja aina za sentensi hizi:**

1. Mwalimu anafundisha na wanafunzi wanaandika.
2. Angelikufahamu asingelikupita.
3. Mkurugenzi ni rafiki yangu lakini mwalimu wa mitaala ananishambulia sana.
4. Ningalijua mapenzi yako ningalikuoa.
5. Mtoto anatumia penseli ingawa kalamu inaandika vizuri.

### Maelezo muhimu kuhusu aina za sentensi

**a. Sentensi ambatano**

Kama ilivyoelezwa hapo juu, sentensi ambatano ni aina za sentensi ambazo huundwa kwa sentensi zenye miundo tofauti pamoja na kiunganishi "na" au "lakini," n. k. Kiunganishi hicho ndicho hufanya kazi ya kuunganisha sentensi zenyewe ili kuunda sentensi ambatano. Muungano huo unaweza kuwa kama ifuatayo:

**1. Sentensi sahili + sentensi sahili**

**Mifano**: - Mama analima/ **na** /Baba anapanda mbegu.

- Bibi anasoma kitabu **na** mama anapika chakula.

**2. Sentensi changamano + sentensi changamano**

**Mifano**: - Ng'ombe aliyezaa amepotea / **na** / ndama aliyezaliwa amekufa.

- Mtoto aliyepotea ameonekana / **ingawa** /walioenda kumtafuta hawajarudi.

3. **Sentensi changamano + sentensi sahili**

**Mifano**: -Dereva aliyesababisha ajali amekufa / **lakini** /abiria wote wamenusurika.

- Wanafunzi waliohudhuria masomo wote wanafaulu / **ingawa** / hawakupewa tuzo.

**Tanbihi:** Wakati mwingine alama ya **mkato** (,) hutumika kama kiunganishi katika sentensi ambatano.

**b. Sentensi shurutia**

Hii ni aina ya sentensi ambazo huundwa kwa vishazi tegemezi. Vishazi tegemezi hivyo huwa na virejeshi ambavyo kwa wakati wake huwa na dhamira za masharti ambayo yamejikita katika mofimu za *-nge*, *-ngeli*, *-ngali*, na -ki- ya masharti. Mofimu hizi hazichanganywi. Ikiwa unatumia mofimu ya -nge- upande wa kwanza, sharti (ni lazima) utumie mofimu -nge- upande wa pili. Sentensi hizi huitwa pia sentensi shurutishi au sentensi zenye masharti.

**Mifano ya sentensi:**

- Angeniomba / ningempa.
- Ungepata bomba / tungekunywa maji safi na salama.
- Tukisoma kwa bidii/ tutafaulu.
- Wakija / nitawapeleka.
- Angeniuliza / ningemjibu.
- Angelitumia dawa / angelipona

## 15.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili

### KAZI YA 7

**Chunguza maelezo haya yafuatayo kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili kisha, ujadili mambo muhimu yaliyochangia kuenea kwake.**

### Maelezo muhimu

Ueneaji wa Kiswahili ulitokana na wenyeji wa pwani pamoja na watumiaji wa Kiswahili waliohitaji kuwasiliana na watu wengine, hivyo mawasiliano hayo yalisaidia lugha ya Kiswahili kuweza kuenea katika sehemu nyingine ambapo Kiswahili kinatumiwa mpaka sasa.

Kuna shughuli mbalimbali zilizochangia kueneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali za dunia kama vile safari za kibiashara baina ya watu kutoka pwani hadi bara, uandishi wa vitabu vya Kiswahili, magazeti yanayotumia lugha ya Kiswahili, taasisi mbalimbali za kuendeleza Kiswahili na vyombo vya habari kama vile redio, televisheni na tovuti.

Leo hii Kiswahili kimefika nje ya bara la Afrika kama vile Uingereza, Ujerumani, Ufaransa na Marekani ambapo Kiswahili kinafundishwa katika vyuo vikuu. Hivi sasa, idadi ya watumiaji wa Kiswahili inazidi kuongezeka kila kukicha.

Kadiri lugha ya Kiswahili ilivyozidi kuenea ndivyo ilivyozidi kukua na kubadilika kimsamiati. Kubadilika kwa lugha ya Kiswahili si hali yake ya kipekee kwani lugha kama chombo cha mawasiliano kati ya watu, inapotumiwa, huendelea na kupata mabadiliko mbalimbali. Mabadiliko ya lugha ya Kiswahili yanatokana na sababu mbalimbali. Sababu hizo ni kama vile kuingiliana kwa watumiaji wa Kiswahili na wengine, kwa mfano: Wareno, Wachina, Wajerumani, Waarabu na wengine. Wageni hawa waliathiri lugha ya Kiswahili kupitia vitu vipya walivyoleta katika eneo la Afrika Mashariki. Baada ya kuona dhana hizo mpya, Kiswahili kilianza kufyonza maneno ya lugha hizo za kigeni na kuyatumia. Kwa mfano neno "dirisha" kutoka Kiajemi (diricha), "pesa" kutoka Kihindi "paisa", "eropleni" kutoka Kiingereza, n.k.

Sababu nyingine ni kuchukua maneno ya kawaida na kuyapa maana mpya ya kisiasa. Baadhi ya maneno haya ni kama vile kitenzi " kunyonya" kilichopewa maana ya Wakoloni kuchukua uchumi wa nchi zetu. Hivi, hao huitwa "wanyonyaji." Neno "kupe" kama mdudu anayeishi kwa kunyonya damu ya wanyama alihusishwa na "mnyonyaji uchumi" katika uwanja wa kisiasa.

Tunapozungumzia mabadiliko ya lugha ya Kiswahili na sababu zake, hatuwezi kusahau mahitaji ya jamii katika kutumia lugha ili iweze kujieleza katika shughuli mbalimbali za kisiasa, za kitaaluma na hata za kidini. Kuna msamiati mpya uliongizwa katika lugha ya Kiswahili kutokana na mahitaji haya (mifano: themometa, protini,...) katika taaluma ya uganga; "futari" katika taaluma ya dini ya kiislamu.

Isitoshe, kuna mabadiliko yaliyojitokeza katika sura ya miundo ya sentensi za Kiswahili, kubadili msamiati wa kale na kuupa sura mpya kimatumizi siku hizi (mifano: chichwa: kichwa, mato: macho, swi: samaki, mbi: mbaya, ...).

Mwishowe, lugha ya Kiswahili hubadilika kulingana na marika ya watumiaji au mahali inapotumiwa yaani rejesta.

## 15.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

### KAZI YA 8

**Jadilini kuhusu nafasi ya Kiswahili barani Afrika kulingana na lugha nyingine za kimataifa.**

## 15.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

### KAZI YA 9

**Kwa kuzingatia sentensi ambatano na sentensi shurutia, tunga kifungu cha habari kuhusu mada ifuatayo "Kiswahili ni Lugha ya Kimataifa."**

### TATHMINI YA MADA YA SABA

1. Eleza shughuli zilizochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali ulimwenguni.
2. Zungumzia kwa ufupi asili ya Kiswahili.
3. Eleza aina za sentensi ulizosoma katika mada hii na kutoa mfano wa sentensi kwa kila aina.

# MADA 8

# MATUMIZI YA KISWAHILI KATIKA MAZINGIRA MBALIMBALI

## Uwezo mahususi

Kuwasiliana kwa ufasaha kwa kutumia Kiswahili sanifu kulingana na mazingira husika.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kutambua na Kueleza msamiati maalum kulingana na mazingira mbalimbali.
- Kutaja majina ya watu tofauti wanaopatikana katika mazingira husika.
- Kutumia msamiati maalumu kulingana na mazingira mbalimbali husika.
- Kuheshimu na kutunza mazingira mbalimbali.
- Kuwasiliana na kujenga uhusiano mwema kati ya watu mbalimbali katika mazingira tofauti.
- Kutumia kimazungumzo na kimaandishi kiambishi cha hali -KI-.
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia majina ya ngeli ya -KU-

## KIDOKEZO

**Tazama kwa makini mchoro ufuatao kisha ueleze kile kinachoendelea**



## SOMO 16: MATUMIZI YA MSAMIATI KATIKA MAZINGIRA YA BENKI

### 16.1. Kusoma na ufahamu: Mutesa aingia benkini

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali ya ufahamu.**

Meneja wa Benki na Mutesa

**Mutesa**: Hodi! Hodi!

**Meneja**: Karibuni! Kaeni hapa!

**Mutesa**: Asante Meneja!

**Meneja**: Nikusaidie nini?

**Mutesa**: Tafadhali Meneja! Nilikuwa na akaunti yangu katika benki yenu lakini leo haitumiki.

**Meneja**: Naam! Nambari ya akaunti yako ni ipi?

**Mutesa**: Nambari ya akaunti yangu ni 000-44567-00.

**Meneja**: Ahaa! Ngoja nichunguze vizuri kwenye tarakilishi hii ili nijue tatizo lilikuwa lipi. Ahhh! Mbona akaunti yako imesinzia! Kumepita muda mrefu bila kuitumia. Ulikabiliana na matatizo gani?

**Mutesa**: Ni kweli, ilifungwa? Nilikuwa nikipitishia mshahara wangu kwenye akaunti hii na kibarua changu kikaisha miezi kumi iliyopita. Sijui kama naweza kuitumia tena!

**Meneja**: Aah! Uamuzi mzuri sana huo! Lakini nimekwambia kuwa akaunti yako imesinzia haijafungwa kwa kuwa inafungwa kwa hiari yako. Je, ulikuwa ukitumia hundi?

**Mutesa**: Hundi ni nini Meneja?

**Meneja**: Hundi ni kikaratasi maalum ambacho hutumiwa kuchukulia na kuwekea pesa benki. Kikaratasi hiki humrahisishia mteja kupata pesa wakati wowote bila usumbufu au kuidhinisha malipo ya mtu mwingine bila ulazima wa kwenda naye benki. Jambo hilo humrahisishia mwenye akaunti kutotembea na pesa mfukoni kwani huweza kwenda kuzichukua wakati wowote kwa kutumia kikaratasi hicho. Mwenye akaunti, kwa mfano, huweza kujaza hundi na kuisaini kisha akampa mtu anayetaka alipwe. Hundi hiyo ndiyo anayoiwasilisha benki ili apewe faranga zake hata kama mwenye akaunti hayupo.

**Mutesa**: Asante sana kwa maelezo hayo Meneja. Lakini mimi sikutumia kikaratasi hicho. Nilikuwa na kiotomotela yaani kadi ya benki na ilikuwa muhimu sana kwangu.

**Meneja**: Haya. Hundi nayo ni muhimu na wateja wengi hupenda kuitumia. Angalia hapa nikuonyeshe! Hii ni hundi. Unachofanya ni kujaza nafasi hizi zilizo wazi ili uweze kuitumia. Kama unamwandikia mtu hundi, unajaza jina lake hapa na kuweka sahihi baada ya kuhakikisha kwamba umeandika kwa usahihi kila kitu, yaani kiasi cha faranga unazompa na majina yake sahihi.

**Mutesa**: Je, mambo hayo yanatosha ili mwenye kuandikiwa hundi apewe pesa ?

**Meneja**:Hapana! Kwanza kama nilivyokuelezea, mwenye kuandika hundi anajaza nafasi hii ya mbele ya karatasi kwa kuandika jina la anayestahili kulipwa pesa, kiasi cha faranga anazostahili kulipwa kwa maneno na tarakimu pamoja na tarehe ya kutoa idhini yake. Lakini, anayepokea hundi naye anapaswa kujaza sehemu ya nyuma ya karatasi hiyo kwa kuandika jina lake, nambari ya kitambulisho chake, mahali na tarehe ya kuchukua pesa hizo, kisha akaweka sahihi.

**Mutesa**: Aa! Aah! Asanteni sana! Maelezo hayo yananifurahisha sana na ninaona kwamba mara hii nami ninapaswa kuwa na hundi.

**Meneja**: Si hayo tu! Kuna karatasi nyingine muhimu sana zitumiwazo katika benki kama stakabadhi au risiti, nayo hutumiwa kwa kuweka na kutoa pesa kwenye akaunti ya mteja. Karatasi hii nayo hujazwa kulingana na maandishi ya maelekezo yaliyowekwa. Unachofanya ni kuisoma tu kisha ukaandika kila jambo katika nafasi yake.

**Mutesa**: Vizuri sana. Ninaona kuwa karatasi hiyo haina utata wowote. Lakini, kadi yangu nayo ilimaliza muda wake. Ninafikiri kwamba nitapewa nyingine kwani hata na nenosiri la kadi silikumbuki. Nilifurahia jinsi ilivyoweza kunisaidia kuchukua pesa kwenye akaunti yangu kupitia njia ya teknolojia wakati wowote bila kuingia ndani ya benki.

**Meneja**: Haya. Ngoja tuiamshe tena akaunti yako. Mengine tutazidi kukufafanulia. Ninafurahia jinsi unavyoyaelewa yote yanayotendeka katika benki yetu na huduma zote tunazotoa kwa wateja wetu. Haya! Kila kitu kipo tayari, akaunti yako waweza kutumia. Nenda umwone afisa wa huduma kwa wateja, akupe fomu za kujaza ili uweze kupewa hundi na kadi mpya.

**Mutesa**: Asante sana meneja kwa kunihudumia vizuri sana! Lakini nina fedha chache ninazotaka kuweka kwenye akaunti yangu. Nifanyeje?

**Meneja**: Utaenda pale dirishani na keshia atakusaidia. Karibu sana! Kwa heri ya kuonana! Na ukiwa na mradi pamoja na dhamana ukihitaji mtaji, njoo tukupatie mkopo kwa faida nafuu kuliko benki nyingine. Afisa mikopo atakueleza taratibu za kufuata.

**Mutesa**: Haya! Nitarudi hivi karibuni kwa sababu nina kitegauchumi ambacho nigependa kuanzisha. Asante sana! Kwa heri ya kuonana!

## KAZI YA 1

**Maswali ya Ufahamu**

1. Akaunti ya Mutesa ilikuwa na shida gani?
2. Hundi ina manufaa gani kwa mteja?
3. Ni mambo gani yanayopaswa kujazwa na mwenye hundi ili atoe idhini ya kuchukua faranga kutoka kwa akaunti yake?
4. Kadi ya benki ina umuhimu gani kwa mteja?
5. Taja aina mbalimbali za karatasi zinazotumiwa katika benki na kueleza matumizi yake.
6. Badala ya kutumia kadi, taja njia nyingine moja mtu anaweza kuitumia akaweka au akapata pesa kutoka kwenye akauti yake bila ya kuingia benkini.
7. Kwa sababu gani katika mazungumzo walitumia maneno yasiyo ya asili ya Kiswahili?

## 16.2. Msamiati kuhusu mazungumzo

## KAZI YA 2

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

i. Nenosiri
ii. Mtaji
iii. Mkopo
iv. Stakabadhi
v. Keshia

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

i. Hundi
ii. Kadi ya benki
iii. Kufungua akaunti
iv. Uamzi mzuri
v. Kibarua

## 16.3. Sarufi: Matumizi ya kiambishi hali -ki-

## KAZI YA 4

**Chunguza sentensi zifuatazo na kujadiliana na wenzako kuhusu matumizi ya -ki-:**

1. U**ki**safisha mwili na nguo zako utaishi maisha mazuri.
2. M**ki**gonga mlango mtafunguliwa.
3. Tulipofika alikuwa a**ki**cheza mpira.
4. Tutaonana Mungu a**ki**penda.
5. A**ki**taka kushinda, yeye hufanya juu chini ili apate alama nzuri.

### Maelezo muhimu

Kiambishi –ki- ni kiambishi kinachotumiwa katika hali mbili.

- Kwanza kiambishi hiki hutumiwa kwa kuonyesha tendo katika hali ya masharti (masharti yanayowezekana) katika hali yakinishi. Katika hali kanushi kiambish huwa –**sipo**- na hutumiwa pamoja na vikanushi **hu**-, **ha**- na **si**-

**Mifano:**

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| U**ki**gonga mlango utafunguliwa | U**sipo**gonga mlango **hu**tafunguliwa. |
| Ni**ki**lala sana nitachelewa kwenda shule | Ni**sipo**lala sana **si**tachelewa kwenda shule |
| Wa**ki**chokoza wenzao waadhibiwe. | Wa**sipo**chokoza wenzao wa**si**adhibiwe. |
| Wa**ki**chokoza wenzao wataadhibiwa. | Wa**sipo**chokoza wenzao **ha**wataadhibiwa. |

- Pili –ki- inaonyesha vitendo ambavyo hutendeka/vinavyotendeka/vilivyotendeka au vitakavyotendeka kwa wakati mmoja.

**Mifano:**

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| Mama a**ki**lala watoto **hu**angalia runinga. | Mama a**sipo**lala watoto **ha**waangalii runinga |
| Mtoto a**me**kwenda shuleni a**ki**lia. | Mtoto **ha**jaenda shuleni akilia. |
| Baba a**na**lima shamba a**ki**sikiliza redio. | Baba **ha**limi shamba akisikiliza redio. |
| Dereva aliadhibiwa kwa sababu a**li**endesha gari a**ki**nywa pombe. | Dereva hakuadhibiwa kwa sababu **ha**kuendesha gari a**ki**nywa pombe. |
| Dereva ataadhibiwa a**ta**kapoendesha gari a**ki**wa amelewa. | Dereva hataadhibiwa a**sipo**endesha gari a**ki**wa amelewa. Dereva hataadhibiwa a**ta**kapoendesha gari a**sipo**kuwa **ha**jalewa. |

## KAZI YA 5

**Kanusha sentensi zifuatazo:**

1. Nikikawia kwa dakika nyingine, nitakosa usafiri.
2. Atakuwa akiwahutubia utakapokuwa ukiwasili.
3. Yeye akiachiwa urithi atafurahi.
4. Mvua ilinyesha jana tulipokuwa tukisoma somo la Kiswahili.
5. Ukisoma kwa bidii, utapita mtihani.

## 16.4. Matumizi ya lugha: Msamiati wa benkini

## KAZI YA 6

**Soma maelezo yafuatayo kuhusu msamiati wa benkini kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

Msamiati unaotumiwa katika mazingira ya benki ni mpana sana kwa sababu uwanja huu unahusiana na maisha ya jamii moja kwa moja.

Benki ni taasisi au shirika la fedha linalohifadhi na kukopesha fedha kwa wateja wake wanaotaka kuendesha miradi yao mbalimbali. Miradi hiyo huweza kuwa ya kuzalisha mali kama vile kufanya biashara, kuanzisha shule, kushughulikia kilimo na ufugaji, ufinyanzi, kufyatua matofali, kununua magari ya abiria na kubebea mizigo, kujenga nyumba za kupangisha, na kadhalika. Miradi hii yote inaomba mtaji. Ndiyo maana wateja huenda benkini kukopa fedha.

Benki ni za aina nyingi. Kuna benki kuu ya taifa, benki za kibiashara, benki ndogo (zenye mtaji mdogo), na benki maalum kama Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na kadhalika. Vilevile kuna mashirika ya uwekezaji na mikopo. Mashirika haya hushughulikia makundi ya watu maalum kama vile walimu, jeshi, wanawake, na kadhalika.

Ili mtu aweze kuwa mteja wa benki anapaswa kufungua akaunti. Akaunti hiyo inaweza kutumiwa kwa kuwekeza fedha au kuomba mkopo. Mteja akipewa mkopo na benki anaurudisha pamoja na riba. Lakini anapaswa kuwa na dhamana ili benki impatie mkopo.

Katika benki kuna wafanyakazi wengi na wenye nyadhifa tofauti. Kuna meneja, mwelekezaji, keshia, mhasibu, afisa mikopo na wengine wengi. Katika mazingira ya benki kunatumika karatasi mbalimbali kama risiti, vijitabu, hundi au hawala, hati ya kulipa na kadhalika. Usipotumia karatasi hizi unatumia kadi.

Kwa kifupi uwanja wa benki una msamiati mpana na uliotolewa ni baadhi yake.

**Maswali**

1. Taja majina matano ya benki za kibiashara za hapa Rwanda.
2. Taja majina mawili ya mashirika ya uwekezaji na mikopo.
3. Taja majina mawili ya karatasi zinazotumiwa benkini.
4. Tafuta maneno kumi yanayotumiwa katika mazingira ya benki kwenye mraba ufuatao:

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | E | S | H | I | A | N | S |
| M | E | N | E | J | A | E | T |
| M | T | S | O | P | K | N | A |
| R | H | A | I | H | A | O | K |
| A | I | U | J | I | U | S | A |
| D | L | B | N | I | N | I | B |
| I | M | P | A | D | T | R | A |
| N | U | N | U | A | I | I | D |
| D | H | A | M | A | N | A | H |
| M | H | A | S | I | B | U | I |

## 16.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 7

**Shirikiana na mwenzako msome kisha muigize mazungumzo kati ya Meneja wa benki na Mutesa hadharani.**

## 16.6. Kuandika

### KAZI YA 8

**Tunga matini fupi, ukitumia msamiati unaotumiwa benkini ukitilia mkazo kwenye matumizi tofauti ya kiambishi –ki-.**

# SOMO LA 17: REJESTA

## 17.1. Kusoma na ufahamu: Mchezo wa kusisimua

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya ufahamu**

Ilikuwa Jumapili majira ya alasiri wakati tuliposhuhudia mchezo mkali wa kandanda kati ya timu mbili hasimu ambazo ni Shule ya Kumekucha na Shule ya Mwanga. Mechi hiyo ilikuwa fainali ya kuwania tiketi ya kutinga katika mashindano ya michezo kati ya shule za Jumuia ya Afrika Mashariki kwa jina maarufu la FEASSA. Timu ya Shule ya Mwanga ndiyo iliyokuwa bingwa mtetezi. Mwaka jana timu hizi zilikutana tena kwenye hatua ya nusu fainali na Shule ya Mwanga ikaicharaza Shule ya Kumekucha mabao manne bila jibu.

Timu mbili zote zilijizatiti kwa maandalizi ya mechi, huku wachezaji wakiwa wakinolea na makochi wao mchana kutwa usiku kucha. Siku hii watu wote walikuwa wakisubiri mshindi wa mechi hii. Hayawi hayawi, huwa! Saa nane kamili timu mbili zilijitokeza uwanjani mara nyimbo za shule hizo mbili kuhinikizwa. Mashabiki wakaimba na kushangilia kwa vifijo na nderemo. **Kushangilia kwao** kulikuwa na maana kwa sababu timu hizi mbili zilikuwa na washambuliaji imara hasa timu ya Kumekucha. Wachezaji wote walisalimia mashabiki na waamuzi wa mchezo. Huku nao wakisalimiana. **Kusalimiana huku** kulikuwa ishara ya adabu katika mechi.

Kila timu ilikaa tayari na refa akapuliza kipenga mara mechi ikaanza. Wachezaji wa Kumekucha wakaonyesha mbwembwe za hapa na pale kwa kupeana pasi murua. Timu ya Mwanga ilikuwa ikilinda lango huku timu ya Kumekucha ikishambulia kama nyuki waliochokozwa. Kwenye dakika ya kumi mshambuliaji mahiri wa Kumekucha alinusa nyavu lakini kipa wa Mwanga akaugusa mpira kidogo ikawa kona. Kona ilipopigwa mshambuliaji wa Kumekucha alijibu kwa kichwa lakini mlindamlango akaudaka mpira. Kulipokaribia muda wa mapumuziko mshambuliaji wa Mwanga alitoa kombora kuelekea lango la Kumekucha mpira ukagonga mwamba, kipa akaumia kwa sababu alipiga kichwa chake kwenye lango akitaka kuliokoa jahazi lake. Mashabiki walianza kusema “Leo ni leo…” **Kuumia kwake** kuliifanya mechi kusimama kwa dakika tano. Hadi mapumuziko, mechi ilikuwa bila kwa bila.

Kipindi cha pili kilipoanza mchezaji wa Mwanga alipiga chenga za hapa na pale na refa akala mchanga. Mashabiki wote wakashika mbavu zao kwa vicheko. Refarii alipoinuka alimwonyesha kadi ya manjano mchezaji huyu. Mashabiki wakaanza kumzomea mwamuzi.

Kwenye dakika ya themanini mchezaji wa Kumekucha aliubabatiza mpira akapiga krosi kuelekeza kwa mwenzake katika boksi lakini kwa bahati mbaya kibendela kikainuliwa. Alikuwa ameotea. Timu ya Mwanga ilijibu mashambulizi hayo viungo wakiwa wakipeana pasi na kusukuma mpira kwa washambuliaji lakini mechi ikaendelea kuwa sare ya kutofungana.

Katika dakika za lala salama, mshambuliaji wa timu ya Mwanga alipiga chenga katika eneo la hatari la timu ya Kumekucha akachezewa rafu. Mashabiki wote nyoyo zikawadunda. Kwa upande wa kushoto kibendera kilikuwa juu. Refarii hakutambua jambo. Bila ya kuchelewa aliendа kuchunguza kwenye “VAR”. Alichunguza na kuchunguza. Kimya kikubwa kilitawala uwanja mzima. Refa aliamua kuwa kulikuwa hakuna penalti. Wachezaji wa Mwanga walianza kuzozana na nahodha wao akatolewa nje kwa kuonyeshwa kadi nyekundu. Kuona hayo mashabiki waliingia uwanjani na askari polisi wakafanya kazi yao. Wengine walikuwa wakirusharusha chupa za kuwekea maji na juisi. Wengi walikuwa wakijiuliza “**Kuamua huku** ni **kupi**?”

Mzozo ulipotatuliwa refa wa nne alinyanyua ubao na kuonyesha dakika tano za majeruhi. Kumekucha wakashambulia na kushambulia. **Kushambulia kwenyewe** kulikuwa na maana kwa kuwa wao walikuwa na idadi kamili lakini Mwanga walikuwa kumi. Pengo la kumkosa beki machachari liliwakera sana Mwanga. Wakati huu timu nzima ilikuwa imerudi nyuma kuzuia mashambulizi. Hauchi hauchi unakucha. kabla ya sekunde mbili mechi kumalizika mshambuliaji wa Kumekucha alipiga shuti kali na mpira ukaingia kimya. Nyavu zikatikisika. Mashabiki wa Mwanga wakainuka na kuanza kumrushia mchezaji huyu noti. Wachezaji waliporudi uwanjani kipenga cha mwisho kilipulizwa. Kumekucha wakatoka kidali kwa ushindi wao wa bao moja kwa nunge. Wachezaji wa Mwanga waliangua vilio na wengine wakigaragara uwanjani.

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Mechi hii ilikutanisha timu gani?
2. Mchezo huu ulikuwa kwenye hatua gani?
3. Matokeo ya mchezo ni yapi?
4. Kwa sababu gani mashabiki walirusha chupa za kuwekea maji uwanjani?
5. Mchezaji aliyeonyeshwa kadi nyekundu alikuwa akichezea kwenye nafasi gani?
6. “Hauchi hauchi unakucha” Sentensi kama hizi huitwaje katika lugha ya Kiswahili?

## 17.2. Msamiati kuhusu kifungu cha habari

### KAZI YA 2

**Toa maana za maneno yafuatayo:**

1. Vifijo
2. Nderemo
3. Kipenga
4. Krosi
5. Beki

### KAZI YA 3

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Kubabatiza
2. Kugaragara
3. Nyavu
4. Kunusa
5. Kushika mbavu

## 17.3. Sarufi: Matumizi ya majina ya ngeli ya ku-na vivumishi vyake

### KAZI YA 4

**Soma upya kifungu cha habari kisha uchunguze matumizi ya maneno yenye wino uliokolea ili uweze kuyatumia katika tungo zako mwenyewe.**

### Maelezo muhimu

Vifungu vya maneno yaliyokolea katika kifungu cha habari hapo juu ni majina ya ngeli ya **KU**- pamoja na vivumishi vyake. Majina hayo huitwa **vitenzijina**; yaani vitenzi vilivyotumiwa kama majina. Majina ya aina hii hayana wingi na hutumia kiambishi **ku-**.

**Matumizi ya vivumishi katika ngeli ya KU-**

- **Vivumishi vya kuonyesha**

- Kuimba **huku/huko/kule** kunapendeza.
- Kuamua **huku/huko/kule** kunasikitisha.

- Kusoma **huku/huko/kule** kutawasaidia maishani.

- **Vivumishi vya kumiliki**
- Kucheza **kwangu/kwetu** kunapendeza.
- Kulia **kwako/kwenu** kulisikitisha wengi.
- Kuombaomba **kwake/kwao** si tabia nzuri.

- **Vivumishi vya sifa**
- Kulala **kuzuri** ni kulala mahali pema.
- Kula **kubaya** kunaletea mwili wako madhara.

- **Vivumishi vya idadi/ kiasi**
- Kuishi **kwingi** kuona mengi.

- **Vivumishi vya kurejesha**
- Kuimba **kokote** kunavutia.
- Kucheza **kwenyewe** kulitufurahisha.
- Kula **kwenye** manufaa ni kula virutubisho.

- **Vivumishi ya kuunganisha**
- Kulia **kwa** mtoto yule kulisikitisha wengi.
- Kucheza **kwa** timu yetu hakupendezi siku hizi.

- **Vivumishi vya kuuliza**
- Ni kuimba **kupi/gani** kunakokuvutia?
- Mnapendekeza kula **kupi/gani**?

### KAZI YA 5

**Andika sentensi kumi zinazobainisha matumizi ya ngeli ya ku-pamoja na vivumishi vyake.**

## 17.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu rejesta

### KAZI YA 6

**Soma upya kifungu cha habari uchunguze namna lugha ya Kiswahili ilivyotumiwa kisha usome maelezo muhimu kusu rejesta.**

- Lugha iliyotumiwa inaitwaje?

**Rejesta**

Rejesta au sajili ni mtindo wa lugha inayotumiwa mahali au katika hali fulani na wala haiwezi kuhamishwa kutoka mazingira yale na kutumiwa mahali pengine. Lugha za aina hizi hutofautiana kwa misingi ya msamiati, muundo wa sentensi na kadhalika.

Kutokana na mambo haya, kuna rejesta za aina mbalimbali. Baadhi ya rejesta hizo ni kama hizi zifuatazo:

**i. Rejesta ya mpirani**

| Rejesta | Maelezo |
|---|---|
| **Kunawa mpira** | Kugusa mpira kwa mkono |
| **Kucheza rafu** | Kufanya kosa mchezoni |
| Gozi | Mpira |
| **Refa/refarii** | Mwamuzi |
| Mpira kuwa mwingi | Mpira kutoka nje ya uwanja |
| Fainali | Mchezo wa mwisho |
| Nusu fainali | Hatua ya mchezo inayotangulia mchezo wa mwisho |
| Kombe | Kikombe kilichotengenezwa kwa madini na kupewa washindi |
| Medali | Kitu cha madini kitolewacho kama tuzo kwa mshindi |
| Mchuano | Shindano |

**ii. Rejesta ya baa/mgahawa/hoteli**

| Rejesta | Maelezo |
|---|---|
| **Mshikaki** | Nyama iliyokatwa vipandevipande na kuchomekwa katika kijiti au chuma na kuchomwa. |
| **Pilau** | Wali uliopikwa kwa kuchanganya viungo pamoja na kitoweo (nyama au samaki) |
| **Nyamachoma** | Nyama iliyochomwa. |
| **Biriani** | Wali uliokaangwa na kuchanganywa na nyama iliyokaangwa na masala. |
| **Chupa** | Kinywaji kinachokuwa chupani |
| **Kidali** | Kifua cha mnyama |
| **Kongoro** | Mguu wa mnyama |

iii. **Rejesta ya benkini**

| Rejesta | Maelezo |
| --- | --- |
| **Mtaji** | Mali inayotumiwa kuanzisha au kupanulia biashara |
| **Deni** | Mkopo |
| **Meneja** | Kiongozi wa tawi la benki |
| **Kuwekeza** | Kutumia mali au fedha katika biashara kwa lengo la kuzalisha zaidi. |
| **Keshia** | Mhudumu wa benki anayepokea na kutoa fedha |

iv. **Rejesta ya mahakamani**

| Rejesta | Maelezo |
| --- | --- |
| **Mahakama** | Mahali ambapo kesi na mashtaka husikilizwa na kuamuliwa. |
| **Kesi** | Mashtaka yanayosikilizwa mahakamani |
| **Kukata rufaa** | Kuomba kesi isikilizwe upya |
| **Faini** | Fedha anazotozwa mwenye hatia kuwa ni adhabu |
| **Kizimba** | Mahali anaposimama mshitakiwa mahakamani |
| **Wakili** | Mtu anayesaidia mshitakiwa kujibu kwa mashtaka mahakamani |

### KAZI YA 7

**Soma sentensi zifuatazo kisha ueleze mahali ambapo lugha hiyo hutumiwa:**

1. Mheshimiwa spika, sheria hii imekiuka katiba ya nchi yetu.
2. Bei rahisi...bei imeshuka. Njoo mteja! Njoo mteja! Usitembee kwa miguu mitupu! Nunua viatu kabla ya bei kupanda!
3. Katika jina la Baba na la Mwana na Roho Mtakatifu. Amina.

## 17.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 8

**Shirikiana na mwenzako kwa kutunga mazungumzo yenye rejesta fulani kisha muigize mbele za wenzenu darasani.**

## 17.6. Kuandika

### KAZI YA 9

**Tunga matini ndogo kuhusu rejesta fulani ukitilia mkazo kwenye matumizi ya ngeli ya ku-.**

### TATHMINI YA MADA YA NANE

1. Taja majina matano ya benki za kibiashara za hapa Rwanda.
2. Taja majina mawili ya mashirika ya uwekezaji na mikopo ya hapa Rwanda.
3. Rejesta ni nini?
4. Rejesta hii hutumiwa wapi?
   - "Kwa jina la Bwana, la Mwana na Roho Mtakatifu"
   - "Mheshimiwa spika, mimi sikubaliani na sheria hiyo hata kamwe"
5. Kanusha sentensi zifuatazo:
   - Ukisoma vizuri utashinda mtihani.
   - Tulimkuta akisafisha chumba chake.
   - Akifika mniamshe.
   - Mtoto alinyolewa akilia.
6. Andika sentensi kumi zenye majina ya ngeli ya **KU**- ambapo sentensi tano zitatolewa katika tungo yakinishi na nyingine tano katika tungo kanushi.

# MADA 9

# KISWAHILI NA TEKNOLOJIA

## Uwezo mahususi

Kutumia kwa ufasaha msamiati maalumu katika uwanja wa teknolojia

**Malengo ya ujifunzaji:**


- Kutumia kwa ufasaha msamiati wa teknolojia ya habari na mawasiliano
- Kueleza msamiati maalumu unaotumiwa katika mawasiliano ya kiteknolojia
- Kutunga matini fupi kwa kutumia msamiati wa teknolojia ya habari na mawasiliano
- Kutumia kwa usahihi viambishi vya masharti -nge-,-ngeli- na -ngali-
















## KIDOKEZO

Chunguza michoro ya hapa juu na kueleza inachokihusu.

# SOMO LA 18. MATUMIZI YA TARAKILISHI NA VYOMBO VYA HABARI

## 18.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi ya tarakilishi





**Soma kifungu cha habari hapa chini na kujibu maswali ya ufahamu yanayofuata.**

Mapendekezo ya kuwa na mradi wa tarakilishi kwa kila mtoto nchini Rwanda yana umuhimu mkubwa sana kwa elimu ya watoto wanaosoma. Mradi huu utawawezesha watoto kupata ujuzi wa kiteknolojia. Watoto wengi watafahamu maana ya tarakilishi, matumizi yake na faida zake katika elimu yao. Watoto wataweza kupata majibu ya maswali yao mengi kupitia kwa mtandao. Itakuwa rahisi kupata maana ya maneno, maelezo na taarifa muhimu kuhusu mada yoyote wanayofundishwa kwa kutumia tarakilishi.

Tarakilishi huwa na kamusi ya msamiati mbalimbali, maelezo na istilahi ambazo ni rahisi kupata kwa haraka. Mtandao umeufanya ulimwengu kuwa kama kijiji kidogo. Kupitia kwa tarakilishi, ni rahisi kuelewa utamaduni wa wanajamii wengine na pia kushirikiana na kutangamana nao. Hii ni kwa sababu watu wanaweza kutafuta habari muhimu kutoka kwenye mitandao kuhusu lugha, mavazi, vyakula na sherehe za watu na jamii nyingine.

Matumizi ya tarakilishi yamechangia katika kuyatunza mazingira yetu kwa kupunguza matumizi ya karatasi nyingi. Jambo hili limechangia katika kupunguza ukataji ovyo wa miti ambao ndicho chanzo cha kuharibu misitu yetu. Rwanda ni miongoni mwa nchi safi sana duniani kutokana na matumizi haba ya karatasi na sandarusi. Kupitia kwa tarakilishi, kiwango cha masomo kimeimarika sana. Watu wengi hasa wanafunzi wanaweza kujisomea kwa kufanya utafiti wao wenyewe na kufanya mazoezi mbalimbali kwenye mtandao.

Katika kuwezesha mawasiliano, kuna matumizi ya fesibuku na watisapu ambayo yanapendwa sana na vijana. Fesibuku ni huduma ya kutuma na kupokea taarifa pamoja na picha ama video. Fesibuku ina faida nyingi: mtu anaweza kutuma na kupokea picha, video na hata nyimbo, majibu yake ni ya haraka, unaweza kutangaza bidhaa pale na kupata wanunuzi kwa haraka, taarifa husambazwa kwa haraka, ni njia rahisi ya kuhifadhi taarifa mbalimbali n. k. Hata hivyo, Fesibuku ina madhara yake kwani inaweza kuwafedhehesha wazazi na watoto ama wafanyakazi na waajiri wao kwa kusambaza habari zisizofaa kwa wanajamii. Mara nyingi, watu husambaza taarifa chafu pamoja na picha chafu zikiwemo za watu walio uchi ama wanaofanya uhalifu. Isitoshe, wahalifu na walanguzi wa dawa za kulevya huutumia mtandao wa fesibuku kuuza dawa za kulevya na kusambaza habari za ugaidi. Watu wengi wamelaghaiwa pesa na hata wengine hasa wanawake kuuawa na watu waliopatana nao tu kwenye fesibuku.

Watisapu ni huduma iliyo ndani ya simu au tarakilishi kwa njia ya mtandao ambapo mtu anaweza kupokea na kutuma taarifa, kupigia simu, kutuma na kupokea nyimbo, picha na video. Upungufu mkubwa wa watisapu ni kwamba bila ya kuwa na simu au tarakilishi iliyowezeshwa, huwezi kupokea huduma hii. Isitoshe, watisapu ina gharama ya juu kwani lazima ununue bandali za intaneti ili uweze kufaidika nayo au kuitumia. Hata hivyo, elimu, uchumi na jamii imeathirika kutokana na matumizi ya watisapu. Baadhi ya vijana wa shule na wafanyakazi hupoteza muda mwingi wakiwasiliana na wenzao na kwa hivyo kupoteza muda mwingi wa masomo ama kazi.

Baruapepe ni ujumbe unaotumwa kwa njia ya kielektroni kupitia kwa tarakilishi au simu ya mkononi iliyounganishwa kwenye mtandao. Kwa ujumla, barua pepe huwa ni njia ya haraka ya kupata ujumbe na kupokea majibu. Huhifadhi wakati na ni nafuu kuliko kuandika barua ya kawaida. Upungufu wake mkubwa ni kwamba, bila kuwa na mtandao ni njia isiyowezekana kutumika. Isitoshe inahitaji umeme. Pia, sharti mwenye kutuma na kupokea ujumbe awe na anwani, kwa mfano: **kiswahili@gmail.com** ama **kiswahili@ yahoo.com.**

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja faida zozote mbili za mradi wa tarakilishi kwa wanafunzi.
2. Taja faida zozote mbili za tarakilishi kwa watu kwa ujumla.
3. Jina jingine la tarakilishi ni lipi?
4. Mtandao hufanya ulimwengu kuwa kama kijiji kimoja. Kweli au la? Kivipi? Eleza.

5. Jadili upungufu mkubwa wa watisapu kulingana na kifungu ulichosoma.
6. Pendekeza anwani nyingine mwafaka kwa taarifa hii.
7. Je, teknolojia ina manufaa gani kwa nchi? Taja manufaa matano
8. Eleza madhara yanayoweza kusababishwa na tarakilishi.
9. Matumizi ya tarakilishi yanawezesha vipi utangamano wa wanajamii mbalimbali?
10. Jadili matumizi, umuhimu na madhara ya:

    a) Fesibuku b) Watisapu c) Baruapepe:

## 18.2. Msamiati kuhusu matumizi ya tarakilishi

### KAZI YA 2

**Toa maana ya msamiati ufuatao:**

a. Mradi
b. Utamaduni
c. Sandarusi
d. Mawasiliano
e. madhara
f. Ugaidi
g. Tarakilishi
h. barua pepe
i. Mtandao

### KAZI YA 3

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo:** watisapu, barua pepe, bandali, mtandao, ujumbe, simu, fesibuku, tarakilishi, kusambaza.

## 18.3. Sarufi: Viambishi vya masharti -nge- na -ngali-

### KAZI YA 4

**Soma sentensi hizi, kisha eleza maana zake na matumizi ya viambishi vya masharti -nge- na -ngali-**

a. Ningekuwa na pesa ningenunua simu.
b. Ningefahamu lugha ya Kiswahili ningetembelea Kenya au Tanzania.
c. Angalifika shuleni mapema angalifanya jaribio la Kiswahili.

### Maelezo muhimu

**-Nge**-na-**ngali** hutumiwa kuonyesha uwezekano au majuto. Kitendo fulani hakikutokea kwa sababu ya kitendo au hali nyingine ambayo haikutimilika. Kwa kifupi, kuna vitendo au hali mbili zinazotegemeana; kwa hivyo tendo au hali ya kwanza ikitokea kuna uwezekano wa kitendo cha pili kufanyika. Ni kosa la kisarufi kuchanganya -NGE- na -NGALI- katika sentensi moja. Ikiwa kipande cha kwanza kimetumia -NGE-, tumia -NGE- katika kipande cha pili, n.k.

**a. Matumizi ya -NGE-**

**-NGE-** hutumika kuonyesha kwamba kitendo fulani hakijafanyika na kwa hivyo jambo fulani halijatokea lakini kuna uwezekano wa kufanya kitendo hicho na jambo hilo litokee.

**Kwa mfano**: -Ni**ng**ekuwa na pesa nyingi ni**nge**safiri ulimwenguni kote→ Sina pesa wala sisafiri ulimwenguni kote, lakini nikipata pesa saa hii, ninaweza kusafiri ulimwenguni kote.

**b. Matumizi ya -NGALI-**

**-NGALI-** hutumika kuonyesha kwamba kitendo fulani hakijafanyika na kwa hivyo jambo fulani halijatokea wala hakuna uwezekano wa kufanya kitendo hicho. Hutumika hasa kuonyesha majuto.

**Kwa mfano:** -Ningalifika nyumbani mapema ningalimkuta baba yangu nyumbani→ Sikufika nyumbani mapema, hivyo basi sikumpata, wala siwezi kumpata kwani nishachelewa naye ashaondoka.

Kukanusha -**NGE-** na -**NGALI-**

Tunapokanusha **-NGE-** na **-NGALI-,** tunamaanisha kwamba kitendo cha pili kilifanyika tu kwa sababu kitendo cha kwanza kilikuwa kimefanyika. Kama jambo la kwanza halikutendeka, jambo la pili halingetokea. Tunakanusha kwa kuongeza kiungo “si” yaani “-NGE-”→-SINGE- na “-NGALI-”→-SINGALI-.

**Mifano ya ukanushaji:**

| SENTENSI YAKINISHI | SENTENSI KANUSHI |
|---|---|
| Kagina angeiba, angekamatwa. | Kagina asingeiba asingekamatwa. |
| Ningeshindwa mtihani , ningefukuzwa mwishoni mwa mwaka huu. | Nisingeshindwa mtihani, nsingefukuzwa mwishoni mwa mwaka huu. |
| Tungalitoroka shuleni tungaliadhibiwa na mwalimu wa nidhamu. | Tusingalilitoroka shuleni tusingaliadhibiwa na mwalimu wa nidhamu. |
| Ingalinyesha kwa wakati mwafaka tungalivuna mavuno ya kutosha. | Isingalinyesha kwa wakati mwafaka tusingalivuna mavuno ya kutosha. |

## KAZI YA 5

**Kanusha sentensi zifuatazo:**

a. Tungalienda hospitalini, tungalitibiwa.
b. Tungelima shamba letu lote, tungepata mavuno mengi.
c. Angekuwa mwerevu shuleni, angeshinda masomo yote.
d. Ungaliomba msamaha, ungalisamehewa.
e. Ungaliparamia mti, ungalianguka.
f. Ungeiba, ungekamatwa na kuadhibiwa.


## 18.4. Matumizi ya lugha: Mawasiliano ya kiteknolojia

## KAZI YA 6

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo: akaunti, mtandao, kadi sakima, kadiwia, kipakatalishi, diski mweko, mtaliga.**

## KAZI YA 7

**Tazama michoro hapo chini ili ujadili umuhimu wa redio na runinga kwa jamii.**





## KAZI YA 8

**Soma kifungu kifuatacho na kujibu maswali yanayoambatana nacho:**

Redio na runinga ni baadhi ya vyombo vinavyotumiwa kupasha habari kwa wananchi. Vyombo hivi huwasaidia kupata habari zinazohusu masuala ya uongozi, kilimo, elimu, biashara, jamii na utamaduni wake, uchumi, michezo, siasa pamoja na habari za kimataifa. Habari hizi hutangazwa kwa kurushwa hewani. Anayerusha habari kupitia vyombo hivi huitwa mtangazaji.

Vyombo hivi vya habari vina umuhimu sana kwani hutusaidia kupata *matangazo* mbalimbali kama vile: matangazo ya kibiashara, taarifa za habari, matangazo ya mpira, matangazo ya kielimu, taarifa za kisiasa, habari kuhusu uchumi wa nchi, matangazo ya tanzia (vifo) na kadhalika. Umuhimu wa redio na runinga hauishii tu katika kutangza habari, bali pia huchangia katika kuburudisha jamii. Mtu anaweza kutazama michezo kupitia runinga au akasikiliza michezo mbalimbali kupitia redio.

Aidha, jamii inaweza kupata fursa ya kujifunza utamaduni wao na utamaduni wa nchi nyingine, kujifunza lugha na fasihi kupitia redio au televisheni yaani runinga. Kama ilivyo katika Nyanja nyingine za kazi, vyombo vya habari hivi hutumia wafanyakazi tofauti ili kupasha habari kwa jamii. Wafanyakazi hao ni kama vile: Mkurugenzi wa runinga au redio anayehusika na mpangilio, sera na utaratibu unaofaa wa kuandaa na kurusha matangazo hewani, Mhariri anayetayarisha habari zote muhimu ambazo zinafaa kupeperushwa hewani na namna zitakavyopeperushwa, mtangazaji ambaye hutangaza habari kwenye redio na/au kwenye runinga ili zimfikie msikilizaji au mtazamaji wa runinga. Msikilizaji na mtazamaji ndiyo hadhira inayopokea ujumbe kwa kusikiliza na/au kutazama kulingana na kituo cha utangazaji kinachohusika.

Ingawa vyombo vya habari vina umuhimu mkubwa kwa jamii, kuna wakati ambapo vinaweza kusababisha madhara ikiwa wafanyakazi wake wanatangaza ama kupeperusha habari zilizo potovu. Baadhi ya madhara hayo yanaweza kuwaathiri watu wazima na hata watoto kwa njia moja au nyingine. Watoto huweza kutazama miziki na filamu chafu kwenye runinga na hivyo kuathiri maadili yao.

Watu wengi huiga mvao na mitindo ya wanamiziki, na waigizaji kwenye runinga. Redio au runinga zinaweza kupeperusha habari za ubaguzi ambazo zinaweza kuchochea uhasama kati ya wanajamii husika. Hili huweza kuathiri maadili ya kijamii.

Kwa hiyo, ni jambo muhimu kwa wafanyakazi kwenye kituo cha utangazaji habari kuwa makini na kutangaza habari zinazofaa kwa jamii. Wasikilizaji au watazamaji wanatakiwa pia kuwa makini na kuchunguza ikiwa habari zinazotangazwa zina manufaa kwao ili kujiepusha na madhara yanayoweza kusababishwa na habari zilizo potovu.

**Maswali ya ufahamu:**

1. Eleza umuhimu wa redio na runinga kwa jamii.
2. Taja mifano ya matangazo yanayotangazwa kupitia redio na runinga.
3. Eleza madhara ya redio na runinga kwa jamii.
4. Taja angalau vituo 5 vya redio na runinga vinavyopeperusha habari nchini Rwanda.
5. Jamii inashauriwa nini kuhusu habari potovu zinazopeperushwa kupitia kwa redio au runinga?

## KAZI YA 9

**Tunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati ufuatao:** (a) mskilizaji, (b) mtangazaji, (c) runinga, (d) redio, (e) kusikiliza, (f) kutazama.

- **Msamiati zaidi kuhusu teknolojia**

- **Diski mweko:** Ni kifaa au diski inayotumiwa kuhifadhi maandishi kutoka kompyuta na kuyapeleka ili kuhifadhiwa katika kompyuta nyingine au kuyapiga chapa.
- **Kadi sakima**: Ni kadi ndogo sana iwekwayo ndani ya simu kuhifadhia muziki, picha na faili tofauti.
- **Kadiwia/mkamimo**: Ni kadi ndogo iwekwayo ndani ya simu kuhifadhia majina na simu za watu.
- **Kinukuzi**: Ni mashine ambayo hurudufu nakala mbalimbali
- **Kipakatalishi**: Ni aina ya kompyuta ndogo mtu anayoweza kutembea nayo kikapuni.
- **Mdaki**: Ni kifaa cha kiteknolojia ambacho hutumiwa kupiga picha.
- **Mtaliga**: Ni aina ya ugonjwa wa kiteknolojia utumiwao kuangamiza kompyuta mbalimbali.

## 18.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

## KAZI YA 10

a. **Jadili umuhimu wa kutumia tarakilishi kwa wanafunzi.**
b. **Andaa taarifa ya Kiswahili na kuitangaza mbele ya darasa**

## 18.6. Kuandika

## KAZI YA 11

**Andika kifungu cha habari kisichozidi maneno mia moja kuhusu maendeleo ya kiteknolojia katika uwanja wa elimu nchini Rwanda.**

# SOMO LA 19. MATUMIZI YA SIMU YA MKONONI










## KAZI YA 1

**Tazama michoro ya hapo juu na kueleza aina ya vifaa vilivyopo na umuhimu wake.**

## 19.1. Kusoma na ufahamu: Matumizi ya simu ya mkononi

**Baba:** (*Akiingia sebuleni*) Habari za mchana mke wangu?

**Mama:** Njema mume wangu. Karibu! Hii simu imenisumbua sana leo. Tangu nilipoipokea sijafahamu matumizi yake hadi sasa.

**Baba:** Simu imefanya nini? Tafadhali nieleze. Mambo ya teknolojia haya mke wangu!

**Mama:** Wajua simu hii bado ni mpya na sijajua jinsi ya kuitumia vyema! Simu hii ya kugusa badala ya kubofya vidude...

**Baba:** Enh? Simu uliyonunuliwa na mwanao huko mjini Kigali? Usiwe na hofu, utajua matumizi yake polepole.

**Mama:** Asante sana. Jana nimemwandikia mwana wetu huyo…. Nikamweleza kuwa nimepokea simu…sikumweleza kuwa simu hii mpya inanitatiza kimatumizi (*akicheka*).

**Baba:** Ulifanya vyema sana. Hata hivyo, ingekuwa bora sana kama ungempigia simu badala ya arafa.

**Mama:** Mume wangu kwani unafikiri hata kuandika arafa hiyo ilikuwa kazi rahisi? Ilinitatiza sana. Unajua simu hii siyo ya kubofya ni ile ya kugusa tu halafu inakupa dunia nzima ya mambo!

**Baba:** (*Akicheka)* Yapi tena? Pole kwa kutatizika. Huku kijijini bado tuko nyuma sana kimaendeleo na kiteknolojia.

**Mama:** Sijui kamera, instagramu, fesibuku, Biblia, kamusi… mengi (*akicheka*).

**Baba:** Naona mawasiliano yatakuimarikia kwa simu mpya uliyonunuliwa.

**Mama:** Nashukuru! Binti yangu amenieleza kuwa bila intaneti mtu hawezi kusoma habari za fesibuku wala watisapu.

**Baba:** Hayo ni kweli kabisa. Kakwambia nini tena?

**Mama:** Simu hii inahitaji chaji nyingi ili isizime. Pia, nilielezwa kuwa kutumia watisapu, kusoma habari za mtandaoni pamoja na matumizi mengine yanahitaji hela nyingi.

**Baba:** (*Akiinamisha kichwa.*) Hayo uliyoambiwa ni kweli. Tatizo jingine ni kuwa aina hii ya simu ikianguka chini inaweza kupasuka skrini yake haraka sana hivyo kuharibika na isitumike tena.

**Mama:** Licha ya matatizo hayo mengi, nafurahia tu kupata simu hii kwa sababu ninaweza kufanya mambo mengi nayo. Naweza kupiga picha na hata kusoma taarifa za kiulimwengu.

**Baba:** Hali itakuwa shwari baada ya kuitumia kwa muda. Utaweza kuyafanya mambo mengi zaidi.

**Mama:** Kweli mume wangu. Tatizo jingine ni kwamba aina hii ya simu inafaa kutumika na walioelimika sana. Sisi wazee zinatutatiza!

**Baba:** Lakini sharti twende na wakati. Hii ni dunia ya teknolojia. Nasi tunapaswa kufuata yanayotukia huku na kule!

**Mama:** Nakubaliana nawe. Sharti tujikakamue.

**Baba:** Kweli (*wanaingia ndani ya nyumba*).

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja wazungumzaji katika kifungu cha mazungumzo ulichosoma hapo juu.
2. Bila shaka mazungumzo yenyewe yanahusiana na teknolojia. Kwa nini? Eleza.
3. Taja chombo cha mawasiliano kilichozungumziwa.
4. Orodhesha matumizi yoyote mawili ya chombo kilichozungumziwa.
5. Mama ana matatizo gani kuhusiana na simu yake mpya?
6. Kulingana na baba, ni nini kinachoweza kutokea na kuathiri matumizi ya simu ya mkononi?
7. Teknolojia ni nini? Eleza kwa maneno yako mwenyewe.

## 19.2. Msamiati kuhusu matumizi ya simu ya mkononi

## KAZI YA 3

**Oanisha msamiati katika sehemu A na maana zake katika sehemu B**

| SEHEMU A | SEHEMU B |
|---|---|
| Arafa | Njia ambayo wenyeji au taifa hufanya mambo kuwa ya kimataifa; kufanya mambo pamoja duniani. |
| Simu ya mkononi | Ujumbe unaotuma kwa njia ya intaneti au mtandao mwingine wa kielektroniki. |
| Utandawazi | Ujumbe mfupi wa maandishi unaotumwa na kupokewa; kwa mfano katika simu. |
| Teknolojia | Simu inayofanya kazi kwa mfumo wa kielektroniki ambayo hupata mawasiliano kwa njia ya mawimbi, pia mtu huweza kwenda nayo popote anapotaka. |
| Barua pepe | Maarifa ya sayansi yaliyowekwa katika matumizi ya vitu k.v. zana au mitambo katika k.v. kiwanda, kilimo, ufundi au mawasiliano. |

## KAZI YA 4

**Tunga sentensi kwa kutumia msamiati ufuatao: kubofya vidude, kugusa, kamera, simu ya mkononi, kiwambo, intaneti, chaji, arafa.**

## 19.3. Sarufi: Kiambishi cha masharti -ngeli-

## KAZI YA 5

**Jadili kuhusu maana za sentensi zifuatazo zenye kiambishi -ngeli-:**

- Tungelisoma kwa bidii tungelishinda mitihani iliyoandaliwa na taifa.
- Wangelinipa mshahara wangu ningelinunua gari jipya.

### Maelezo muhimu

Kama viambishi -nge- na -ngali- tulivyoona hapo katika somo lililotangulia somo hili, kiambishi –ngeli- huonyesha masharti yasiyowezekana katika hali yakinishi. Katika hali kanushi kikanushi -si- huongezewa na kufuatwa na -ngeli-.

**Mfano:**

- Usingelinijulisha habari nisingelihudhuria mkutano wa Kata.
- Wasingelienda sokoni wasingelinunua nguo zile.
- Tusingeliandika vitabu vya Kiswahili tusingelipata vitabu vya kufundishia.

## KAZI YA 6

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viambishi -nge-, -ngeli- na -ngali-.**

a. Usingelikuwa mwerevu shuleni ……………………………………………
b. Ningelipokea ujumbe kuhusu mkutano wa viranja wote ………………
c. Wangelitunza vizuri mazingira ……………………………………………
d. Tungelipanda miti milimani ………………………………………………
e. Nisingelikuwa mfanyabiashara ……………………………………………
f. Usingelikuwa na uzembe ……………………………………………………
g. Angelikuwa na cheti cha udereva …………………………………………
h. Asingeliumwa malaria ………………………………………………………

## 19.4. Matumizi ya lugha: Matumizi ya simu ya mkononi

### KAZI YA 7

**Chagua neno linalofaa kati ya haya yafuatayo na kujaza kifungu cha habari kinachofuata:** simu ya mkononi, kadiwia, ujumbe, kamera, kubofya, fesibuku, zilizotengenezwa, arafa, kiteknolojia, madhara.

Teknolojia ya habari na mawasiliano ilipiga hatua sana kimaendeleo. Zamani za kale wazazi wetu walikuwa hawawezi kupashana habari mara kwa mara bila ya kutembelea rafiki zao na kuwapelekea …………………… kwa njia ya usafiri. Mara nyingi watu walikuwa wakilalamikia familia zao kwa sababu ya kufanya harusi, kuita mtoto jina, n.k bila ya kuwapasha habari.

Matumizi ya ………………………..yalipoanza, watu walianza kufurahia maendeleo haya kwani mawasiliano yalikuwa rahisi baina ya familia na wanamemba wao. Iliwabidi tu kununua simu ya mkononi na ……………..ili kuhifadhia majina ya watu na simu za watu.

Mwanzoni, simu zilizokuwepo ni zile za …….. vidude lakini jinsi maendeleo yalivyozidi kwenda kwa kasi simu za mkononi ………….. hutumiwa kwa kugusa skrini.

Simu hizi zina umuhimu sana kwani zina ………. nzuri zinazotumiwa kupigia picha na kuzituma kwa watu wengine wakiwa wanahitaji picha hizo. Simu hizi zilirahisisha siyo tu mawasiliano ya kifamilia bali pia mawasiliano ya kibiashara kwani mfanyabiashara anaweza kutangaza bidhaa zake kupitia simu hizi akipiga picha bidhaa zake na kuwatumia wateja wake picha za bidhaa anazoziuza.

Ingawa simu hizi ni muhimu lakini hutumia …………………za intaneti ili uweze kutumia watisapu, ……………………, na kutuma baruapepe au …………………………….

Ili kulinda watoto hasa hasa wanafunzi kupotoshwa na matumizi ya simu za mkononi, wazazi hushauriwa kufundisha watoto wao umuhimu wa kutumia vyombo hivi vya …………………… na kuwatahadharisha kuhusu ……………… yanayoweza kusababishwa matumizi yake mabaya.

## 19.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu matumizi ya simu

### KAZI YA 8

**Jadili kuhusu madhara ya kutumia simu ya mkononi kwa wanafunzi shuleni.**

## 19.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

### KAZI YA 9

**Katika ukurasa mmoja, tunga kifungu cha habari kuhusu umuhimu wa simu ya mkononi.**

### TATHMINI YA MADA YA TISA

1. Taja faida 4 za kutumia redio na runinga.
2. Taja wafanyakazi muhimu wanaopatikana kwenye kituo cha redio au runinga.
3. Tunga sentensi tano kwa kutumia viambishi vya masharti -nge-, -ngeli- na -ngali- katika tungo kanushi.
4. Jadili madhara ya kutumia tarakilishi.
5. Kamilisha kifungu cha habari kifuatacho kwa kuchagua neno linalofaa kati ya maneno yafuatayo: *mawasiliano, kupigia, watisapu, kuhudumia, umma, kuzima, wanapoendesha*.

Simu ya mkononi ni muhimu sana katika (1)..........................ya kijamii. Mtu akiwa mbali na familia yake anaweza (2)...................... simu mzazi wake au ndugu yake ili kumjulisha hali yake ya maisha.

Katika biashara, kifaa hiki hutumiwa kuonyesha wateja bidhaa zinazouzwa kwa kutumia (3)...................ambayo ina uwezo wa kutuma picha zinazohusu chochote kinachohitajika kutangazwa.

Watu wengi hupenda kutumia simu za mkononi bila ya kutilia maanani mahali walipo. Utawaona watu wanaotumia watisapu wakiwa kazini katika shughuli zao wenyewe na kushindwa (4)..................wateja wao vilivyo.

Baada ya kuona kwamba matumizi ya simu ya mkononi yanaweza kuzorotesha maendeleo ya taasisi tofauti na kuweza kusababisha ajali kwa njia moja au nyingine, kumetolewa maagizo yafuatayo: Kwanza, inakatazwa kuzungumza kwa sauti ya juu unapozungumza kwa simu ya mkononi ukiwa katika maeneo ya (5)………………… Pili, inashauriwa (6)…………………simu ya mkononi au kutumia mfumo wa kutetema badala ya kutoa mlio unapokuwa kwenye mkutano, kanisani, msikitini, n.k.

Tatu, madereva nao wanashauriwa kutotumia simu ya mkononi (7)…………………………gari.

# MADA 10

# SANAA KATIKA JAMII


## Uwezo mahususi wa mada

Kutofautisha aina za sanaa kwa ujumla na kuonyesha nafasi ya sanaa katika jamii.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya sanaa
- Kutaja aina mbalimbali za sanaa
- Kuonyesha umuhimu wa sanaa katika jamii
- Kubainisha aina za maneno ya Kiswahili na matumizi yake

## KIDOKEZO



**Tazama mchoro hapo juu na kutoa maoni yako kuhusu shughuli zinazopatikana kisha ujibu maswali yafuatayo :**

1. Wahusika wanaopatikana kwenye mchoro huo wanafanya nini?
2. Wahusika hao ni nani (husisha na kazi zao)?
3. Shughuli zao zina umuhimu gani kwa jamii?

# SOMO LA 20 : DHANA YA SANAA

## 20.1. Kusoma na ufahamu: Sanaa na manufaa yake

**Soma kifungu cha habari kuhusu Sanaa na manufaa yake, kisha jibu maswali uliyotolewa hapo chini**

Sanaa ni kazi ya ustadi na ufundi wowote wa kuibusha mawazo yaliyomo katika akili ya binadamu na kuyaonyesha kwa njia mbalimbali. Mtu hueleza hisia zinazomgusa kwa kutumia umbo fulani ambalo limesanifiwa. Kazi yoyote ya sanaa inategemewa ionyeshe ufundi wa hali ya juu ili iwe na mvuto kwa hadhira yake. Kazi yoyote ya sanaa inapaswa kuwa na sifa tatu muhimu: uzuri, upya na ujumbe.

Sanaa ni za aina mbalimbali. Kuna sanaa za uonyeshi ambazo uzuri wake hujitokeza katika umbo la kudumu, umbo ambalo linaweza kuhifadhiwa, hivi kwamba uzuri wake ukaendelea kupatikana wakati wowote ule. Hizi ni kama uchongaji, uchoraji, ufinyanzi, ufumaji, ushonaji, ususi na kadhalika. Tena kuna sanaa za vitendo ambazo uzuri wa sanaa hizi umo katika umbo la vitendo hivyo, ilimradi kuupata uzuri huo ni lazima kutazama vitendo vinavyofanyika au ukasikiliza yale yanayosimuliwa kama vitendo vyenyewe ni vya kimasimulizi. Sanaa hizi ni kama zile zinazoambatana na ngoma, utambaji, masimulizi na kadhalika.

Wanyarwanda na Waafrika kwa ujumla wanasifiwa kwa kuwa na sanaa mbalimbali zinazowapendeza watu wengi. Miongoni mwa wasanii ambao hupendwa zaidi ni pamoja na wale wenye ustadi wa kuzingatia mfumo wa kijadi wa Kiafrika na wengine wanaotumia mbinu za kiteknolojia za kisasa. Hawa wote lengo lao ni kuendeleza jamii katika nyanja mbalimbali za maisha yake. Wao hutajirika kupitia shughuli zao za kisanaa ambazo huwaletea pato kubwa kila mwezi. Nchini Rwanda, wasanii wengi hujiunga katika vyama vya ushirika vyenye kuzalisha mali ambavyo huwanufaisha kwa namna tofauti. Mfano mzuri ni vyama vinavyopatikana katika maeneo mengi yaliyojengwa ili kurahisisha shughuli zao za kisanaa. Majengo hayo yanayojulikana kwa jina "*AGAKIRIRO.*" Aidha, yamejengwa katika sehemu mbalimbali za wilaya zote ili kurahisisha shughuli zinazofanywa na wasanii na kukuza vipaji vyao kiasi kwamba mafanikio na manufaa yao hayakadiriki.

Muhire ni kiongozi wa Chama cha Ushirika cha Wafinyanzi ambao hupatikana katika sehemu moja ya wilaya ya Nyarugenge. Yeye huongoza vizuri chama chake na wanachama wote humpenda sana kwani yeye hujitolea sana kwa maendeleo ya chama chao. Yeye huwahimiza wanachama wote waungane na wadumishe ushirikiano kati yao ili pato lao liweze kuongezeka.

Katika kazi zao, wao hutumia udongo maalumu wa kutengeneza vyungu vya kupikia, vyungu vya maua, mitungi, sanamu mbalimbali kama vile sanamu za watu walioacha vitendo muhimu katika jamii, mashujaa, ndege, wanyama na kadhalika. Udongo huu unaotumiwa unajulikana kwa wafinyanzi wote kuwa ni bora kwa shughuli zao kwani unanata na kushikana kwa urahisi. Ni udongo wenye umbile laini kiasi kwamba wateja wao hupenda bidhaa zao.

Muteteri ni kiongozi wa shirika kubwa la maseremala ambao hutengeneza samani za kupendeza kwa kutumia mbao : viti, vitanda, makochi, meza, madawati, makabati, na kadhalika. Wao hutengeneza pia milango na madirisha mazuri ya nyumba. Mara nyingine, kazi zao hufanyiwa nje ya karakana yao kwani watu wengi huwaita kuwatengenezea mapaa ya nyumba zao kwa kutumia miti na mbao za aina mbalimbali. Katika kazi zao maseremala hawa huhitaji misumeno, misumali, nyundo, randa, patasi, kekee na kadhalika. Licha ya kazi hii kuonekana kuwa ni ya kiume, Muteteri na wanawake wenzake hawana tabu ya kuifanya wakishirikiana na wanaume. Kazi hizi zote huwaingizia maseremala hawa kipato kikubwa sana kiasi kwamba mwaka uliopita waliweza kujinunulia gari kubwa la kuwabebea mbao kutoka maeneo mengi ya nchi ya Rwanda. Muteteri binafsi ameshakamilisha jengo la kifahari mjini Kigali ambalo nalo linamletea faranga nyingi kila mwezi.

Mujyambere yeye ni msusi. Pamoja na wenzake kazi yao ni kutengeneza nywele za wanawake kwa kutumia mafuta, nyuzi na hata nywele bandia. Chama chao cha Ushirika kinachoitwa DUFATANYE kinaundwa na vijana wa kiume na wa kike walio na umri kati ya miaka 20 na 35. Wao hupendwa sana na kina mama kwa sababu wanaimudu vizuri kazi yao. Kila binti anayejiandaa kwa sherehe yoyote kama vile kufunga pingu za maisha ni lazima awaendee ili wamrembeshe ipasavyo.

Manufaa yanayotokana na kazi za sanaa ni mengi mno. Mutesi na Kiza wao ni wapishi maarufu katika mgahawa mmoja upatikanao mjini Musanze. Kila asubuhi mgahawa huu hujaa wateja tele kwa sababu ya vitafunio na vyakula vinavyoandaliwa kwa usimamizi wao. Mutesi husimamia upishi wa kinyarwanda, naye Kiza husimamia upishi wa kizungu. Watu wengi wanaofika katika mgahawa wao hufurahia chakula wanachopewa pale. Viongozi wa hoteli nyingi maarufu mjini Kigali walitaka kuwaajiri lakini bosi wao akawapandishia mshahara ili wasimponyoke.

Miongoni mwa wasanii maarufu wanaopata faida kubwa hatuwezi kusahau Agasaro na Mugemana. Wao ni walemavu wa miguu lakini wanaongoza Chama cha Ushirika cha wahunzi kinachopatikana mjini Rubavu. Agasaro ndiye Mkuu wa shirika hilo naye Mugemana makamu wake.

Kazi wanayoifanya pamoja na wanachama wenzao ni kufua madini ya chuma na bati kwa kutengeneza vifaa mbalimbali kama mashoka, panga, visu; mikuki na mishale ya kupambwa nyumbani. Madini haya yakikosekana wao hutumia vyuma vilivyozeeka. Katika kazi yao wahunzi hawa huwasha moto na kuingiza chuma ndani. Chuma hiki kikipata moto wao hukiweka juu ya fuawe na kukipigilia kwa kutumia nyundo hadi kikawa na sura ya kifaa wanachohitaji.

Mbali na sanaa hizo zilizotajwa hapo juu, kuna sanaa nyingine zenye malengo ya kuburudisha, kustarehesha na kuelimisha wanajamii. Mathalani mwanamziki Kabeja ambaye anajulikana kwa nyimbo zake nzuri za kumsifu na kumtukuza Mungu. Bendi yake huimba nyimbo za aina mbalimbali: Nyimbo za kidini, za mapenzi, za kisiasa na nyingine za kijamii. Nyimbo hizi huwatumbuiza mashabiki wao kwa sauti zao laini na zenye mvuto na midundo inayowafurahisha watu wengi. Kila mwishoni mwa wiki wao hupanga tamasha kubwa ambapo bendi yao huimba nyimbo nzuri na kusimulia mashairi kwa watazamaji wao. Licha ya kazi hizi, bendi hii ina tena uzoefu wa kucheza michezo ya kuigiza. Katika kazi yao bendi hii hutumia ngoma, gitaa, zumari, marimba, tarumbeta na kadhalika. Kundi hili hualikwa tena katika sherehe mbalimbali na kutoka likiwa na kitita cha fedha.

Kweli, kazi za sanaa ni nyingi na wasanii wengi hupata mafanikio mengi wanapofanya kazi zao kwa bidii. Wao huwa na nafasi kubwa katika jamii kwani ndio wanaoisaidia kutosheleza baadhi ya mahitaji yao muhimu katika maisha yao ya kila siku. Kutokana na umuhimu wao, Serikali ya Rwamda huwahimiza Wanyarwanda wote kufanya kazi mbalimbali kwa ubunifu katika mradi "Fanya kazi ujitegemee". Ili kufikia lengo lake, sheria imewekwa kwa kulinda kazi zinazobuniwa na wasanii ili zisiigwe, kunakiliwa, kuingiliwa au kuibiwa na wenye hamu ya kula jasho la wengine. Wasanii wengi wameshaelewa umuhimu wa kujiweka pamoja na kushirikiana katika vyama mbalimbali vya kuzalisha mali kupitia sanaa zao. Wao hufikiria kama wahenga waliosema "jifya moja haliteleki chungu."

## KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Sanaa ni nini ?
2. Kazi yoyote ya sanaa huwa na sifa zipi?
3. Taja majina ya wasanii wanaosimuliwa katika kifungu hiki na kueleza kazi zao?
4. «Ulemavu si ugonjwa.» Jadili msemo huu kwa kuuhusisha na yale uliyoyasoma katika kifungu cha habari hapo juu.
5. Unaelewa nini kuhusu methali isemayo « Jifya moja haliteleki chungu?»

## 20.2. Msamiati kuhusu sanaa na manufaa yake

### KAZI YA 2

**Andika maana za maneno haya yafuatayo kulingana na matumizi yake katika kifungu cha habari hapo juu, kisha tunga sentensi moja kwa kutumia maneno hayo.**

1. Ustadi
2. Umbo
3. Karakana
4. Kuburudisha
5. Chama

### KAZI YA 3

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo:**

1. Shabiki
2. Madini
3. Kutumbuiza
4. Fuawe
5. Jifya

## 20.3. Sarufi: Matumizi ya aina za maneno

### KAZI YA 4

**Angalia sentensi zifuatazo ukichunguza maneno yaliyopigiwa mistari kisha ujibu maswali ya hapo chini.**

**a.** <u>Mtoto</u> <u>anacheza</u> mpira <u>wake</u>.

**b.** <u>Yeye</u> <u>ni</u> mrefu sana.

**Maneno yaliyopigiwa mistari ni: nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi.**

- **Nomino/ jina**

  **a. Maana ya nomino**

Nomino au jina ni neno linaloita kitu chenye uhai au kisicho uhai kwa kukitofautisha na vingine.

  **b. Aina za nomino**

  - **Nomino za pekee :** haya ni maneno yanayotaja majina maalum ya watu, mahali, vitu na hata Mungu (Mifano : Kamasa, Kigali, Nyange, Mola, Muhanga, Kagoyire, Akagera, Nyabarongo)
  - **Nomino za kawaida :** haya ni maneno yanayotaja vitu vya kawaida bila kutaja vitu hivyo (Mifano : mtu, mto, ndege, kanzu, kofia, ...)
  - **Nomino za dhana au za dhahania :** ni maneno yanayotaja vitu vya kufikiria au vya hisi tu (Mifano : uchungu, usingizi, uchoyo, uwili, ...)
  - **Nomino za jamii/ za makundi :** ni maneno yanayotumiwa kurejelea vitu au watu wanaotokea kwa makundi (Mifano : jeshi, kamati, kaumu, umati, umma, taifa, familia, ...)
  - **Nomino za wingi :** ni maneno yanayorejelea vitu ambavyo huwa katika hali ya wingi (Mifano : maji, mafuta, mawaidha, maziwa, manukato, ...).
  - **Nomino za kitenzi-jina** : haya ni maneno yanayotokea kwa vitenzi lakini yanapotumika huwa ni nomino (Mifano : **kucheza** kunapendeza. **Kuimba** ni kuzuri. **Kutembea** kwao kunachesha.)

- **Kitenzi**

  **a. Maana ya kitenzi**

Kitenzi ni neno linaloeleza jambo linalotendwa au kufanywa na nomino au kiwakilishi chake.

  **b. Aina za vitenzi**

■ **Kitenzi halisi :** ni kitenzi kimoja kinachotumiwa katika sentensi. Vitenzi halisi huchukua viambishi mbalimbali.

**Mifano:**

  - Mwanafunzi **anasoma** kitabu.
  - Mgeni wetu **atawasili** kesho.

■ **Vitenzi vikuu :** kitenzi kikuu hueleza kitendo chenyewe kwa wakati uliotajwa. Wakati mwingine vitenzi viwili hutumika pamoja kueleza kitendo kimoja. Kitenzi cha kwanza huitwa kisaidizi na cha pili ndicho kitenzi kikuu.

**Mifano:**

  - Mtoto alikuwa **akisoma**.
  - Yeye anataka **kuondoka**.

- **Vitenzi visaidizi :** kama tulivyoeleza hapo juu, vitenzi visaidizi hutumika pamoja na vitenzi vikuu katika kueleza taarifa kamilifu.

**Mifano:**

- Maandishi **yangali yanasomeka**.
- Zamani watu **walikuwa wanasaidiana** kazi.

- **Vitenzi vishirikishi :** haya ni maneno ambayo hutumiwa katika sentensi kuonyesha ushirikiano au uhusiano baina ya nomino na kiwakilishi, kivumishi na nomino. Vitenzi vishirikishi vina dhana ya kitenzi **kuwa** au **kuwa na**.

Vitenzi vishirikishi huwa vya aina mbili kuu:

- **Vitenzi vishirikishi vikamilifu :** hivi ni vitenzi vishirikishi vinavyoweza kuchukua viambishi vya wakati na viambishi nafsi.

**Mifano:**

- Wavuvi **wangali** baharini.
- Wewe **umekuwa** mzembe.

- **Vitenzi vishirikishi vipungufu :** hivi ni vitenzi vishirikishi ambavyo vinaweza huchukua viambishi nafsi lakini havichukui viambishi wakati.
  - Walimu **si** waongo**.**
  - Wewe **u** mrefu**.**
  - Mimi **ni** mwalimu**.**
  - Mimi **ndimi** mwalimu**.**

## KAZI YA 5

**Jibu maswali yafuatayo:**

a. Taja aina za nomino katika sentensi zifuatazo:
- Mheshimiwa Rais atakuja.
- Katika jamii ya Wanyarwanda watu husaidiana.

b. Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo:
- ni
- mkisoma
- palilia
- sambaza
- utakuwa

## 20.4. Matumizi ya lugha: Dhana ya sanaa

### KAZI YA 6

**Soma maelezo yafuatayo kisha ujibu maswali ya hapo chini**

Sanaa ni ufundi wa kuwakilisha mawazo na hisia alizonazo binadamu kwa njia ya ubunifu. Njia hizo zaweza kuwa wimbaji, uchoraji, ushonaji, ujenzi, ufinyanzi, masimulizi na kadhalika. Njia hizi tofauti ndizo zinatufanya tuwe na aina mbalimbali za sanaa. Kwa hivyo, kulingana na njia zilizotajwa hapa, ni dhahiri kwamba tutapata sanaa ya uimbaji, sanaa ya uchoraji, sanaa ya ujenzi, sanaa ya ufinyanzi, na kadhalika. Mtu anayeshughulikia sanaa huitwa msanii.

Kila kazi ya sanaa inapaswa kuonyesha uzuri wa aina yake. Uzuri huu waweza kuonekana, kuguswa, kusikiwa au kuonjwa kulingana na aina ya sanaa inayohusika. Pia kazi ya sanaa inapaswa kuwa na upya. Upya ndio unaotofautisha sanaa za msanii fulani na za wenzake. Kisha kazi ya sanaa inapaswa kuwa na ujumbe. Kusema kuwa kazi ya sanaa inapaswa kuwa na jambo fulani inalowasilisha katika jamii.

Kila kazi ya sanaa ina nyenzo au zana zinazotumiwa kwa kufanikisha kazi hiyo. Kwa mfano mfinyanzi huhitaji udongo, mchongaji hutumia mawe au miti na sonara hulazimika kuwa na madini.

**Maswali :**

1. Toa maana ya sanaa.
2. Ni zipi sifa za kazi ya sanaa?

## 20.5. Kuzungumza na Kusikiliza: Majadliano

### KAZI YA 7

***Jadili kisha uwasilishe kuhusu*** *"Madhara yanayoweza kujitokeza katika jamii pale sanaa inapotumiwa vibaya."*

## 20.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari


### KAZI YA 8

**Tunga kifungu cha habari chenye mada hii*:***

"Umuhimu wa sanaa katika Jamii"

# SOMO LA 21. UMUHIMU WA SANAA KATIKA JAMII

## 21.1. Kusoma na ufahamu: Umuhimu wa sanaa katika Jamii



### KAZI YA 1

**Eleza tukio mnaloliona kwenye mchoro hapo juu.**

***Soma kifungu cha habari kuhusu* "Sanaa katika jamii"*, halafu jibu maswali yaliyotolewa hapo chini***

Mwishoni mwa mwezi Oktoba wa kila mwaka, viongozi wetu hutoa tangazo la kuwaalika vijana wote kutoka tarafa zetu ili wakusanyike kwenye uwanja wa mpira wa wilaya yetu kuhudhuria mashindano ya maonyesho ya vipawa mbalimbali. Mwaka uliopita, vijana walioshiriki katika mashindano hayo walikuwa vijana wengi mno. Makundi mengi yalikuwa yamejisajili kwa kushiriki katika mashindano hayo na kila mwanakundi alikuwa akijigamba kwa uwezo wake akijilinganisha na wenzake waliotoka katika tarafa mbalimbali. Makundi ya wanamuziki, wacheza ngoma, wachoraji, wafinyanzi, wanafasihi, wafumaji, watarizi, wasusi, na wengine kutoka kila tarafa walikuwa wamejiandaa kwa sanaa zao za kuvutia. Watazamaji wote walikuwa na hamu kubwa ya kuona kundi litakaloshinda wengine kwa kuonyesha vipaji vyao na kuwavutia watazamaji.

Uwanja ulikuwa umefurika, hapa mashabiki wa kila kundi wakishangilia kundi lao kwa kelele nyingi, ngoma, vifijo na nderemo. Baada ya muda mfupi, jopo la tathmini lilifika hapo na kila mwanajopo akachukua kiti chake. Jopo lenyewe lilikuwa limeundwa na watu watatu : waume wawili na mwanamke mmoja. Sote tuliamrishwa kutulia na kufuata maelekezo yaliyotolewa na mkuu wa jopo hilo. Makundi yote yalitakiwa kuchagua mwakilishi wao wa kuja kuchagua nambari itakayoonyesha zamu yao kupita jukwaani. Huu ulikuwa wakati wa tumbo joo, hivi kila kundi likiwa na woga wa kutangulia makundi mengine. Kundi la ngoma lilitangulia kupanda kwenye jukwaa na watu wote wakasimama kushabikia. Kundi hili lilikuwa limesindikizwa na wasichana pamoja na wavulana waliokuwa wakicheza ngoma hizo kwa ustadi mkubwa huku wapigaji ngoma kwa upande wao, wakijigamba na kuruka kiufundi huku na kule. Muda wao wa kuigiza ulipokwisha, walipongezwa na kupigiwa makofi mengi nao wakarudi kwenye nafasi yao. Huu ulikuwa sasa wakati wa kundi la uchoraji. Washindani katika kundi hili walikuwa watano: wavulana wawili na wasichana watatu, kila mmoja akiwa na vifaa vyote vya uchoraji vilivyohitajika. Waliambiwa kufanya mchoro wa ng'ombe watatu pamoja na mchungaji wao kwa dakika tano hivi wakionyesha ustadi wa kuchanganya rangi.

Watu wengi walistaajabu kusikia hilo, wakidai kwamba haiwezekani kufanya mchoro wa namna hiyo kwa dakika tano tu. Mwamuzi alipokipuliza kipenga cha kuanza, umati wote ulisimama na kuangalia kwa makini jinsi vijana hao walivyoonyesha ustadi wao katika uchoraji. Filimbi ya mwisho ilipopigwa msichana mmoja alikuwa amekwishamaliza. Hawa wote watano wakaambiwa kuonyesha michoro yao. Umati wote ulishangilia na kustaajabu sana walipoona jinsi mchoro wa msichana yule ulivyofanywa kwa ufundi wa hali ya juu kushinda michoro mingine. Yeye alichukua nafasi ya kwanza na kufuatwa na mvulana ambaye pia alikuwa na ulemavu wa miguu. Huyu alikuwa amemaliza mwaka mzima baada ya kunusurika katika ajali ya gari alipotoka Kampala kushiriki katika Mashindano ya Kimataifa ya Wachoraji wenye umri wa chini ya miaka ishirini.

Makundi yote yalipewa muda wa kujitokeza na kuonyesha vipawa vyao kwenye jukwaa lililokuwa limetengenezwa kwa ajili ya mashindano hayo. Waigizaji wa mashairi walipewa nafasi yao ya kuonyesha umahiri wao katika utunzi wa mashairi. Katika kundi hili Karasira na Mukamwiza ndio walioibuka na ushindi. Karasira aliimba wimbo mzuri sana uliowafurahisha wengi. Yeye alionekana kuwa na sauti nzuri, nyororo na maneno matamu aliyoyatumia yaliwafurahisha wengi. Maudhui ya wimbo wake yalielekea kuwasifu wazazi wote kwa jumla kwa kudhihirisha jinsi wanavyojitolea kuwatafutia kila wanachohitaji na kuwapatia malezi mema tangu utoto hadi wanapokuwa watu wazima.

Kundi lake lilikuwa moja kati ya makundi mengine yaliyoigiza vipawa mbalimbali vya kifasihi. Makundi mengine ya kifasihi yaliyoshiriki katika mashindano hayo yalihusisha watunzi wa mashairi, Watambaji hadithi, waigizaji wa michezo mbalimbali kama vile wacheshi walioonyesha ubingwa na ubunifu mkubwa katika matumizi ya lugha. Badhi ya watambaji hadithi walikuwa wametunga hadithi kwa kusimulia matukio mbalimbali kuhusu sungura na wanyama wengine.

Upande wa mashairi nao ulichangamsha sana umati uliokuwepo. Watunzi wengi wa mashairi walizingatia maudhui yaliyolenga umuhimu wa fasihi katika jamii. Pamoja na shairi hili, umma uliweza kuelimika na kufungua macho mpaka wengi wakatangaza kuwa waliweza kutambua udhaifu uliojitokeza katika jamii na mambo mbalimbali yaliyotakiwa kurekebishwa na kupewa mwelekeo katika jamii yao. Wanamashairi hao waliwafundisha mengi, wakaburudika mpaka walipoanza kutokwa na machozi kwa furaha tele. Kupitia mashairi mengi yaliyosimuliwa pale, watu walipata mwanya wa kuthamini umuhimu wa fasihi, yaani sanaa ya kuitumia lugha. Wazee waliokuwepo waliwaelezea vijana wengi kwamba fasihi au sanaa ya kuitumia lugha ni njia bora ya kuonyesha mawazo ya wasanii kwa kuitumia lugha.

Watazamaji wote waliweza kuelewa utamu uliopatikana katika misemo ya washindani waliokuwepo kushangaa kuona jinsi uzuri huo uliweza kuambatanishwa na umuhimu wa sanaa hiyo katika jamii. Wengi walikuwa wakisema kuwa fasihi huendeleza, huhifadhi na kurithisha utamaduni, mila na desturi za jamii na pia kwamba fasihi huwaelimisha wanajamii kwa njia moja au nyingine. Pamoja na hayo yote, watu wote waliahidi kuithamini walipotambua kuwa iliweza kulinganishwa na jiwe kubwa la thamani linalohitaji kuhifadhiwa na kutunzwa vizuri. Wao waliweza kuelewa jinsi lugha inavyotumiwa na kuvutia masikio ya wote waliokuja kushiriki katika mashindano hayo. Mwishoni mwa tamasha hilo watazamaji wote walikuwa wamechangamka kwa vicheko na furaha kubwa.

Mkuu wa kamati ya majaji alisimama na kuyashukuru makundi yote yaliyokuwa yamehudhuria tamasha hilo. Washindani walikuwa tayari kuyasikiliza matokeo ya michezo na maonyesho yao. Kwa kweli, mioyo yao ilikuwa ikiwadundadunda walipokuwa wakisubiri maneno yaliyotarajiwa kutangazwa na Mkuu wa Jopo. Lakini, kama wasemavyo wahenga : « Asiyekubali kushindwa si mshindani ». Watu wote walikuwa wametulia tuli kama maji mtungini. Punde si punde mkuu wa jopo alitangaza washindi kulingana na sanaa zote zilizoshirikishwa na zawadi nyingi zikatolewa. Watazamaji walitoka wakicheka na kuwapongeza sana wanafasihi wote walioshiriki katika mashindano kwa sauti kubwa « Fasihi ! Fasihi ! Fasihi ! Oyeeee ! Oyeeee ! ». Wao walifurahia maonyesho yote ya kifasihi na jinsi washindani walivyoonyesha ufundi mkubwa katika mawasilisho yao.

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Kazi ya jopo la tathmini ilikuwa ipi ? Jopo hilo liliundwa na nani?
2. Kwa nini wachezaji ngoma walipongezwa?
3. Wachoraji waliambiwa kufanya nini? Nani aliweza kushinda kati ya wachoraji wote?
4. Ulemavu wa kijana mvulana aliyechukua nafasi ya pili ulitokana na nini?
5. Maudhui ya wimbo wa Karasira yalihusu nini?

## 21.2. Msamiati kuhusu sanaa katika Jamii

## KAZI YA 3

**Eleza maana ya maneno yafuatayo kulingana na muktadha wa matumizi yake katika kifungu cha habari.**

1. Umahiri
2. Umati
3. Jopo
4. Mashindano
5. Kuthamini

## KAZI YA 4

**Tumia mshale kwa kuoanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Shairi | a. Furaha kubwa inayohusisha michezo na burudani inayofanywa kusherehekea jambo fulani. |
| 2. Vipawa | b. Kuwako mahali penye shughuli fulani k.v. mkutanoni au kwenye sherehe. |
| 3. Tamasha | c. Uwanja umejaa watu wengi kupita kiasi |
| 4. Jukwaa | d. Mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi. |

| | |
|---|---|
| 5. Umahiri | e. Uwezo mtu aliozaliwa nao ambao humwezesha kufanya jambo fulani vizuri. |
| 6. Fasihi | f. Mambo yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi |
| 7. Mashabiki | g. Maneno ya maonyo au mafunzo, mashauri. |
| 8. Kuhudhuria | h. Uhodari wa kufanya jambo fulani |
| 9. Mawaidha | i. Somo linalohusiana na tungo za sanaa kama vile ushairi, riwaya, tamthiliya, tenzi, semi, vitendawali, hadithi na ngano |
| 10. Tumbo joto | j. Watu wenye kupenda sana jambo au kitu fulani. |
| 11. Umati | k. Hali ya kuwa na woga. |
| 12. Uwanja umefurika | l. Sehemu iliyoinuliwa ndani ya jengo kubwa au katika uwanja ambayo hutumika kuonyesha michezo au kutolea hotuba. |

## 21.3. Sarufi: Matumizi ya aina za maneno ya Kiswahili

### KAZI YA 5

**Angalia maneno yaliyopigiwa mistari halafu utaje aina zake.**

- Mwanafunzi **mdogo** anakimbia.
- **Yeye** yu wapi?
- **Wadogo** walitaka kuingia hapa.

- **Mdogo** ni kivumishi.
- **Yeye, wadogo** ni viwakilishi.

### Maelezo muhimu kuhusu aina za maneno

Katika masomo yaliyotangulia, umeweza kujifunza aina mbalimbali za maneno. Somo hili linashughulikia aina mbili yaani kivumushi na kiwakilishi.

- **Vivumishi**

**a. Maana ya kivumishi**

Vivumishi au visifa ni maneno yanayotuelezea zaidi kuhusu nomino. Aghalabu vivumishi hutanguliwa na nomino.

**b. Aina za vivumishi**

- **Vivumishi vya sifa**

Hivi ni vivumishi ambavyo hutoa sifa ya kitu, mtu, mahali, n.k

**Kwa mfano:** kizuri, kali, safi, mrembo,...

- Mama yule **mweusi** hupika chakula **kitamu.**
- Mvulana **mkorofi** aliadhibiwa na mwalimu kutokana na tabia zake **mbaya.**
- Sauti **nzuri** humtoa nyoka **mkali** pangoni.

- **Vivumishi vimilikishi**

Vivumishi hivi hutumika kuonyesha nomino inamiliki nyingine. Mizizi ya vivumishi hivi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali: *-angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao*

**Kwa mfano:** changu, lako, yake, kwetu, vyenu, zao.

- Nitatumia talanta **zangu** kwa manufaa ya taifa **letu**.
- Aliweka kitabu **chako** sebuleni **mwako.**
- Katosha amepata nguo **yake** katika sanduku **lao.**

- **Vivumishi vya idadi**

Hutueleza zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi.

a. Idadi kamili - hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino.

**Kwa mfano:** tatu, mbili, kumi.

- Msichana **mmoja** amewaua nyoka **wawili.**
- Siku **kumi** zimepita tangu Bi Safina alipojifungua watoto **watatu.**

b. Idadi isiyodhihirika - huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili.

**Kwa mfano:** chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani.

- Watu **wachache** waliohudhuria mazishi ya Musabende walikula chakula **kingi** sana.
- Baba yao alikuwa mateka kwa miaka **kadhaa.**

- **Vivumishi viulizi**

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza swali.

Baadhi ya vivumishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli.

**Kwa mfano:** -ngapi?, -pi?, gani?

- Ni walimu **wangapi** wamefukuzwa? (- kuulizia idadi)
- Je, ni dawati **lipi** lenye funguo zangu?
- Unazungumza kuhusu kipindi **gani?**

- **Vivumishi viashiria / vionyeshi**

Vivumishi viashiria hutumika kuonyesha au kuashiria nomino kulingana na mahali.

**Kwa mfano:**

**Karibu** - hapa, huyu, hiki, hili, huku, haya, ule, wale, pale.

**Mbali kidogo** - hapo, huyo, hiyo, hicho.

**Mbali zaidi** - pale, lile, kile.

- Msichana **huyu** ni mkubwa kuliko **yule.**
- Jani **hili** la mwembe limekauka.
- Tupa mpira **huo!**

- **Vivumishi visisitizi**

Husisitiza nomino fulani kwa kurudiarudia kivumishi kiashiria

**Kwa mfano:** Yuyu huyu, wawa hawa, kiki hiki, papo hapo, mumu humu.

- Jahazi **lili hili.**
- Wembe **ule ule.**
- Ng'ombe **wawa hawa.**

- **Vivumishi vya KI-Mfanano**

Vivumishi vya KI- ya Mfanano hutumika kulinganisha sifa ya nomino na hali au tabia nyingine. Vivumishi hivi hutanguliwa na nomino, kiunganishi cha A-unganifu na huchukua kiungo **KI.**

**Kwa mfano:** wa kifalme, za kijeshi, ya kitajiri, n.k

- Chifu wa Vikwazoni anaishi maisha **ya kimaskini.**
- Chali anapenda kusikiliza muziki **wa kizungu.**
- Bi Naliza huvulia mavazi **ya kifalme.**

- **Vivumishi vya A-unganifu**

Vivumishi hivi hutuelezea zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha kitu kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha **kiambishi** cha nafsi/ngeli pamoja na a-unganifu, kisha nomino.

**Kwa mfano:** cha, la, kwa, za, ya.

- Watoto **wa mwalimu mkuu** wana tabia nzuri.
- Chai **ya daktari** imemwagika.

## KAZI YA 6

**Pigia mstari vivumishi katika sentensi zifuatazo:**

a. Kutokana na mvua kubwa iliyonyesha, hapatapatikana mazao bora na mengi.
b. Jambo zuri la kufanya ni kujitenga na mambo maovu duniani.
c. Nguo ile imempendeza mtu yule.
d. Kiti hicho kimevunjika, niletee kile pale.
e. Ni mwanafunzi gani anaugua?

- **Viwakilishi**

**a. Maana ya viwakilishi**

Viwakilishi ni maneno yanayotumika badala ya nomino. Kiwakilishi hakiwezi kuambatanishwa na nomino inayorejelewa.

**b. Aina za viwakilishi**

- **Viwakilishi vya nafsi**

Viwakilishi hivi hutumika kwa niaba ya **nafsi** kwa umoja na kwa wingi.

**Kwa mfano: Mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao ni viwakilishi nafsi huru**.

Ni-, u-, a-, tu-, m-, wa- ni **viwakilishi nafsi viambata**.

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| **Nafsi ya Kwanza** | Mimi **ni**naimba | Sisi **tu**naimba |
| **Nafsi ya Pili** | Wewe **u**nakula | nyinyi/ninyi **m**nakula |
| **Nafsi ya Tatu** | Yeye **a**naandika | Wao **wa**naandika |

- **Sisi** tuliwatangulia **nyinyi** kufika hapa.
- **Mimi** si mjinga kama vile **yeye** anavyofikiria.

- **Viwakilishi viashiria**

Viwakilishi viashiria (vionyeshi) hutumika badala ya nomino kwa kutumia kuonyesha nomino inayorejelewa bila kuitaja.

**Kwa mfano:** huyu, yule, hapa, n.k.

- **Hiki** hakina maandishi yoyote.
- **Hao** hawajui tofauti ya viwakilishi na vivumishi.

- Tumekuja **hapa** ili kuwaburudisha kwa nyimbo tamu tamu.

- **Viwakilishi visisitizi**

Hutumika kwa niaba ya nomino kwa kutumia kiashiria chake mara mbili mfululizo.

**Kwa mfano:** yuyu huyu, wawa hawa, kiki hiki, papo hapo, mumu humu, n. k.

- **Zizi hizi** ndizo zilizovunjika wiki jana.
- **Yule yule** aliyekamatwa juzi, ameiba tena.

- **Viwakilishi vya sifa**

Husimama badala ya nomino kwa kurejelea sifa yake.

**Kwa mfano:** -eupe, -zuri, -tamu, -embamba, -rembo.

- **Vyekundu** vimehamishwa.
- **Warembo** wamewasili.
- **Kitamu** kitaliwa kwanza.

- **Viwakilishi vya idadi**

Hutumika kusimama badala ya nomino kwa kurejelea idadi yake.

a. Idadi Kamili - hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino.

**Kwa mfano:** saba, mmoja, ishirini.

- **Wawili** wamepigwa risasi na polisi leo jioni.
- Alimpatia mtoto wake **hamsini** kununua chakula

b. Idadi isiyodhihirika - huelezea kiasi cha nomino kwa jumla, bila kutaja idadi kamili

**Kwa mfano:** chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani.

- Tutazungumza na **wachache** kabla ya kuanzisha maonyesho yetu.
- **Kadhaa** zimeripotiwa kupotea.

- **Viwakilishi viulizi**

Viwakilishi viulizi hutumika kwa niaba ya nomino katika kuulizia swali.

Baadhi ya viwakilishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli.

**Kwa mfano:** -ngapi?, -pi?

- **Vingapi** vinahitajika? (Kuulizia idadi)

- **Zipi** zimepotea?

Kuna viwakilishi viulizi vingine ambavyo havichukui viambishi vyovyote.

**Kwa mfano:** papi?, gani?,  nini?, vipi?

- **Gani** imefunga bao hilo?
- **Papi** hapana majimaji?
- **Nani** amefika?
- Mvulana yule alikupatia **nini?**
- Uliongea naye **vipi?** (Kuulizia namna)

- **Viwakilishi vimilikishi**

Viwakilishi hivi hurejelea nomino kwa kutumia vimilikishi.

**Kwa mfano:** -angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao.

- **Kwetu** hakuna stima.
- **Lake** limekucha.
- **Zao** zimeharibika tena.

- **Viwakilishi virejeshi**

Hutumia O-rejeshi kurejelea na kusimamia nomino.

**Kwa mfano:** ambaye, ambao, ambalo, ambacho.

- **Ambalo** lilipotea limepatikana.
- **Ambaye** hana mwana, aeleke jiwe.

- **Viwakilishi vya A-unganifu**

Huwakilisha nomino kwa kutaja kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha **kiambishi**/ngeli pamoja na a-unganifu, kisha nomino nyingine.

**Kwa mfano:** cha, la, kwa, za, ya

- **Cha** mlevi huliwa na mgema.
- **Za** watoto zitahifadhiwa.

## 21.4. Matumizi ya lugha: Maelezo muhimu kuhusu dhima za sanaa katika jamii

### KAZI YA 7

**Soma maelezo muhimu yafuatayo kisha jibu maswali yafuatayo:**

Sanaa ina umuhimu mkubwa katika jamii. Kwanza sanaa inaweza kuelimisha jamii. Kwa mfano ukitumia fasihi unaweza kukosoa, kuionya na kuierekebisha jamii. Fasihi huchambua na kuchochea umma na kuwafumbua macho wanajamii ili waweze kufichua uwezo au udhaifu uliomo katika jamii.

Sanaa ina umuhimu wa kuburudisha jamii. Ukitumia fasihi na muziki unaweza kuburudisha, yaani husisimua kimwili na kiakili msikilizaji au msomaji na kuvutiwa kihisia.

Sanaa nyingine zinaweza kuhifadhi na kurithisha amali za jamii. Kwa mfano katika fasihi, uchoraji na uchongaji watu wanaweza kutunza na kuhifadhi mila na desturi za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

Isitoshe, sanaa ina umuhimu wa kumtajirisha msanii: kazi ya sanaa inaweza kumletea pato msanii.

Kisha sanaa ina umuhimu wa kuikomboa jamii. Mara nyingi kazi za sanaa zilitumiwa kama silaha ya ukombozi kwa kumwezesha mwanadamu kueleza yale yote yaliyokuwa yakimsumbua na kupigania uhuru wake.

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja aina tano za umuhimu wa sanaa katika jamii.
2. Kwa sababu gani sanaa inachukuliwa kama silaha ya ukombozi wa jamii?

## 21.5. Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

### KAZI YA 8

**Jadili na wenzako mada ifuatayo "*Sanaa inaweza kujenga na kujengua jamii,*" kisha uwasilishe kazi yako darasani.**

## 21.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

### KAZI YA 9

**Tunga kifungu cha habari chenye mada hii:**

*"Umuhimu wa sanaa katika jamii"*

### TATHMINI YA MADA YA KUMI

1. Sanaa ni nini?
2. Taja aina tano za sanaa.
3. Eleza aina tano za sanaa na umuhimu wa kazi za kisanaa kwa jamii.

MADA 11

# FASIHI KATIKA JAMII

**Uwezo mahususi wa mada**

Kuelezea umuhimu wa tanzu mbalimbali za fasihi katika jamii.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Kueleza maana ya fasihi.
- Kuonyesha mchango wa fasihi katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi katika jamii.
- Kukumbuka aina za maneno ya Kiswahili.
- Kueleza vipengele vya fasihi ya Kiswahili na tanzu zake.

## KIDOKEZO

**Chunguza kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza wahusika unaowaona kwenye picha hii.
2. Wahusika hao wako wapi?



# SOMO LA 22: FASIHI NA UMUHIMU WAKE KATIKA JAMII

## 22.1. Kusoma na ufahamu: Maana ya fasihi

**Soma kifungu cha habari kuhusu dhana ya fasihi, kisha jibu maswali uliyotolewa hapo chini.**

Jumatatu moja mwalimu wetu wa Kiswahili aliingia darasani na kikapu begani na madaftari mkononi. Kama kawaida alitusalimia huku akitabasamu. Wanafunzi wote katika madarasa matano ya mchepuo wa lugha tulimpenda sana kwani alikuwa mwalimu mwerevu, mzuri na mpole. Tena aliheshimu watu wote na wote wakamheshimu. Wakati huo nami nilikuwa nikisoma katika kidato cha tano, mkondo wa lugha.

Mwalimu alianza somo ambalo liliwavutia wanafunzi wote darasani. Sote tulikuwa na vitabu vya Kiswahili vya mwanafunzi na kila mwanafunzi alikuwa amefungua kitabu chake. Mwalimu alituomba kuunda makundi ili tusome kifungu kuhusu dhana ya fasihi na umuhimu wake katika jamii. Aliomba makundi yote kujiandaa kwa kazi yao. Baadaye, kila kundi lilipewa dakika kumi na tano za kuwasilisha hadharani matokeo ya kazi. Makundi yote yalikuwa yamejitahidi kufanya kazi vizuri. Sote darasani tulielewa vizuri kwamba fasihi ni sanaa ya lugha ambayo hushughulikia masuala yanayomhusu binadamu.

Makundi yote yaligundua kwamba fasihi huzungumzia na kuonyesha maisha ya jamii, kwa kuelezea mambo yote yaliyomo katika jamii hiyo: matatizo, mitazamo, migogoro, itikadi, na shughuli mbalimbali za kijamii zilizopo huwa ni mambo yanayobainishwa katika kazi ya fasihi; yaani sanaa ambayo hutumia lugha. Vile vile, wanafunzi wote walielewa kuwa kila mtu anayejishughulisha na utunzi wa kazi ya fasihi hulenga kudhihirisha hisia alizonazo kulingana na mazingira anamoishi. Yeye huitazama jamii yake na kueleza yote yatendekayo katika jamii hiyo kwa njia ya lugha.

Makundi yote yalipomaliza kuwasilisha, mwalimu wetu alisisitiza kwamba fasihi hutumia lugha kisanaa na kuwa malengo ya fasihi ni kuelimisha wanajamii, kuwaburudisha na kuwastarehesha. Yeye alieleza kwamba fasihi huwaonya wanaotenda maovu kuacha maovu yao na kuwahimiza wanaotenda mema kuendeleza matendo yao mazuri. Vilevile, fasihi ni kioo cha jamii na mwavuli wake. Inalinda jamii kwa kuhifadhi na kueleza vitendo vyake ambapo vitendo vizuri huhimizwa na kuchochewa ilhali vitendo vibaya hukatazwa. Msanii ambaye ni mwanafasihi huitumia lugha fulani kwa kujulisha jamii mengi yaliyomo katika utamaduni wake.

Somo hilo lilitupendeza wote kiasi kwamba tuliamua kujifunza vizuri lugha ya Kiswahili ili tuweze kuitumia kisanaa.

Leo hii, wanafunzi wengi tuliosoma pamoja enzi hizo tunajishughulisha na kazi mbalimbali za kisanaa zinazotumia lugha ya Kiswahili. Baadhi yao ni waimbaji, watunzi wa mashairi na waandishi wa vitabu kama mimi. Kila mwaka tunakutania katika maonyesho ya kitamaduni na huwa tunapata faranga nyingi.

### KAZI YA 1

**Maswali ya ufahamu**

1. Taja mambo matatu yanayoweza kugusiwa katika kazi ya fasihi.
2. Kwa nini wanafunzi waliamua kujifunza vizuri lugha ya Kiswahili?
3. Fasihi inahusianaje na utamaduni?
4. Msimulizi anafanya nini siku hizi?
5. Katika mistari michache, eleza maana ya fasihi na umuhimu wake katika jamii.

## 22.2. Msamiati kuhusu dhana ya fasihi

### KAZI YA 2

**Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayofuata:** sanaa, mwanafasihi, jamii, utamaduni, imani, mtazamo, wanajishughulisha, fasihi, maovu, waliamua.

1. ............................. anatarajiwa kutumia vizuri vipaji vyake vya kisanaa.
2. Sote tunalazimika kukuza ................................. wa usafi katika kazi.
3. Mimi nitaendelea na masomo ya .................................. chuoni.
4. .......................wake kuhusu michezo shuleni ni tofauti na ule wa mkurugenzi.
5. Fasihi kama .............................. inaweza kumpa mtu faida na kumtunza.
6. Baada ya majadiliano makali .................................... kusikilizana kwa ajili ya kuishi kwa amani kati yao.
7. Kila mwanadamu anatarajiwa kuepuka mambo ...........................
8. Watu wengi tuliosoma pamoja ....................... na kazi mbalimbali za kisanaa wakitumia lugha ya Kiswahili.
9. Ninapenda .......................yetu ya Rwanda kwani inapiga marufuku ubaguzi wowote.
10. Ndugu zangu wana ................................. kwamba watamaliza masomo yao na kuwa wasanii maarufu.

## 22.3. Sarufi kuhusu matumizi ya aina za maneno

### KAZI YA 3

**Taja aina za maneno ambayo yamepigiwa msitari katika sentensi hizi:**

1. Mtoto aliposoma **sawasawa** alipewa biskuti na wazazi.
2. Nyimbo ziimbwazo **kitoto** huchekesha **kwelikweli**.
3. Vigelegele vililia **lelelele** **lelelele** **juzi**.
4. Ukichokorachokora sikio lako utajitia mashakani **polepole**.

### Maelezo muhimu

**Vielezi**

Vielezi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu kitendo kilivyofanyika. Pia vielezi hutoa habari zaidi kuhusu hali, vivumishi na vielezi vingine.

**Tazama aina mbalimbali za vielezi katika jedwali na matumizi yake**

| | Aina ya vielezi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | **Vielezi vya namna au jinsi:** Haya ni maneno ambayo huarifu jinsi ya kutendeka kwa mambo. | Wanakijiji hufanya kazi **kwa bidii** pamoja.<br>Usisumbuke **bure**! Tutakusaidia.<br>Tutaimba **kwa furaha** siku ya harusi yako.<br>Tembea **haraka** tumechelewa mkutanoni. |
| 2. | **Vielezi vya wakati:** Nayo haya ni maneno yanayofafanua ama kueleza wakati wa kutokea kwa kitendo. | Mkutano ulianza **mapema.**<br>Tutaondoka hapa **saa kumi jioni**.<br>Wanasiasa hawa walianza kushirikiana **zamani**. |
| 3. | **Vielezi vya kiasi/idadi:**<br>a) **Idadi kamili** - hutaja idadi kamili ya mara ngapi kitendo kilifanyika.<br>**Kwa mfano:** mara mbili, siku mbili kwa juma, mara kumi. | Kazi ya umuganda hufanywa **mara moja** kwa mwezi.<br>Nilipoenda harusini **mara ya kwanza** nilikula sana. |
| | b) **Idadi isiyodhihirika**<br>- huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili<br>**Kwa mfano:** mara chache, mara kwa mara, mara nyingi, mara kadhaa. | a. Yeye hunipigia simu **mara kwa mara.**<br>b. Mwizi wa kuku alipigwa **mara kadhaa** kabla ya kuokolewa na polisi. |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | **Vielezi vya mahali:** Ni maneno ambayo hutoa habari kuhusu mahali ambapo kitendo kilifanyiwa. | a.Msipite **sokoni** mkienda **kanisani**.<br>b.Mtoto hajatulia **nyumbani**.<br>c.Alitoka **Butare** leo.<br>d.Twende **uwanjani**. |

## KAZI YA 4

**Chunguza sentensi zifuatazo kisha utaje aina za maneno ambayo yamepigiwa mistari:**

1. Anasoma vizuri lakini hashindi.
2. Baba na mama hupendana.
3. Utaenda mjini au utabaki hapa?
4. Yeye hapendi nyama wala wali.

### Maelezo muhimu

- **Viunganishi**

Viunganishi ni maneno yanayofanya kazi ya kuunganisha. Huonyesha uhusiano baina ya neno na neno, fungu moja la maneno na fungu jingine au sentensi na sentensi.

**Mifano zaidi ya viunganishi:**

1. **au:** Nunua shati jekundu **au** jeupe!
2. **bali:** Kuzungumza Kiswahili si vigumu, **bali** ni rahisi.
3. **basi:** Nilitaka sana kula piza, **basi** nilienda mkahawani.
4. **bila:** Basi lilifika **bila** mama.
5. **ijapo: Ijapo** nitakufa, sitakubali uwongo.
6. **ila:** Kila mtu amelala **ila** baba.
7. **ingawa:** Anapenda familia yake **ingawa** yeye ni maskini.
8. **kama:** Ninahitaji televisheni **kama** hii.
9. **kisha:** Nesi huyu ni mfupi **kisha** ni mwembamba.
10. **kwa sababu:** Nilienda darasani **kwa sababu** nilitaka kusoma Kiswahili.
11. **kwamba; kuwa:** Ninaona **kwamba** / **kuwa** mnyama huyu ni mkali.
12. **lakini:** Uwera anacheka **lakini** Kabera analia.
13. **na:** Nitanunua kalamu **na** daftari dukani.
14. **pamoja na:** Nilienda dukani **pamoja na** mama yangu.

15. **tena:** Sijui mtoto huyu, **tena** sijamwona.
16. **wala:** Hakuna mchele **wala** unga.
17. **isipokuwa:** Wanafunzi hawa ni wazuri **isipokuwa** Gakwaya.
18. **ikiwa: Ikiwa** nitashinda mtihani, nitapata digrii yangu.

### KAZI YA 5

**Tumia viunganishi mwafaka kuunganisha sentensi zifuatazo:**

1. Hana mbele. Hana nyuma.
2. Musabyimana alikula staftahi. Musabyimana alienda ofisini.
3. Alimsogelea adui yake. Hakuwa na hofu.

## 22.4. Matumizi ya lugha: Umuhimu wa fasihi katika jamii

### KAZI YA 6

**Shirikiana na wenzako kusoma maelezo yafuatayo na kujibu maswali hapo chini.**

Fasihi ni sanaa ya lugha, inayoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu: matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake na mazingira yake. Inawasilisha ujumbe unaohusu maisha ya jamii kwa kutumia lugha. Umuhimu wake ni kuburudisha jamii kwa kufurahisha, kutumbuiza, kusisimua hadhira, n. k.

Fasihi inaelimisha hadhira kuhusu mambo tofauti yanayoikumba jamii, mazingira, n.k. Inadumisha maadili katika jamii kwa kuelekeza, kuonya na kunasihi hadhira jinsi ya kufuata mwelekeo unaokubalika katika jamii. Inaunganisha jamii kwa kuleta umoja wa watu pamoja na kukuza lugha kwani tungo zote za fasihi hutumia lugha na mbinu nyingi zake. Fasihi inahifadhi mila, tamaduni na itikadi za jamii kutokana na kuwa kazi za fasihi huambatanishwa na desturi mbalimbali za jamii husika. Vipera vingi vya fasihi huwachochea hadhira kufikiri sana ili kupata suluhisho, na vilevile fasihi inakuza uwezo wa kufikiri.

**Maswali:**

1. Ni nini maana ya fasihi?
2. Kuhusu maadili, fasihi inasaidiaje jamii?
3. Kwa kuegemea kifungu hiki cha habari ulichokisoma, eleza umuhimu wa vipera vingi vya fasihi kwa hadithi/jamii.

## 22.5. Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

### KAZI YA 7


**Shirikiana wa wenzako na kujadili kuhusu** "Namna fasihi inavyoweza kuendeleza umoja wa Wanyarwanda."

## 22.6. Kuandika: Utungaji wa kifungu cha habari

### KAZI YA 8

**Tunga kifungu cha habari ambacho kina vielezi na viunganishi kuhusu mada** "Matumizi mazuri ya fasihi yanahitajika katika kutayarisha Rwanda ya kesho.

# SOMO LA 23: TANZU ZA FASIHI YA KISWAHILI



## KAZI YA 1

**Tazama mchoro hapo juu kisha ujibu maswali haya:**

1. Unaona nini kwenye mchoro huu?
2. Wahusika unaowatazama kwenye mchoro huo wanafanya nini?

## 23.1. Kusoma na ufahamu: Tanzu za fasihi ya Kiswahili

**Soma kifungu cha habari ambacho kinafuata kisha ujibu maswali hapo chini.**

Fasihi ni sanaa muhimu ya matumizi ya lugha inayohusiana na tungo kama hadithi, maigizo, mashairi, tungo fupi kama methali, vitendawili, nahau, tamthilia na kadhalika. Kimsingi, fasihi hugawanyika katika tanzu kubwa mbili kuu: fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi simulizi hutegemea zaidi usemi kuliko fasihi andishi, ambapo fasihi andishi hutegemea zaidi maandishi kwa kiasi kikubwa. Katika fasihi simulizi kuna tanzu ndogo ambazo huitwa vipera. Kipera cha kwanza ni hadithi ambayo ni mtungo wa fasihi simulizi wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha ya nathari kwa kusudi la kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Msimulizi wake huitwa fanani au mtambaji.

Hadithi huainishwa kulingana na wahusika: khurafa, hekaya, mighani na mazimwi, au kulingana na maudhui: usuli, visasili na mtanziko. Kwa maelezo zaidi, khurafa ni hadithi ambazo wahusika ni wanyama, hekaya ni hadithi yenye mhusika mmoja (kama vile Sungura) ambaye huwa mjanja kuliko wenzake, mighani ni hadithi za mashujaa, mazimwi huwa na wahusika majitu au mazimwi, usuli huelezea chanzo cha jambo au hali fulani, visasili huelezea asili au chimbuko la jamii au mambo ya kiada k.v mauti, ndoa na tohara, ambapo mtanziko humwacha mhusika katika hali ya kutojua chaguo linalofaa. Kila achagualo lina matukio mabaya.

Maigizo kwa wakati wake ni sanaa ambayo watendaji huwa ndio wahusika. Wahusika ndio huzungumza katika sehemu zao mbalimbali. Aina zake ni michezo ya kuigiza ambapo watendaji huiga maneno na matendo ya wahusika mbele ya hadhira, miviga ambayo ni sherehe mbalimbali katika jamii fulani ambapo watu hujumuika kulingana na tamaduni zao, ngomezi yaani sanaa ya ngoma ambapo midundo mbalimbali ya ngoma hutumika kuwasilisha jumbe mbalimbali, ulumbi ama uwezo wa kipekee wa kuzungumza mbele ya hadhira, vichekesho yaani sanaa ya kutoa vihadithi vifupi au sentensi zenye uwezo wa kuwafanya wasikilizaji wacheke na maonyesho ya sanaa yaani maonyesho

yanayohusisha watu wa jamii au kundi fulani wanaoonyesha taaluma, ujuzi au sanaa yao kwa watazamaji.

Mashairi ni tungo za kisanaa zenye mpangilio maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika na kuwasilisha ujumbe fulani. Mashairi hugawika katika makundi mawili: mashairi ya kimapokeo au mashairi arudhi ambayo hutungwa kwa kufuata au kuzingatia sheria na kanuni za utunzi kama vile kuzingatia vina, idadi fulani ya mizani, mishororo na vipande vya mishororo, na mashairi huru ambayo hutungwa bila kuzingatia kanuni hizo. Aina za mashairi ni kama ngonjera yaani shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi na tenzi yaani mtungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani.

Tungo fupi hujumlisha sanaa simulizi zinazoundwa kwa maneno machache. Tungo hizo ni kama methali ambazo ni tungo fupi za sentensi moja zinazotoa funzo fulani kwa njia ya mafumbo. Methali hutumika kwa minajili ya kutoa funzo kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Kuna pia vitendawili: tungo fupi ambazo huwa na swali fupi na jibu kwa makusudi ya kupima ufahamu wa hadhira kuhusu mazingira yake. Anayetoa kitendawili huulizia swali kwa kutoa maelezo mafupi yanayorejelea umbo la kitu hicho, sauti, harufu au kukifananisha na kitu kingine ambapo anayejibu huhitajika kufikiria haraka na kujibu kwa moja au maneno mawili. Kuna tena nahau yaani mafungu ya maneno ambayo hutumika kuleta maana tofauti na maana halisi ya maneno yaliyotumika.

Fasihi andishi: Ni sanaa ambayo hutumia maneno yaliyoandikwa kupitisha ujumbe. Ina tanzu kuu hizi: hadithi fupi yaani kazi andishi ya fasihi isiyokuwa ndefu sana, riwaya au kazi andishi ya fasihi ambayo huwa ndefu kuliko hadithi fupi, tamthilia yaani kazi andishi ya fasihi inayowasilisha mchezo wa kuigiza, na mashairi yaliyochapishwa. Tamthilia huwa na aina ya mapenzi, ya kihistoria, ya kisiasa, ya kidini, ya kiuchumi, n.k. Lakini hizi zote huangukia katika makundi makuu haya: tanzia maana yake tamthilia iliyojaa huzuni ndani yake, matokeo ya vifo na mateso makali. Mwisho wake huwa ni wa masikitiko au maanguko na hasara kubwa kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Pengine huitwa simanzi au trejedia.

Kuna ramsa au tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, maneno yaonyeshayo ujinga, n.k. Lengo lake ni kukosoa jamii, watawala na tabia mbaya za watu binafsi. Aina hii huitwa tena tamthilia cheshi au komedia. Mwisho wake kuna tanzia – ramsa: ni mchezo wenye sifa za ramsa, lakini ndani ya uchekeshaji wake mna tanzia kama vile kifo cha mhusika mkuu au kuanguka kwa jamii. Pengine huitwa trejikomedia. Fasihi andishi hupitishwa kwa njia ya maandishi tena ni mali ya mtu binafsi. Inatumia mbinu za lugha za sanaa na

haiwezi kubadilishwa.

## KAZI YA 2

**Maswali ya ufahamu**

1. Kwa kuegemea kifungu cha habari, nini maana ya fasihi?
2. Andika tanzu kubwa za fasihi.
3. Fasihi simulizi ina tanzu ndogo au vipera gani? Vieleze vipera hivyo.
4. Taja aina za tamthilia.
5. Taja sifa nne za fasihi andishi.
6. Eleza aina za mashairi.
7. Mwenendo wa vitendawili ni upi?

## 23.2. Msamiati kuhusu tanzu za fasihi

## KAZI YA 3

**Tunga sentensi zenye maana kwa kutumia maneno yafuatayo**

1. Hadithi
2. Maigizo
3. Mashairi
4. Methali
5. Vitendawili
6. Nahau
7. Tamthilia
8. Tanzu
9. Sanaa
10. Vipera

## 23.3. Sarufi kuhusu matumizi ya aina za maneno

## KAZI YA 4

**Taja aina za maneno yaliyopigiwa msitari katika sentensi hizi:**

1. **Haki ya Mungu!** Mimi sikuiba.
2. Rais wetu, **oyee!**
3. **Ala!** Vipi mtu kujitia wazimu namna hii!
4. **Afanaalek!** Nimesahau kabisa kuwa leo ni siku ya kuzaliwa kwangu.
5. **Huree!** Tumemaliza kujenga nyumba.

**Maelezo muhimu kuhusu vihisishi**

Vihisishi ni maneno ambayo yanaonyesha hisia za mtu za ndani kwa mujibu wa hali na muktadha. Yanaonyesha hangaiko la moyo ama kudokeza mguso wa moyo ama hata wa akili. **Kwa mfano**: Kuna kukosekana kwa matumaini, furaha, huruma, mshangao, hasira, wasiwasi na kadhalika. Ili kuonyesha baadhi ya mahangaiko haya, yapo maneno fulani yanayotumiwa.

**Mifano ya baadhi ya vihisishi ni hii ifuatayo:** hmmm! Ebo! eti! alaa! basi, afanaalek!, ajabu!, pole!, sasa!/tena!, haki ya Mungu!, ewe!, inshallah!, ohoo!, kumbe!, oyee!, hata!, salaale!, la hasha!, alhamdulillah!, maskini! lo!, haya!, na kadhalika.

## KAZI YA 5

**Tumia vihusishi vifuatavyo kukamilisha sentensi:** Sawa na, karibu na, baada ya, hadi, moja kwa moja

1. Kitabu hiki ni ..................................... kile.
2. Alikimbizwa hadi ..................................... nyumba yake.
3. ....................................... kula chakula tulinawa mikono.
4. Walisoma .................................. usiku wa manane.
5. Alienda ................................... kwa mwalimu mkuu.

### Maelezo muhimu kuhusu vihusishi

Vihusishi ni maneno yanayoonyesha uhusiano baina ya watu au vitu viwili au zaidi. Kuna vihusishi vya kuonyesha mahali, wakati na hali.

**Mifano:**

1. **kabla ya:** Kabla ya kuimba nitakunywa chai.
2. **baada ya:** Nitarudi nyumbani baada ya kusoma somo la Kiswahili.
3. **nje ya:** Niko nje ya nyumba.
4. **ndani ya:** Nimeweka vitabu vyangu ndani ya kabati.
5. **juu ya:** Miti ilianguka juu ya nyumba.
6. **chini ya:** Viatu vyangu viko chini ya meza.
7. **baina ya:** Niambie tofauti iliyopo baina ya fasihi andishi na fasihi simulizi.
8. **kati ya:** Mimi hunywa pombe kati ya Ijumaa na Jumapili.
9. **mbele ya:** Vitabu vipo mbele ya dirisha.
10. **nyuma ya:** Paka analala nyuma ya kochi.
11. **karibu na:** Ninaishi karibu na mji wa Butare.

12. **mbali na:** Nyumba yako iko mbali na pwani.
13. **kando ya:** Wilaya ya Nyamasheke iko kando ya ziwa Kivu.
14. **mpaka; hadi:** Nitasoma kutoka saa nne hadi saa tano asubuhi.
    Nilikimbia kutoka saa nane mpaka saa tisa mchana.
15. **kisha:** Ninaenda sokoni kisha nitarudi nyumbani.
16. **tangu; toka:** Nilisoma Kiswahili tangu saa mbili hadi saa tano asubuhi.
    Yeye atakaa hotelini toka Jumanne mpaka Ijumaa.
17. **katika:** Tunazungumza katika Kiswahili.
18. **miongoni mwa:** Kagina amechaguliwa kuwa miongoni mwa wanafunzi watakaohudhuria mkutano wa viranja wa darasa tarafani kwetu.
19. **usoni pa :** Anaishi usoni pa duka.
20. **pembeni mwa :** Anakaa pembeni mwa darasa.
21. **ubavuni mwa :** Mtoto amekaa ubavuni mwa mama.

## 23.4. Matumizi ya lugha: Nafasi ya fasihi ya Kiswahili katika jamii

### KAZI YA 6

**Shirikiana na wenzako kusoma kifungu na kujibu maswali ya hapo chini**

Fasihi na jamii ni kitu kimoja kwani pasipo jamii hakuna fasihi na hakuna jamii bila fasihi. Mambo haya yanategemeana na kukamilishana. Fasihi ni zao la jamii na mielekeo yake kwa sababu inatokana na jamii, tena wanafasihi ni wanajamii, na yale wayawasilishayo kwa kutumia fasihi chanzo chake ni jamii na huwafikia wanajamii pia.

Msanii huiga mambo au matendo yanayofanywa na wanajamii wenzake na kuyawasilisha kwa wanajamii hao akionyesha uzuri na ubaya wake.

Fasihi ya Kiswahili kama fasihi yoyote ile, ina nafasi ya kuelimisha wanajamii. Ili kukamilisha jukumu hili, fasihi inaonya, inarekebisha, inafahamisha, inatoa mawaidha na kadhalika. Kupitia kwa fasihi hii, wanajamii husimuliana matukio, huelekezana kimaadili, huelimishana, hudumisha ushirikiano, huonyana na kupeana taarifa za makuzi na malezi kwa njia ya kisanaa. Leo hii, uwasilishaji wa fasihi simulizi umekumbwa na mabadiliko makubwa kutokana na t**eknolojia ya habari na mawasiliano,** **a**mbapo mitandao ya kijamii imekuwa jukwaa kubwa kabisa la mawasiliano ya kila siku, na mitandao hiyo hutumia maandishi. Hata hivyo, fasihi ya Kiswahili ilienda sambamba na mageuzi kwenye jukwaa hilo.

Katika ulimwengu wa mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa kutumia vyombo vya kisasa kama vile mtandao wa tovuti na simu, utakuta kwamba fasihi pia inabadilika kwa kuendana na mabadiliko ya kila siku, kwa sababu hakuna wakati wowote ule ambapo fasihi haina nafasi kubwa katika mchango wa maendeleo ya jamii.

**Maswali:**

1. Kwa nini fasihi ni zao la jamii?
2. Fasihi ina nafasi gani katika jamii?
3. Katika mabadiliko ya sayansi na teknolojia fasihi inafanyaje?

## 23.5. Kusikiliza na kuzungumza

### KAZI YA 7

**Sikiliza jinsi mkufunzi anavyosoma kifungu cha hapo juu kisha usome kwa sauti kubwa ukimwiga.**

## 23.6. Kuandika

### KAZI YA 8

**Katika aya mbili, andika mtungo wenye kutumia vihusishi na vihisishi.**

## TATHMINI YA MADA YA KUMI NA MOJA

1. Nini maana ya fasihi?
2. Tanzu kuu za fasihi ni zipi?
3. Andika tanzu ndogo (vipera) za fasihi andishi.
4. Eleza vipera vya tamthiliya.
5. Nafasi ya fasihi katika jamii ni ipi?
6. Taja aina za maneno ambayo yamepigiwa msitari katika sentensi zifuatazo:
   a. Nitakuonyesha kitabu changu kipya kesho.
   b. Mchungaji anahubiri mbele ya Wakristo.
   c. Angalia! Kalamu yako imeangukia chini ya meza.
   d. Timu ya Amavubi oyeee!
   e. Musaniwabo na Beneyo wanakwenda sokoni.
7. “Fasihi ina nafasi kubwa katika jamii ya Wanyarwanda.” Jadili. (Usizidi ukurasa mmoja)

# Marejeo


1. **Waititu, F. na Wenzake (2008).** *Kiswahili Fasaha. Kitabu cha Mwanafunzi. Kidato cha tatu*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Nairobi, Kenya.
2. **TUKI (2004).** *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Toleo la pili.* Oxford University Press.
3. **Bakhressa, S. K. na Wenzake (2008).** *Kiswahili Sanifu. Kitabu cha Mwanafunzi. Darasa la Saba*. Oxford University Press, East Africa Ltd, Elgon Road, Upper Hill, Nairobi, Kenya.
4. **Nkwera, F. M. V. (1978).** *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Tanzania Publishing House, Dar Es Salaam.
5. **HARERIMANA, F. (2017).** *Tujivunie Lugha Yetu. Kitabu cha Mwanafunzi, Kidato cha 5*. MK Publishers (R) Ltd. Kigali, Rwanda.
6. **Ndalu, A. E. (2016).** *Masomo ya Kiswahili Sanifu. Kitabu cha mwanafunzi. Kidato cha 2*. Moran (E.A) Publishers Limited.
7. **Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017).** *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 5*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.
8. **Kenya Literature Bureau (2006).** *Kiswahili kwa Darasa la nane. Kitabu cha Wanafunzi*. Kenya Literature Bureau, Nairobi, Kenya.
9. **Ntawiyanga, S. na Wenzake (2017).** *Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Mchepuo wa Lugha, Kidato cha 6*. Longhorn Publishers (Rwanda) Limited. Kigali, Rwanda.
10. **Niyirora, E. na Ndayambaje, L. (2012).** *Kiswahili Sanifu kwa Shule za Sekondari. Kitabu cha Mwanafunzi kidato cha tano*. Tan Prints (India) Pvt. Ltd.
11. *http://learn.e-limu.org/topic/view/?c=207&t=1579*